Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

**Kikao cha Tisa – Tarehe 17 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 80

**Daraja Mbadala – Morogoro Mjini**

**MHE. OSCAR T. MLOKA** aliuliza:-

Kwa kuwa sikuridhika na majibu ya Serikali kwa swali langu Na. 3422 lililojibiwa mapema mwaka huu Bungeni kuwa daraja mbadala kwenye eneo la *Shan-Cinema* nililobainisha kuwa halipo kwenye ramani ya Mji, lakini baada ya kuliwasilisha jambo hilo kwenye Baraza la Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imedhihirika kuwepo kwa daraja hilo pamoja na barabara yake ambayo haijajengwa iliyo mkabala na *Community Centre* kando kando ya Mto huo wa Morogoro:-

Je, Serikali italirejea jibu lake ililotoa Bungeni na kutafuta fedha za kujenga daraja hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Thobias Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swali Na. 3422 Mheshimiwa Mbunge alitaka Serikali kujenga daraja la waenda kwa miguu lililopo *Community Centre* kwa kiwango cha

kupitisha magari ili kupunguza msongamano ulioanza kujitokeza Mjini Morogoro. Wakati nikijibu swali hilo ambalo lilikuwa Na. 2 katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge Novemba, 2002, nilibainisha sababu za kutoweza kujengwa daraja kwenye eneo lililopo daraja la waenda kwa miguu kuwa ni pamoja na zifuatazo:-

- Katika ramani ya Mji sehemu hiyo haionyeshi au haikupangwa iwe barabara;

- Kama daraja lingejengwa pale, ingelazimu *Community Centre* ibomolewe ili kutoa nafasi;

- *Alignment* ya barabara hiyo ni ya hatari kwani italazimu kuwepo na kona ndipo uingie darajani kwa kutokea Mwere.

Aidha, niliishauri Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro pamoja na wakazi wake kulinda daraja la *Shan Cinema* wakati Serikali ikitafuta fedha za kujenga daraja mbadala katika eneo litakaloteuliwa na Halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye ramani ya Manispaa ya Morogoro hakuna barabara inayopita kwenye daraja la waenda kwa miguu bali kuna mwendelezo wa Mtaa wa Kikundi unaokatisha Mtaa wa Nkomo na kuvuka Mto Morogoro na kuungana na barabara inayopita mbele ya Shule ya Msingi ya Mwere. Sehemu hiyo ndipo panatakiwa kujengwa daraja. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imekwishafanya usanifu wa awali wa daraja hili na linakadiriwa kuwa na urefu wa mita 40 na ujenzi wake utagharimu Tsh. 920m/=. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa kushirikiana na Serikali Kuu inatafuta fedha za ujenzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, daraja hili ni jipya na licha ya ombi la awali la Mheshimiwa Mbunge la kujenga daraja la waenda kwa miguu kwa kiwango cha kuwezesha magari kupita, ningependa kurudia kuishauri Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na wakazi wake kuendelea kwa sasa kutunza lile daraja lililopo wakati Serikali inatafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa daraja hili mbadala ni la kukwepesha msongamano uliopo pale *Shan Cinema* na kwa kuwa kazi hii ilipaswa kufanywa na *TANROADS* kwamba wao wana uzoefu wa kujenga madaraja makubwa makubwa yenye gharama kubwa kama hizo, gharama ambazo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro haina uwezo. Je, Waziri atakubaliana na ushauri wangu kwamba ipo haja ya kuzungumza na Wizara ya Ujenzi ili isaidie ujenzi huo kwa sababu wao wana uzoefu wa kutengeneza madaraja makubwa makubwa kama hili na walishawahi kutusaidia katika ujenzi wa barabara ya kuingia Morogoro Mjini kutoka Msamvu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningewaomba watawala wa Manispaa ya Morogoro wapate mtaalam hasa wa madaraja na *Engineer* wa

madaraja wa kukadiria daraja hili ambalo tunaambiwa ni sh. 900m/=. Mimi linanitisha sana kwamba bei hii ni kubwa mno. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, kitu kingine kizuri ni kwamba Manispaa ya Morogoro ijenge hoja baada ya kupata mtaalam hasa wa makadirio sahihi ya daraja, ijenge hoja ya kupeleka TAMISEMI halafu TAMISEMI watawasiliana na Wizara ya Ujenzi tuone tunaweza kufanya nini.

Na. 81

**Barabara ya Hotel i – Tatu – Lihimalyao**

**MHE. OMAR M. MWENDA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Hoteli Tatu – Pande hadi Lihimalyao ni muhimu sana kiuchumi hasa kwa zao la korosho na kwa kuwa fedha za *Road Toll* zinazotengwa huko Wilayani hazitoshi kuitengeneza barabara hiyo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuongeza fedha za kuwezesha kumaliza matengenezo ya barabara hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kutomalizika kwa barabara hilo ni kuanguka kiuchumi kwa wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mohamed Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara ya Hoteli Tatu-Mkazambo-Pande-Lihimayao yenye urefu wa kilomita 48 ni sehemu muhimu sana kiuchumi kwa maeneo husika na inasaidia sana katika usafirishaji wa mazao ya wakulima hasa zao la korosho ambalo ni zao kuu la biashara katika maeneo haya.

Barabara hii imekuwa na matatizo makubwa ya kupitika kipindi cha mvua kutokana na aina ya udongo na mfinyanzi uliopo sehemu inapopita barabara hiyo. Aidha, mvua inaponyesha barabara hujaa tope zito na kusababisha utelezi.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza matatizo ya mawasiliano katika barabara hii Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imekuwa ikiifanyia matengenezo ya muda maalum pamoja na matengenezo ya sehemu korofi kufuatana na upatikanaji wa fedha kama ifuatavyo:-

Kubwa katika jambo lote hilo ni kwamba fedha hizo ambazo zimekuwa zikipatikana ni zile ambazo hazitoshelezi kwa kiasi cha kuridhisha kutengeneza barabara yote. Hata hivyo ofisi yangu itajaribu kadri itakavyoweza kwa kushirikiana na Halmashauri ili tuweze kumaliza tatizo hilo katika kipindi kinachokuja kwa kuzingatia na uwezo wa bajeti utakaopatikana.

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa maeneo haya wamekerwa sana na barabara hii hatimaye sasa wanafanya michango mbalimbali ya kutaka kuitengeneza barabara hii. Je, Serikali sasa itatoa tamko rasmi kuwaambia wananchi hawa ili wasivunjike moyo? (*Makofi*)

Pili, kwa kuwa amehakikisha katika jibu lake la msingi kwamba pesa hazitoshi. Je, waziri yuko tayari kuongeza pesa? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwapongeze sana wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Mwenda, tena kwa dhati kabisa kwa kazi nzuri ambayo wameionyesha na ndio maana nimesema unapoona juhudi kama hizi ni jukumu la Serikali kutafuta kila njia kujaribu kutatua tatizo hili ambalo linawapa kero kubwa sana.

Lakini kama nilivyosema fedha hazitoshi, ninachoweza kuwahakikishia wananchi hawa ni kwamba tutajitahidi kwa ushirikiano wa karibu na Halmashauri hii tuweze kupata kwa kweli ufumbuzi ambao utapunguza kabisa matatizo ya wananchi.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi amesema kuwa barabara hii ina udongo wa mfinyanzi na kwa kuwa kiukweli ni kwamba si eneo lote toka Hoteli Tatu mpaka Pande ina udongo wa mfinyazi ni kama *stretch* ya kilomita ishirini tu. Je, Serikali haiwezi kuwahakikishia wananchi hawa ikakwangua udongo wote ule wa mfinyanzi ikatuwekea changarawe ili kuhakikisha usafiri katika sehemu hizi korofi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kwa hali ya kawaida pengine hizo kilomita 20 zenye udongo wa mfinyanzi ikaonekana pengine gharama zake zinaweza kuwa ni ndogo kiasi kwamba Serikali iweze kutoa kauli, lakini mambo haya ni ya kitaalam yanahitaji Wahandisi kuweza kutwambia *exactly* tunachohitaji ni nini. Naomba nimhakikishie tu Mama Watondoha kwamba jambo hili tunalitambua na kwa kweli kama nilivyosema tutajitahidi sana kujaribu kuondoa kero hii katika eneo hili. Urefu ni kilomita 48 tu lakini linasumbua karibu kwa miaka mingi.

Na. 82

**Mradi wa Kusambaza Maji Vijijini**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI (K.n.y. MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna mradi mkubwa wa kusambaza Maji Vijijini kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia:-

Je, ni lini mpango huo utaanza kutekelezwa Mkoani Kagera?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji na Usafiri wa Mazingira Vijijini unatekelezwa katika Wilaya 12 kwa kutumia fedha za mkopo nafuu wa Benki ya Dunia wa dola za Marekani milioni 26.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2004/2005, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa mradi huu ungepanuliwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ingezihusisha Wilaya 38 zaidi na kuzifanya Wilaya za mradi kufikia 50. Awamu ya pili ilikuwa ihusishe Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya maandalizi ya upanuzi wa mradi huu imeonekana kwamba kuna haja ya kubadilisha mfumo wa utekelezaji wa mradi ili uwe *program* ambayo itashirikisha wafadhili wengi zaidi na kutekelezwa katika Wilaya zote nchini.

Ili kufanikisha ushiriki wa wafadhili mbalimbali, *Program* ya Taifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini imetayarishwa katika mwaka wa fedha 2004/2005. *Program* hii inayolenga utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira nchini kote tayari imekuwa ikijadiliwa na wadau mbalimbali wakiwemo wafadhili. Lengo ni kuwa fedha za kutekeleza *program* ya maji zitumwe moja kwa moja Wilayani kutoka Wizara ya Fedha ili kupunguza urasimu na kuongeza kasi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu unalenga katika kutuwezesha kufikia malengo ya Taifa ya Milenia (*Millennium Development Goals* (*MDGs)* na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (*Development Vision* 2025) na yale ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Spika, Benki ya Dunia tayari imeshatenga dola za Kimarekani milioni 150 kwa ajili ya Sekta ya Maji Tanzania kuanzia Julai, 2006. Fedha hizi zitatumika kwa ujenzi wa miradi ya maji Vijijini na Mijini na pia kwa kuendeleza rasilimali za maji nchini. Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Umoja wa Nchi za Ulaya na Serikali ya Uholanzi, Ujerumani, Japan na Ufaransa nao wamekubali kushiriki katika utekelezaji wa *program* hii. Aidha, majadiliano yanaendelea na wafadhili wengine ili kuhakikisha fedha zinapatikana ifikapo Julai, 2006.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa miradi midogo midogo imeainishwa katika Wilaya zote nchini ikiwemo Wilaya ya Bukoba Vijijini kwa lengo la kuitekeleza mapema ili kuondoa kero ya maji kwa wananchi. Baadhi ya miradi hii midogo midogo imetekelezwa katika mwaka wa fedha 2004/2005. Aidha, mwezi Julai, 2005 maandalizi ya miradi mikubwa inayohitajika usanifu wa kina yataanza katika Wilaya zote nchini zikiwemo Wilaya zote za Mkoa wa Kagera, ili ujenzi uanze mara tu fedha zitakapopatikana mwezi Julai, 2006.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo Wizara yake inajitahidi sana katika kushughulikia tatizo la maji. Sasa naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mkoa wa Kagera una tabia inayofanana, una mvua zinazotosheleza na nyingi katika mwaka mzima na kwa kuwa wanawake na watoto ndio wengi ambao huathirika na kuchota maji sehemu za mbali. Je, katika mkakati huu wa Benki ya Dunia kusaidia mradi wa Maji Vijiji na Mijini Serikali itakuwa tayari kusaidiana na akinamama kujenga visima vya maji kila nyumba ili kuweza kukinga yale maji ya mvua inayonyesha mwaka mzima?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa maeneo mengine yapo mbali na wanaishi watu na ni karibu na misitu na mbuga za wanyama na watu hao bado wanahitaji kusaidiwa. Je, Serikali itakuwa tayari kusaidiana nao kuchimba visima vifupi na virefu ili kuweza kuondokana na tatizo la maji?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Ruth Msafiri, kwa jinsi anavyofuatilia shughuli za maji katika Jimbo lake.

Lakini pili, kama tulivyosema kwenye sera, Wizara itashirikiana na wadau wote katika kupanga na kuanzisha miradi. Kwa hiyo, tutawashirikisha hao akinamama kadri inavyowezekana na kuangalia nini kifanyike kama ni kisima, bwawa au bomba tutaangalia tutakapofika kwenye eneo la mradi wenyewe.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mpango huu wa Maji Vijijini na Mijini ni mpango mzuri na kwa kuwa Wizara nyingi zimeweka kipaumbele katika Wilaya mpya ikiwemo ya Kilolo. Je, Wizara hii sasa imeweka mikakati gani kuhakikisha Wilaya zote mpya zinapewa kipaumbele katika suala la maji? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Mwamoto ni mmoja wa watu wanaofuatilia sana miradi yao ya maji katika Majimbo yao. Ni kama nilivyosema katika maelezo yangu kwamba, tunajitahidi kuhakikisha miradi inapatikana nchi nzima sio lazima Wilaya iwe mpya. Kipaumbele kipo katika suala la kuhakikisha maji yanapatikana Mijini na Vijijini ili kutekeleza malengo ya Kitaifa na Kimataifa. (*Makofi*)

Na. 83

**Uagizaji wa Soya**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipokuwa ikijibu Swali Na. 44 Bungeni, tarehe 5 Novemba, 2002 ilisema kuwa imeamua kuagiza soya toka nje ya nchi na kwamba haitatozwa ushuru:-

(a) Je, kuagiza soya toka nje ya nchi pamoja na kwamba haizalishwi kwa kiwango kikubwa hapa nchini, Serikali haioni kuwa ni kitendo cha kudidimiza wakulima wa hapa nchini?

(b) Je, kufanya hivyo ni kuisadiia nchi itakayoingiza soya hapa Tanzania?

(c) Je, Serikali inaweka mikakati gani ya kuwahamasisha wananchi ili kuongeza uzalishaji wa soya kwa kipindi hiki ambapo inahitajika sana badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali kuagiza na kuondoa ushuru kwa zao la soya ni kumsaidia mwananchi mfugaji wa Tanzania kuboresha kipato chake kwa kuongeza ubora wa mazao ya kuku yatakayokuwa na ubora unaokidhi haja ya soko. Hata hivyo, msamaha wa kodi au ushuru ni kwa muda tu mpaka hapo hali ya uzalishaji itakapokuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, soya kutoka nje ya nchi ni ile ambayo imekwishaandaliwa kitaalam na kuondolewa vimeng'enyo hasi (*inhibitors*) vinavyozuia kupatikana kwa viini lishe muhimu (*trypin amino acids*). Hapo nyuma na kwa muda mrefu hatukuwa na uwezo wa kusindika soya hapa nchini. Hata hivyo, hivi sasa ipo mashine ya kusindika soya iliyopo Dar es salaam ambayo haijaanza kufanya kazi kwa kuwa uzalishaji wa soya nchni bado ni mdogo. Mashine hiyo ina uwezo wa kusindika soya tani 300,000 kwa mwaka, wakati soya inayopatikana haifikii hata asilimia moja ya uwezo wa mashine hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la swali Na. 44 la tarehe 5/11/2002, mahitaji ya soya kwa ajili ya kutengeneza vyakula vya mifugo ni tani 150,000. Aidha, uzalishaji wa soya hapa nchini kwa mwaka ni tani 596.8 tu. Kutokana na takwimu hizi inaonyesha kwamba

uzalishaji hautoshelezi kabisa na hivyo kuwa na haja ya kuagiza soya kutoka nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina nia yoyote ya kuzinufaisha nchi za nje zinazoingiza soya hapa nchini bali ni kuwezesha uzalishaji wa mazao ya mifugo yenye viwango bora na yatakayokidhi ushindani wa kibiashara. Kadhalika, kufanya hivyo kunawasaidia pia wafugaji wa hapa nchini kupata vyakula bora vya mifugo.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula katika kuhamasisha kilimo cha soya kwa wingi hapa nchini. Punde uzalishaji utakapoimarik,a na kutosheleza mahitaji yetu, Serikali itahakikisha soya ya humu nchini inanunuliwa kwanza kabla ya kutoa vibali vya kuagiza soya toka nchi za nje. Kwa kufanya hivyo mkulima wa Tanzania atanufaika kwa kupata soko zuri.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge tusaidiane kwenye juhudi zetu za kuhamasisha kilimo cha soya na ikiwezekana tushiriki wenyewe ili tuweze kupunguza au kuacha kabisa kuagiza zao hili kutoka nje ya nchi yetu. (*Makofi*)

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza. La kwanza, wanawake wa Tarafa ya Chilangala ambao walishalima huko nyuma walipata hasara ya kutupa soya. Kwa kipindi hiki leo Waziri anasema nini kuhusu wale wanawake? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili, je, Waziri haoni kwamba kuendeleza hiyo dhana ya kuchukua soya kutoka nchi za nje ni kudhoofisha uchumi na kuwafanya hao wanawake wakose soko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri unasema nini juu ya hawa wanawake? (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hawa wanawake wa Chilangala naendelea kuwahimiza walime soya. Nami nahawakikishia kwamba soko la soya lipo, tatizo la soko la soya halipo nchini, tatizo ni kwamba soya iliyopo haitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nasema kwa nini tunaagiza soya kutoka nje, niliwahi kueleza Bunge letu kwamba wakati fulani baadhi ya wachinjaji wa kuku hapa nchini, kuku wa Tanzania alikuwa na ladha ya samaki badala ya ladha ya kuku kwa sababu wanalishwa dagaa nyingi zaidi kuliko soya. Ndio maana tukasema lazima tuwasaidie, tuagize soya kutoka nje ili kuku wetu awe na ladha ya kuku na aweze kushindana katika soko la kuku hapa nchini.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri kwamba soya inahitajika na bahati nzuri mashine ambayo inahusika na usindikaji wa soya ipo Dar es Salaam.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa wakati umefika soya iagizwe ipelekwe kwenye maduka yanayouza soya nikimaanisha mbegu ya soya ili wananchi waweze kuhamasika akiwemo na mama Wejja ambaye ni mkulima mkubwa ili tuweze kupata soko kubwa na soya iweze kupatikana katika nchi hii? Mheshimiwa Waziri anasema nini?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli Mheshimiwa Wejja ni mmoja wa wakulima wakubwa kule Kiteto.

Nampongeza sana kwa jitihada zake hizo. Namhimiza aendelee kufanya bidii na sisi tupo tayari kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuhakikisha kwamba zao la soya linafanyiwa kampeni ya kutosha na linalimwa vya kutosha hapa nchini. (*Makofi*)

Na. 84

**Ujenzi wa Madaraja Katika Barabara ya Tunduma - Sumbawanga**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa madaraja muhimu katika barabara kati ya Tunduma na Sumbawanga yamekamilika hadi Mpui na kwa kuwa bado madaraja machache kati ya Mpui kupitia Kaengesa hadi Sumbawanga Mjini na baadaye hadi Mpanda:-

(a) Je, ujenzi wa barabara ya lami unaweza kuchelewa kutokana na tatizo hilo la madaraja?

(b) Je, Serikali haiwezi kuamua kuanza kazi ya ujenzi wa barabara ya lami wakati madaraja yanajengwa?

(c) Je, katika mpango wa ujenzi wa barabara ya lami itakapofikia Mjini Sumbawanga; kwa nini michoro ya upanuzi wa barabara katika eneo la Mji lisitizamwe pamoja na kuwa na uwezekano wa *Service Road* katikati ya eneo la Mji toka Kizwite hadi enao la Sumbawanga Wenyeji?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa madaraja 11 katika barabara hii ulikamilika tangu mwezi Machi, 2004 na umegharimu kiasi cha Sh. 4.7bn/=. Benki ya Dunia ilitoa sh. 4.3bn/= kama mkopo na Serikali ya Tanzania ilichangia sh. 362m/=. Madaraja haya yamejengwa kwenye njia (*alignment*) ambayo imethibitika kuwa ni ya kudumu kati ya Tunduma, Mpui, Kizwite na Sumbawanga Mjini.

Aidha, madaraja saba yaliyopo kati ya Mpui na Kizwite hayakujengwa chini ya mradi uliotajwa hapo juu kwa kuwa njia ya kudumu katika sehemu hii ilikuwa inategemea kukamilika kwa hatua ya upembezi yakinifu. Upembuzi yakinifu umekamilika tangu mwezi Mei, 2004 kwa gharama ya sh. 437m/= kwa fedha kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, upembuzi yakinifu umekamilika. Hatua inayoendelea ni ya kumtafuta Mhandisi Mshauri ambaye atafanya usanifu wa kina wa ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa kilomita 230 kwa kiwango cha lami. Benki ya Dunia itagharamia usanifu huo. Katika mchakato huu, ujenzi wa madaraja saba umeainishwa ndani ya mradi wa ujenzi wa barabara husika. Hivyo suala la ucheleweshaji wa kazi za barabara halitakuwepo tena.

(b) Kwa kupitia taarifa ya upembuzi yakinifu iliyokwishakamilika, kazi ya ujenzi wa barabara itafanyika sambamba na ujenzi wa madaraja saba yaliyobakia.

(c)Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya barabara unafuata taratibu za msingi zinazohusisha upembeuzi yakinifu, usanifu wa kina na hatimaye ujenzi.

Hatua tuliyofikia hadi muda huu bado inaturuhusu kufanya marekebisho yoyote ambayo tutayaona ni lazima kuyafanya kwa maeneo yaliyo muhimu. Ushauri wa ujenzi wa *Service Roads* katikati ya eneo la Mji wa Sumbawanga umezingatiwa. Wataalam wa Wizara ya Ujenzi wakishirikiana na Mhandisi Mshauri watayafanyia kazi mapendekezo hayo. *(Makofi)*

Hata hivyo ni vema nikatoa tahadhari kwamba kuna uwezekano wa kubomoa majengo na nyumba ndani ya Mji. Hili litabidi tulipime kwa makini hasa ukizingatia uzito wake katika bajeti ya Taifa. Lakini vile vile kwa wananchi husika wanaoishi katika barabara hii. Tutapenda ushauri mkubwa utoke Manispaa ya Sumbawanga ili watu wawe wameridhika tunapoanza bomoa bomoa.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri ambayo yanatia moyo kwamba sasa barabara

itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kutokana na urefu wa barabara kutoka Tunduma hadi Sumbawanga itabidi wakati wa ujenzi wa lami atumie njia yoyote tupate makandarasi zaidi ya wawili au watatu ili wajenge wakati huo huo madaraja pamoja na kuweka lami kwa wakati mmoja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, je, Waziri anafahamu kwamba kutokana na ubovu wa barabara ya kutoka Tunduma hadi Sumbawanga kwa kipindi cha mwaka uliopita zaidi ya tani 32,000 za mahindi zimekwama kwa sababu wanunuzi binafsi hawakuwepo isipokuwa *SGR* peke yake ambayo nayo imeshindwa kusafirisha mahindi hayo? Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanza kutoa angalau kipaumbele kwa kuongeza fedha zaidi kusaidia ujenzi wa barabara hiyo haraka iwezekanavyo ili kuukomboa Mkoa wa Rukwa kutokana na umaskini uliokithiri?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Paul Kimiti kwa kufuatilia ujenzi wa barabara hii na hasa ujenzi wa kiwango cha lami Mjini Sumbawanga. Yeye anang'ang'ania lami ianze Sumbawanga Mjini ije huku na mimi nafikiri ni suala la msingi na kwa sasa muda umefika kwa Sumbawanga kupata lami Mjini na kwa barabara hii itapata.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida kwa barabara ndefu yoyote siku hizi Wizara ya Ujenzi haipangi mkandarasi mmoja tena. Inapanga makandarasi zaidi ya wawili kwa vipande vifupi vifupi ili mmoja akikwama mwingine atakuwa amekamilisha kipande hicho. Kwa hiyo, hilo lisikupe wasiwasi kabisa, tutakapoanza watakuwepo makandarasi wengi na kwa kawaida mkandarasi wa madaraja yeye ni tofauti sana na hawa wanaojenga barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubovu kukwamisha mazao. Mwaka huu mvua zilikuwa nyingi na za ghafla na za kutisha. Kwa hiyo, barabara nyingi ziliharibika pamoja na barabara hii. Nakiri kwamba barabara hii iliharibika, lakini suala la kuongeza pesa inategemea bajeti. Kwa hiyo, tutaangalia kwenye bajeti tuone tumetenga fedha kiasi gani, lakini nadhani zitakuwepo fedha za kutosha za kukarabati barabara hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hili ni tatizo maalum la Mkoa wa Rukwa. Kwa hiyo, nitampa nafasi Mheshimiwa Lephy Gembe, pamoja na Mheshimiwa Margareth Bwana.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika swali la msingi Mheshimiwa Paul Kimiti ameitaja Mpanda na Mpanda ni maarufu na ni Mji wa siku nyingi na kwa sababu ni maarufu kwa madini na mbuga za wanyama. Je, mpango wa kujenga barabara ya lami kutoka Sumbawanga mpaka Mpanda ukoje?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mpanda ni maarufu na Mpanda ina kila aina ya vivutio mbuga za wanyamapori, biashara na mazao

lakini kupanga ni kuchagua. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge astahimili kwanza tutengeneze barabara ya lami kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga halafu baadaye tuelekee huko Mpanda.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kufuatia swali la msingi lililoulizwa na Mheshimiwa Paul Kimiti na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba suala la mchoro na upembuzi yakinifu umegharimu karibu shilingi milioni 400. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutueleza hizi gharama zote za shilingi milioni 400 zimefanya shughuli gani na kwa nini upembuzi yakinifu unakuwa na gharama kubwa kiasi hicho? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nilipoteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi nilishtuka sana kwa mahesabu kama haya, nilikuwa ninadhani fedha hizi zinaibiwa. Lakini baadaye nilipofika mimi mwenyewe na kuangalia hizo kazi zinavyofanywa, kwa hakika fedha hizo zinafanya kazi kubwa sana. Usanifu wa barabara maana yake wanachora mchoro inchi moja hadi nchi moja nyingine ya barabara hiyo kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga na kumweleza mtengenezaji wa barabara ambaye hatakutana na huyo mchoraji kwamba lazima afuatilie ramani hiyo ambayo wao wameichora. Hapa patakuwa na daraja, hapa patakuwana tuta na hapa patakuwa na kalvati. Hivi ni vitu ambavyo ni vya kiutaalam na kweli vinatumia fedha nyingi sana. Kwa hiyo, hizo fedha zinatengeneza kazi hasa ya barabara. *(Makofi)*

**Na. 85**

**Usafi Kandokando ya Barabara Kuu Nchini**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wakala wa Barabara *TANROADS* wanafanya kazi nzuri ya kusimamia mikataba ya makandarasi nchini, matengenezo ya barabara na ufyekaji wa nyasi kandokando ya barabara kuu nchini, lakini kazi hii ya ufyekaji nyasi hufanywa na wanaume tu:-

(a) Je, kuna makandarasi wangapi wa kike na ni wangapi kati ya hao wamepewa tenda?

(b) Je, ni lini wanawake watapewa nafasi ya kufyeka nyasi kando kando ya barabara kuu nchini ili nao waondokanae na umaskini?

(c) Katika mikataba hiyo; je, kuna kipengele chochote kinachotamka watu wa jinsia zote wahusishwe, na kama jibu ni “Sivyo”. Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuleta marekebisho ya sheria husika Bungeni ili ifanyiwe marekebisho ili kuondoa kasoro hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kampuni za ujenzi ambazo zimesajiliwa zikiwa zinamilikiwa na wanawake ni 47. Aidha, hatuna takwimu rasmi kwa nchi nzima ya kuonyesha kwamba ni kampuni ngapi za aina hiyo zimepewa kandarasi za ujenzi. Tutajitahidi kuweka kumbukumbu ili siku za baadaye tuwe na orodha rasmi kwa nchi nzima ya makampuni yanayomilikiwa na wanawake yanayopewa kazi za kandarasi za ujenzi. Lakini hii inaweza vile vile kusababisha makampuni ya akinamama ya ujenzi ama yakakosa kazi ama yakapewa kazi kwa sababu yatakuwa yanabaguliwa. Sisi tungependelea makampuni ya ujenzi yaombe kama makampuni ya ujenzi na yapate kazi.

(b) Zabuni za kufyeka nyasi huwa zinatangazwa na makandarasi mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanavijiji waishio kandokando ya barabara husika huomba kazi hizo. Wakala wa Barabara mara nyingi umekuwa ukiwapa kipaumbele wananchi waishio karibu na barabara husika ili kuwasaidia kuwapa ajira na kupunguza umaskini. Hivyo akinamama ambao wana uwezo vilevile wakiomba hupewa kazi hizo.

(c) Mara zote kazi za ujenzi zinapotangazwa, kinachosisitizwa ni uwezo wa kampuni katika kazi inayotakiwa kufanyika.Lakini pia huwekwa vipengele vya kusema kuwa kampuni zinazomilikiwa na wanawake zenye uwezo zinashauriwa kuomba. Wizara yetu inazingatia sana suala la jinsia na kwa sababu hiyo imekuwa inajitahidi sana katika miradi yake ya ujenzi kupitia makandarasi, kuwashawishi kuwaajiri pia wanawake ambao wana ujuzi sawa na wanaume katika kazi zao bila shaka mmeshawaona wanawake wanaoendesha mitambo mbalimbali kama mtambo wa kushindilia barabara *(vibration rollers*), mtambo wa kukata udongo *(graders),* wapima darubini *(Surveyors*) na kadhalika.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mradi wa *TASAF* ulionyesha mfano mzuri sana wa kuwashirikisha akinamama kwenye maeneo ya kutengeneza barabara. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuiga mfano huo wa *TASAF* kwa kuhakikisha kwamba akinamama wanashirikishwa kwa wingi?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba kuna makampuni 47 tu, na nina uhakika hayo makampuni yapo katika Mikoa 11 tu ya Tanzania. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuanzisha kitengo katika Wizara yake cha kuhakikisha basi anapata takwimu sahihi za kujua makampuni ya wanawake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, *TASAF* na Wizara ya Ujenzi na utaratibu wa utendaji wake wa kazi ni vitu viwili tofauti. *TASAF* mkopo unatoka kwenye kijiji kwa madhumuni maalum ya kujenga shule ama barabara na hivyo wanavijiji wanashiriki. Ama wana utaalam ama hawana wanashiriki, lakini mojawapo atakuwa mtaalam kuwepo hapo kuwasaidia. Tukitoa tenda ya kutengeneza barabara ina masharti mengi sana ambayo lazima yafuatiliwe na hizo ni fedha ambazo lazima zihesabiwe kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kusema kwamba tufuate mtindo wa *TASAF,* tutoe fedha tu ili wanakijiji na wananchi washiriki tutashindwa ku-*account for* fedha hizo zimetumika vipi na sisi haja yetu ni kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika kwenye barabara na inayotakiwa na kwa utaratibu unaotakiwa. Barabara za *TASAF* hazichorwi, barabara zetu lazima zichorwe, mojawapo ya tofauti hiyo. Kwa hiyo, mimi sioni uwezekano kabisa kwamba tutafuata mfano wa *TASAF,* ila tutawashirikisha akinamama kwa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, makampuni yapo 47 tu, je, kuna uwezekano wa kuanzisha kitengo cha wanawake katika Wizara ya Ujenzi. Ningependa kutoa taarifa hapa kwamba kipo kitengo cha wanawake katika Wizara ya Ujenzi. Bahati nzuri kitengo hiki kilianza na kukamilika wakati Mheshimiwa Anna Abdallah, alipokuwa Waziri wa Ujenzi na sasa hivi na sisi tunakiendeleza na kipo na kinahudumia wanawake na kinakusanya ma-*engineer* wote wanawake na kimeanzisha kampuni maalum ya wanawake. Kwa taarifa yenu Mwenyekiti wa Makampuni ya Makandarasi ni mwanamke, tena Mtanzania. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba katika Wizara ya Ujenzi kuna kitengo maalum cha Wananawe; na kwa kuwa amesema kwamba ni makampuni machache tu ambayo yanamilikiwa na wanawake. Kwa vile kuna vikundi vingi vya Kiuchumi vya Wanawake Vijijini na hizi barabara zinapita kule Vijijini. Je, hicho kitengo kilichoundwa cha masuala ya wanawake kinafanya jitihada gani za kuwaelimisha wanawake hasa vikundi vya kiuchumi ili waweze kuunda makampuni ya ujenzi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, makampuni ya wanawake ambayo yapo Tanzania si machache yapo 47, haya yangeweza kabisa kama yangekuwa na uwezo mkubwa wa kufanya kazi nzuri. Kipo kitengo cha wanawake kinachofanyika na kitengo hiki ni kwenda Mkoa hadi Mkoa na mara nyingine kwenye Wilaya na mara nyingine tunawambia waende Vijijini kuwaelimisha wanavijiji na hasa

akinamama jinsi gani ya kuanzisha vikundi, jinsi gani ya kuomba kazi za barabara na jinsi gani ya kukusanyika na kuanzisha kampuni. Inapofikia hatua ya kuanzisha kampuni sasa huo ni utashi na uwezo wa vikundi maalum. Hata kama wakitaka kuomba msaada wanapata msaada. Lakini mara nyingine akinamama wanarudi nyuma wenyewe kwa kuogopa kuanzisha kampuni. Zipo sheria za kuanzisha kampuni sasa huwezi kuzivuruga hizo lazima uende kwenye sheria hizo uzikamilishe.

Na. 86

**Viwanda vya Kuchambulia Pamba**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa viwanda cha kuchambulia pamba (*Ginneries*) vimechakaa sana kutokana na ukosefu wa fedha katika viwanda hivyo; na kwa kuwa katika miaka ya 1980 Serikali ilivipokea viwanda hivyo kutoka kwa wafadhili wa Uholanzi na kufanyiwa ukarabati:-

Je, Serikali inaweza kuwapa mikopo ambayo itarejeshwa baada ya miaka 3 au 4 ili viwanda hivyo vifanyiwe ukarabati na kuwezesha ushirika kuwa na nguvu za kuwahudumia vyema wakulima wa pamba kwa nia ya kupambana na umaskini vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika miaka ya 1980, Serikali ilikopa fedha kutoka kwa wahisani kwa ajili ya kuvifanyia ukarabati baadhi ya viwanda vya kuchambua pamba vilivyokuwa vinamilikiwa na Vyama Vikuu vya Ushirika ili kuongeza uwezo wa kuchambua pamba. Uamuzi huo ulifikiwa kutokana na pamba kutochambuliwa kwa wakati kutokana na kuwapo kwa uwezo mdogo wa kuchambua pamba, hali ambayo ilisababisha kuingiliana kwa misimu ya pamba na kushuka kwa ubora na usafi wa pamba. Wakati huo uwezo wa kuchambua pamba ulikuwa chini ya marobota 300,000 kwa kipindi cha miezi 9.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuanzishwa kwa sera ya uchumi wa soko, uwezo wa kuchambua pamba umeongezeka kutoka marobota 300,00 katika kipindi cha miezi 9 katika mwaka wa 1993/1994 hadi zaidi ya marobota 750,000 katika kipindi cha miezi 6 katika mwaka wa 1999/2000.

Hali hii inatokana na wafanyabishasra kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vipya. Idadi ya viwanda imeongezeka kutoka viwanda 33 mwaka wa 1980 hadi viwanda 58 mwaka wa 2005.

Kiwango cha juu cha uzalishaji wa pamba kilikuwa katika msimu wa 2004/2005 ambapo marobota 640,000 yalizalishwa. Sababu zilizopelekea Serikali kukopa kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kuchambua pamba kwa sasa hazipo.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika vinashauriwa kufanya uchambuzi wa kina wa kila kiwanda cha kuchambua pamba ili kubaini mahitaji na gharama za kuvikarabati. Uchambuzi wa aina hiyo utaviwezesha Vyama vya Ushirika kuamua hatua zenye manufaa za kuchukuliwa.

Vyama hivyo vitaweza kumaua kuchukua mikopo ya benki kugharamia ukarabati au kuingia ubia na wafanyabiashara wa pamba wenye uwezo wa kuvikarabati au kuvikodisha kwa watu ambao miongoni mwao mambo mengine watavifanyia ukarabati au yote hayo yakishindikana na iwapo wanachama wataamua hivyo, kuviuza.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kutafuta fedha za kukarabati viwanda vya kuchambua pamba vya Vyama vya Ushirika. Jukumu hilo ni la Vyama vya Ushirika vyenyewe na kama vinahitaji ushauri wa Serikali, Serikali iko tayari kuvishauri ipasavyo. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kiwanda cha Singida ni kati ya viwanda hivyo ambavyo Mheshimiwa Leonard Derefa ameuliza na sasa hivi kiwanda hicho kilishauzwa na Chama cha Ushirika kwa mfanyabiashara binafsi; na kwa kuwa mfanyabiashara huyo baada ya kukinunua kiwanda hicho sasa hakifanyi kazi na kimekufa kabisa. Je, Serikali haioni sasa kwamba iweze kusaidia kukirudisha kiwanda hicho ili wakulima wa Mkoa wa Singida waweze kukimiliki tena na kuendelea kulima pamba? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Mheshimiwa Hamisi Nguli kiwanda aliuziwa huyo mfanyabiashara na kwa hiyo kimetoka kutoka Chama cha Ushirika na kwenda kwa mtu binafsi. Kwa hiyo, kama itabidi Serikali iingie hapo ni lazima kwanza Chama cha Ushirika kifanye utaratibu wa kukikomboa kiwanda hicho kutoka kwa yule waliyemuuzia na kutoka hapo mawasiliano yafanyike baina ya Chama cha Ushirika na Serikali. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIAM F.SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kama alivyouliza swali Mheshimiwa Leonard Derefa maeneo ya viwanda vya kuchambulia pamba ni maeneo muhimu sana katika uhai na hatma ya zao la pamba na kwa wakulima wa zao la pamba. Sasa je, kwa nini mpango unaoelezwa na Serikali usifanyike haraka iwezekanavyo kwa lengo la kuvishauri Vyama vya Ushirika viweze kukamilisha mipango hiyo na kwa kusukumwa na Serikali viweze kweli kuboresha viwanda hivyo vya kuchambulia pamba ikiwa pamoja na *ginnery* za Buyangu, Nyamiriro, Nyakalilo katika Wilaya ya Sengerema ili hatimaye viwanda hivyo viweze kuwa viwanda vidogo vidogo vya kutengeneza nyuzi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi uwezekano wa kufanya hayo yote inabidi sisi viongozi na hasa sisi Waheshimiwa Wabunge ambao tuko karibu sana na wananchi tuwashauri. Kwa hiyo, jibu nililotoa ni tegemeo langu lipitie katika Bunge hili Tukufu na Mheshimiwa Leonard Derefa, maarufu kama *Brother* alipeleke jibu hilo na kwa kupitia kwa Mheshimiwa Dr. William Shija, ninaomba tuwashauri Wanaushirika na Vyama vingine vyote nchini wafanye hivyo na hiyo ndiyo azma ya Serikali.

Na. 87

**Bei Nzuri kwa Zao la Tumbaku**

**MHE. LEPHY B. GEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Tumbaku ni zao la biashara kwa wakulima wa Wilaya ya Mpanda na limeanza kulimwa katika maeneo hayo miaka ya 1970 lakini bei ya manunuzi ya zao hilo ni ya chini sana:-

Je, ni lini Serikali itaanza kununua Tumbaku hiyo toka kwa wakulima ili waweze kupata bei nzuri, badala ya kuwaachia wafanyabiashara binafsi kujinunulia zao hilo kwa bei ya chini sana ikilinganishwa na gharama za uzalishaji?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Lephy Benjamin Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Mpanda ni moja ya Wilaya kadhaa hapa nchini inayolima zao la pamba na Tumbaku kama zao la biashara kuanzia miaka ya 1970 na kwamba miaka mingi ya nyuma, Serikali chini ya mfumo wa uchumi wa Soko Hodhi iliweza kununua mazao makuu yote ya biashara ikiwa ni pamoja na zao la Tumbaku.

Lakini kufuatia kuanzishwa kwa mfumo wa uchumi wa soko nchini, Serikali ilijiondoa katika shughuli za moja kwa moja za biashara, ikiwa ni pamoja na shughuli za ununuzi wa mazao ya kilimo na upangaji wa bei za mazao hayo likiwemo zao la Tumbaku. Katika mfumo huu wa soko huru, ununuzi wa mazao umeachiwa sekta binafsi ikiwa ni pamoja na Vyama vya Ushirika na Vikundi vya aina nyingine vya wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali haiwezi tena kuanzisha mpango wa kununua zao la tumbaku kwani kufanya hivyo itakuwa ni sawa na kurejea kwenye mfumo wa uchumi hodhi ambao tulikwishaachana nao.

Mheshimiwa Spika, chini ya mfumo huo wa uchumi wa soko na Sera ya Soko Huria iliyoanzishwa na Serikali, bei ya kununulia tumbaku kwa mkulima imekuwa

ikijadiliwa na kupatiwa muafaka katika Vikao vya Halmashauri ya Tumbaku, ambayo inajumuisha Wawakilishi wa Wakulima, Wanunuzi wa tumbaku na wadau wengine wa zao la tumbaku nchini. Katika majadiliano ya bei ya tumbaku kwa mkulima, mambo mbalimbali muhimu huzingatiwa, ikiwa ni pamoja na gharamza za uzalishaji kwa mkulima na kiwango cha ubora wa tumbaku. Katika vikao hivyo vya Halmashauri ya Tumbaku, Serikali hushiriki katika majadiliano hayo kama mshauri kwa pande zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku na kwa kuwashirikisha wadau wa sekta ya Tumbaku itaendelea kuweka mazingira muafaka ya uzalishaji na biashara ili kuongeza tija na kiwango cha ubora wa tumbaku kwa kuwapa wakulima mafunzo ya kilimo bora cha tumbaku pamoja na matumizi ya mbegu na mbolea bora zaidi. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya majadiliano ya bei baina ya wakulima na wanunuzi katika Halmashauri ya Tumbaku ili kuhakikisha mkulima anaendelea kupata bei ya haki kulingana na ubora wa tumbaku yake. Na kama ambavyo imekuwa ikifanya, Serikali itaingilia kati kutatua migogoro yoyote inapotokea katika majadiliano baina ya wakulima na wanunuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu tulizonazo mwenendo wa bei ya tumbaku ya mvuke kwa kilo zilizojadiliwa na kuafikiwa katika Halmashauri ya Tumbaku unaonyesha kuwa malinganisho ya bei hizo na gharama za uzalishaji ziliwapatia faida wakulima. Kwa mfano, katika misimu ya 2002/2003 na 2003/2004 gharama za uzalishaji wa kilo moja ya tumbaku ya mvuke zilikuwa shilingi 482.20 na shilingi 458.60 sawia ikilinganishwa na bei ya mkulima ya wastani wa shilingi 750.80 na shilingi 881.50 sawia katika vipindi hivyo. Wazalishaji wa tumbaku yenye ubora wa juu walinufaika zaidi kwa kuuza kwa wastani wa bei ya shilingi 1,119/= mwaka 2002/2003 na shilingi 1,231/= mwaka 2003/2004. Faida kwa mkulima huongezeka pale anapoongeza tija kwa kuzalisha tumbaku nyingi katika eneo dogo.

Kwa hiyo, Serikali inawahimiza wakulima kuwa ili waweze kupata bei nzuri na faida kubwa hawana budi kuzalisha tumbaku nyingi yenye kiwango cha juu cha ubora na Serikali itaendelea kuwasimamia chini ya utaratibu uliowekwa.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa makampuni yameachiwa kufanya biashara mbili. Kwanza, yanawakopesha mbolea wakulima wa tumbaku. Lakini pili, wananunua tumbaku. Je, leseni ya makampuni ya tumbaku ni ya kazi zote mbili au ni wanunuzi wa tumbaku peke yake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, suala la wanunuzi kutoa mbolea kwa wakulima ni mapatano kati ya wakulima na wanunuzi hao. Leseni ambayo wanapata wanunuzi hao ni ya kununulia tumbaku. Lakini kutokana na uwezo mdogo wa wakulima wa kupata mbolea wakati wanapokuwa wanaihitaji ndiyo wanafanya mikataba na wanunuzi hao kuwapa mbolea kwa makubaliano kwamba watakapouza tumbaku yao waweze kukata gharama za mbolea ambayo wameitoa.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, Serikali mara nyingi imekuwa inasisitiza kwamba wakulima wanaweza kujikomboa kuondokana na tatizo hili kama wataanzisha mifuko yao wenyewe kupitia Vyama vya Ushirika na mifuko ya aina nyingine na kwa hiyo wanunue mbolea moja kwa moja badala ya kuwategemea hao wanunuzi binafsi.

**SPIKA:** Bado tunayo maswali mawili ya msingi, kwa hiyo naomba tuendelee.

Na. 88

**Upungufu wa Mahakimu Nchini**

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE (K.n.y . MHE. ROBERT K. MASHALLA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mahakama ni chombo kinacholinda maslahi ya Taifa na haki za wananchi; na kwa kuwa Mahakama zetu hapa nchini zina upungufu mkubwa wa Mahakimu hasa wa Mahakama za Mwanzo, hivyo upungufu huo husababisha msongamano wa kesi ambazo huchukua muda mwingi bila kusikilizwa:-

(a) Je,Serikali katika zama hizi za utawala na haki za binadamu ina mpango gani wa kuboresha Mahakama zetu ili ziwe na uwezo wa kusikiliza kesi na kuzimaliza kwa muda muafaka?

(b) Je, isingekuwa busara kuwachukua vijana wetu wahitimu wa kidato cha nne na cha sita na kuwapeleka chuoni ili baadaye waweze kujaza nafasi zilizokosa Mahakimu zilizopo sasa?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Kaji Mashalla, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mashalla kuhusu kuwepo hali ya upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Nchini. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mashalla kuwa Serikali inalitambua tatizo hilo na inachukua hatua za kulikabili.

Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Mahakama zisizokuwa na Mahakimu kutembelewa na Mahakimu kutoka Vituo vingine.

(ii) Kuajiri Mahakimu wapya.

(iii) Kuendeleza mkakati wa kupanua Chuo cha Lushoto.

(iv) Kuwachukua vijana wa Kidato cha nne na sita kujiunga na Chuo cha Lushoto.

(v) Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Sekta ya Sheria ya 2005/2006 – 2007/2008 wenye makusudi ya kuongeza idadi ya Mahakimu.

Kuhusu mipango ya kuboresha Mahakama zetu ili ziwe na uwezo wa kusikiliza kesi na kuzimaliza kwa muda muafaka, hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(i) Kuimarishwa kwa Kamati za Kusukuma Mashauri (*Case Flow Management Committee*) kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa kesi za jinai zilizokwama au kuchelewa kusikilizwa.

(ii) Kuwapangia mashauri Majaji na Mahakimu tangu mwanzo wa mashauri yanapofunguliwa ili waweze kuyafuatilia vizuri zaidi (*Individual Calender System*).

(iii) Kuendeleza utaratibu wa Usuluhishi Muafaka nje ya Mahakama (*Alternative Dispute Resolution* (*ADR).*

(iv) Kutilia mkazo suala la ukaguzi wa Mahakama ili Mahakama ngazi za juu ziweze kusimamia utendaji kazi wa kila Hakimu kwa ukaribu.

(v) Kuimarisha mafunzo na pia kuwapatia vitendea kazi muhimu Mahakamani vikiwemo vitabu vya sheria na ripoti za kesi ili kuboresha uwezo wao wa kumudu kesi nyingi walizonazo.

(vi) Kuimarisha Mahakama kwa kuiongezea uwezo kifedha na nguvukazi ili iweze kumudu majukumu iliyonayo kwa ufanisi zaidi.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia nafasi niulize swali moja tu la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nilitaka niulize tu kwamba kwa kuwa tuna Majaji wachache sana katika nchi hii na milundikano ya kesi zilizopo kwenye Mahakama zetu ni zile zinazosubiri Majaji kwa mfano, kesi za mauaji zinasubiri sana Majaji. Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati pengine tufanyie marekebisho sheria hii ili tuwaruhusu Mahakimu wa Mikoa au hata wa Wilaya waweze kusikiliza kesi kama hizo zinazowasubiri Majaji? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli idadi ya Majaji haitoshelezi, lakini kasi ya kuwateua Majaji imeongezeka hivi karibuni na nadhani katika Awamu ya Nne suala hili itabidi litupiwe macho karibu zaidi. Utaratibu wa kufanya Mahakimu waweze kusikiliza kesi za mauaji badala ya Majaji, utaratibu huo upo na tumekuwa tukiutumia.

**MHE. ALI SAID SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kwa mujibu wa swali la msingi kuna ucheleweshaji mkubwa sana wa kesi katika Mahakama zetu za kawaida; na kwa kuwa baada ya miezi 3 ijayo kutakuwa na shughuli ya uchaguzi jambo ambalo linadhihirisha kwamba kutakuwa na ongezeko kubwa la kesi za kisiasa na kesi cha uchaguzi; na kwa kuwa Katiba zetu zote mbili kifungu namba 21 kinaruhusu kuanzishwa kwa Mahakama za Katiba. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni muda muafaka wa kuanzisha Mahakama hii ili kesi zote zinazohusu uchaguzi zikahamishwa katika Mahakama hii ili kuhakikisha kwamba zinamalizwa katika muda muafaka? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mahakama ya Katiba siyo Mahakama yenyewe, Mahakama ya Katiba ina shughuli zake. Lakini pamoja na hayo ningependa tu kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka 1995 baada ya Uchaguzi Mkuu tulivyokuwa na kesi nyingi kipaumbele kilipewa kesi hizi ambazo zilikuwa na utata katika masuala ya uchaguzi. Kwa hiyo, kama suala hili litajitokeza basi itabidi tuweke utaratibu wa kesi hizi baada ya Uchaguzi kusikilizwa mapema inavyowezekana.

Na. 89

**Umri wa Kugombea Urais**

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Nchi yetu, sharti mojawapo la mtu kuweza kugombea Urais ni kuwa na umri usiopungua miaka 40; na kwa kuwa kwa hivi sasa wastani wa maisha ya Mtanzania ni kati ya miaka 40 na 45:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupunguza umri huo ili mtu aweze kugombea Urais akiwa na umri usiopungua miaka 30 kwa lengo la kuwapa haki vijana kulitumikia Taifa lao katika ngazi zote za Uongozi?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Nafasi ya Rais, ambaye kwa mujibu wa Ibara ya 33(2) ya Katiba ya Nchi yetu ndiye Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali, na Amiri Jeshi Mkuu, anahitajika kwamba mtu wa kushika madaraka haya makubwa awe ni mtu mwenye ukomavu, busara na uzoefu wa uongozi wa kutosha. Serikali inaamini kwamba pamoja na sifa nyingine

zilizoainishwa, inafaa iendelee kushikwa na mtu mwenye umri usiopungua miaka 40. Hivyo, Serikali haioni umuhimu wa kulipunguza sharti la umri wa miaka isiyopungua 40 lililowekwa na Katiba kwa mtu kustahili kugombea nafasi hiyo. Zipo nafasi nyingi sana za uongozi ambazo vijana walio chini ya umri huo wanaweza kuzifanya na zinawawezesha kulitumikia Taifa. Uongozi katika nafasi hizo utawapa uzoefu kuwafanya waweze kuimudu kwa mafanikio nafasi hiyo muhimu watakapokuwa na umri wa miaka 40 au zaidi.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliongoza Taifa letu akiwa na chini ya umri wa miaka 40 na pia hivi sasa umri wa Mtanzania kuishi ni chini ya miaka 40. Wastani wa Mtanzania umri wake wa kuishi miaka 40 kutokana na mambo mengi yanayomzingira kijana. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hii ni sababu tosha ya kuteremsha umri?

Mheshimiwa Spika, pili, Watanzania matarajio yao kwa Rais ajae ni kutamka hivi kuanzia leo ni mwisho wa rushwa, bei ya pamba iwe angalau shilingi 500/= kwa wakulima na kwa sababu Serikali yetu inasema haya mambo hayawezekani na haiwezi pia kupandisha mishahara kwenda shilingi angalau 200,000/=. Je, akitokea Mtanzania anayeamini kwamba anaweza haya na yuko chini ya umri wa miaka 40 kama Muttamwega Mgaywa, Serikali iko tayari kuleta mabadiliko ya Katiba ili aweze kugombea na kutimiza ahadi ya Watanzania? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza la kumfananisha Mwalimu na kijana wa sasa hivi mwenye umri wa miaka 38. Niseme tu kwamba Mwalimu alikuwa ni mtu wa aina yake na kweli itachukua muda mrefu na pengine karne nzima kuweza kumpata mtu wa namna hiyo. Yaani mtu mwenye akili, busara, mkakamavu kama Mheshimiwa Mbunge alivyotoa sifa zenyewe katika swali lake la msingi.

Leo masharti ya kumpata Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba awe amefanya kazi sio chini ya miaka 15. Kwa hiyo, nazungumzia Mwanasheria Mkuu ambaye ana umri zaidi ya miaka 40. Hivyo hivyo kwa Jaji Mkuu na kwa Majaji na sembuse kwa Rais na dunia ya sasa hivi ni *more complex* kuliko wakati ule wa Mwalimu. Lakini nimalizie tu tulipokuwa tunamtafuta mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi kulikuwa kuna sifa 13 na zikaongezewa 5 na Mwenyekiti. Sasa Mheshimiwa Mgaywa kama unazo sifa hizo jaribu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nadhani na swali la pili nimejibu hapo hapo?

**SPIKA:** Ndiyo !!! Waheshismiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha namaswali yamekwisha sasa matangazo ya vikao vya Kamati kwa leo. Ziko Kamati tatu ambazo zimepangiwa kufanya vikao. Ya kwanza ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Janguo anaomba kuwatangazia wajumbe

kwamba leo Ijumaa tarehe 17 kutakuwa na kikao katika chumba Na. 219 ghorofa ya 2 mara baada ya kipindi hiki cha maswali.

Kamati ya pili, ni Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omar Kwaangw', anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo ya Huduma za Jamii kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 17 Juni, 2005 saa 4.30 asubuhi katika chumba Na. 133.

Kamati ya tatu, ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Mgana Msindai, Mwenyekiti anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuwa kutakuwa na kikao leo tarehe 17 Juni, 2005 saa 5.00 asubuhi ghorofa ya 2 chumba Na. 231. Tangazo la pili, linahusu semina ya kesho.

Naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho tarehe 18 kutakuwepo na Semina Kuhusu Umuhimu wa Sheria za Kazi na Uhusiano Wake na Upunguzaji Umaskini Nchini katika ukumbi huu huu wa Bunge kuanzia saa 3.00 asubuhi kama kawaida. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa Kamati tatu zinakutana mara baada ya maswali endapo kuna mjumbe wa Kamati yoyote kati ya hizo tatu ameomba kuchangia naomba aniarifu ili badala ya kuitwa akaonekana hayupo nimpangie nafasi nyingine au labda Jumatatu au mapema. Naomba tufanye hivyo. Mwisho wa matangazo Katibu endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006
### Ofisi ya Waziri Mkuu

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba aliyoitoa na kwa namna alivyoiwasilisha. Lakini pia nikumbuke kuwapongeza wasaidizi wake, Mawaziri, Manaibu Waziri, vile vile na watendaji wakuu na hata wale wadogo katika ofisi yake ambao wamemsaidia kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla pia sijaweza kuzungumza zaidi naomba na mimi pia nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya Hayati Abu Kiwanga kwa kupotelewa na mpendwa wao lakini pia hata wapiga kura wa jimbo la Kilombero.

Mheshimiwa Spika, mimi pia kama Mwana-CCM napenda nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kumteua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa mgombea wa Urais kwa tiketi ya CCM na pia Mheshimiwa Ali Mohamed Shein kama mgombea mwenza na hatimaye kuwa Makamu wa Rais. Aidha, nikipongeze chama kwa kumteua Mheshimiwa Amani Abeid Karume kama mgombea wa Urais kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo mimi napenda kuitambua na kuipongeza kazi kubwa ya Serikali katika kipindi hiki ambayo imefanywa katika kuinua hali na kiwango cha elimu kwa msaada au kwa mpango wa MMEM. Mpango wa MMEM umetekelezwa kwa mafanikio makubwa lakini matokeo yake yakawa kama vile tunavyosema kwamba unapotatua tatizo moja basi unatengeneza lingine. Watoto wamesoma wengi wa kutosha na wamefaulu kwa kiwango kikubwa kumaliza Shule ya Msingi. Lakini utakuta kwamba wengi walibaki walikosa mahali pa kwenda kwa sababu ya Shule za Sekondari zimekuwa ni chache mno, kwa hiyo wengine wamebaki.

Lakini pia nipongeze hatua za Serikali kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake kwamba angalau kila Kata ya nchi hii iweze kujenga Shule ya Sekondari. Mpango huu umepokelewa vizuri sana katika maeneo yote nchi nzima na hata Mkoani Kagera yeye alitembelea baadhi ya Wilaya na aliweza kujionea Shule za Sekondari nyingi zikijengwa huko vijijini, nyingi alizizindua nyingine aliweka mawe ya msingi na pia kuweza kuchangia katika kuendeleza ujenzi wa shule hizo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa hizi shule za Kata ni nzuri sana. Lakini mpango huu unahitaji kuboreshwa zaidi. Kuboresha mazingira ya shule hizi za sekondari katika Kata. Kama tunavyojua nchi yetu ni kubwa sana na maeneo mengi yako mbali sana vijijini. Kwa hiyo mazingira yake kwa kweli hayafanani fanani vizuri kama Shule za Sekondari zingine tunazozifahamu. Kwa hiyo, watoto kweli watasoma lakini zipo hitilafu nyingi ambazo zitawakumba watoto hawa kwa sababu watoto watakuwa wanatoka eneo hilo hilo, kwa hiyo mazingira hayatatofatiana sana na zile Shule za Msingi.

Kwa hiyo mimi nilikuwa nafikiri kwamba Serikali katika huu Mpango wa MMES basi ifanye mahesabu vizuri zaidi maana shilingi 7 milioni zinazotolewa kwa chumba kimoja mimi naona hazitoshi. Kwa sababu shule hizi ili kuzifanyia mazingira mazuri ya watoto kusoma na hata walimu wakaweza kuvutika kwa sababu tumeona tatizo lingine linalozikumba shule hizi walimu wengi wanakataa kwenda katika shule hizo kwa sababu mazingira yake ni ya vijijini sana. Kule hakuna umeme, shule zile hazina maji, kwa hiyo mimi nilikuwa nadhani Serikali iangalie utaratibu wa kuweza kuzifanya hizi shule ziwe na mazingira mazuri ya kujifunzia na kufanyia kazi hasa kwa walimu. Tumekwishashuhudia kabisa katika shule nyingine kwa mfano shule ya Nyakahura ambayo sehemu ilipo si pabaya sana lakini walimu wanatoroka wanasema huku ni vijijini sana kwa sababu walimu nao wanahitaji mahali pazuri penye umeme, maji ili waweze kusoma na kufundisha vizuri.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kuwepo na mpango hata kama si umeme huu lakini angalau umeme wa *solar, generator* hata zile ndogo ndogo lakini watoto waweze kujifunza vizuri zaidi. Lakini pia kwa watoto wa kike shule hizi zina matatizo kwa sababu watoto wanalazimika kutembea mwendo mrefu kati ya kilomita 5 au 6 wakati mwingine hata 10. Kwa sababu watoto na wazazi sasa wanayo kiu ya elimu wanapenda kusoma na wazazi wamekuwa na mwamko mkubwa sana kusomesha watoto wao wa kike. Lakini mwendo huu mrefu unawaathiri sana watoto wote lakini zaidi wale wa kile maana hata *lift* tu ya baiskeli inaweza ikamtoa mtoto kwenye msimamo wake. Kwa hiyo,

mimi nilikuwa naomba Wizara ya Elimu iandae utaratibu wa kuona kama katika baadhi ya shule, ipange baadhi ya shule ziwe ni shule za kulala wasichana ili wapate muda mzuri zaidi wa kujifunza na kuweza kuepukana na matatizo mbalimbali ambayo yanaweza kuwakumba katika huu mwendo mrefu. Isitoshe pia kwamba kwa kweli kutembea kilomita 6 kwenda shule na kilomita 6 kurudi hata ule uchovu wa mwili basi hautaweza kumsaidia mtoto kujifunza vizuri maana saa zote anawaza kutembea. Anapokuwa darasani anaweza leo sijui nitatembeaje kufika nyumbani.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba Wizara au Serikali nzima iangalie kuziboresha hizi shule ziwekewe miundombinu ambayo itawavutia watoto maana mtu hujifunzi kwa kukaa darasani tu lakini unaweza kujifunza kwa kukutana na watu wengine na kwa kuangalia mazingira tofauti na yale uliyoishi tangu ulipozaliwa. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani kwamba uwepo utaratibu hata wa kuwachanganya watoto watoke hata Wilaya nyingine waende hata Kata nyingine. Mtoto atoke labda Rufiji aje basi akasome Kagera akakutane na watoto wa Kagera aone wale wanaishije kama vile sisi tulivyokuwa tunasoma shule unatoka Ngara unakuja kusoma Bwiru, unatoka Bwiru unakuja kusoma Tabora basi ulikuwa una uwezo wa kukutana na watoto wengine na kujifunza kutoka kwao na wao wakajifunza kutoka kwako. Kuliko mtoto mazingira aliyozaliwa anasoma Shule ya Msingi na hapo hapo akaendelea na Sekondari kwa hiyo abadilishe mazingira. Kwa hiyo, mambo atakayojifunza ni yale ya darasani tu na yenyewe atayapata nusu nusu kutokana na mazingira yale ya kuja kukosa miundombinu niliyoyazungumzia hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa napenda kuzungumzia ni kuhusu maendeleo ya Mkoa wa Kagera. Maendeleo ya Mkoa wa Kagera yanaathiriwa na matatizo mbalimbali. Mawasiliano ya Mkoa wa Kagera ni ya shida, shida sana na haya yanatokana moja kutokana na uwanja wa ndege wa Bukoba. Uwanja wa ndege wa Bukoba ni wa shida mno. Mvua zikinyesha basi ndege hazitui wala ndege haziondoki kama ilikuwepo pale. Hili ni tatizo ambalo limekuwa wimbo kwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera miaka yote tumelia mwisho tulipoona kulia hakutoshi tukaona afadhali tuanze kuimba sasa sijui tufanye nini. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba Serikali sasa iwe na masikio kama ilisikia vilio ikanyamaza lakini angalau basi wimbo tunaoimba sasa basi waweze kusikia uwanja wa ndege wa Bukoba ufanyiwe matengenezo mazuri ili ndege ziweze kutoa na kuondoka wakati wowote. Lakini pia hata ndege nyingine kubwa ziweze kutua mimi kwa hatua hii nalipongeza Shirika la *Precision Air* kwa kweli limekuwa ni mkombozi wa mkoa wetu kwa ajili ya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linalotukumba ni huu ubovu wa reli ya kati ambao hauwezeshi mizigo, bidhaa kupakiliwa kutoka Dar es Salaam kwenye mabehewa badala yake yanapakiliwa Dodoma. Hili limesababisha bei za bidhaa nyingi hasa bidhaa za ujenzi kupanda bei mno. Wakati mfuko wa saruji unanuliwa shilingi 7,000/= au 8,000/= Dar es Salaam, Mkoa wa Kagera tunaununua shillingi 15,000/= na vile vile Mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa hata Tabora. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba Serikali iliangalie reli ya kati wakati sambamba na kuangalia mawasiliano ya barabara lakini iangalie reli ya kati kwa kuangalia watu wa Mkoa wa Kagera, Mara, Shinyanga, Mwanza, Tabora na Kigoma. Kwa sababu sisi tunaathirika mno hata watu wanajiuliza

hivi watu tutaendelea namna gani, tutaendelea kuishi katika nyumba za nyasi mpaka lini, tutaishi katika nyumba za udongo mpaka lini, kwa sababu bei ni kubwa sana.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba hilo lisikilizwe na liweze likatekelezwa na hasa ingewezekana katika bajeti hii tunayoizungumzia. Tumelizungumza miaka mingi kabla hata tatizo halijajitokeza hili la reli lakini sasa bei imezidi imekuwa kubwa mno. Sasa watu wanajiuliza hivi sasa tuhame twende Uganda, Rwanda na Burundi matatizo ya kule tutayaweza. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba niwasilishe tatizo hilo Serikalini ili liweze likafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho mimi nilikuwa naomba huduma za jamii ziboreshwe zaidi hasa katika zahanati na mahospitali. Mahitaji yanayohitajiwa kwa ajili ya kuwahudumia akina mama wazazi, watoto na wazee liweze kuangaliwa zaidi kwa sababu hawa watu tunasema kwamba wana haki ya kupata matibabu bure. Lakini haifanyiki hivyo katika baadhi ya hospitali. Sehemu nyingine wanakacha wasema aah !! dawa hakuna au wanasema vifaa hakuna labda *drip* hakuna kwa hiyo mtu anaambulia kwenda kununua. Lakini kununua si wengi wenye uwezo. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba mahitaji haya Serikali ihakikishe kwamba yanapatikana na watu wanapata huduma kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba kama haya mawili niliyozungumzia yataweza kufikiriwa na kuweza kupewa umuhimu unaostahili na naomba nikushukuru tena nikiomba kwamba haya niliyozunguza yatazingatiwa yatapewa umuhimu unaostahili. Naunga mkono hoja Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi natoa rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Marehemu Abu Kiwanga, aliyetutoka hapa naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa sina shukrani kwamba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwani kipindi kilichopita tulipata ajali ya gari ya kwangu *VX* ilipinduka mara nne porini. Kwa kweli Mungu ametusaidia, ametunusuru kwa hiyo hilo nalo nishukuru. Lakini nishukuru vile vile Ofisi yako kwamba kwa kweli vijana walitufuata Muhimbili na kutusaidia pale palipotakiwa kutusaidia nashukuru kwa utawala huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niseme tu machache kuhusiana na Hoja iliyoko mbele yetu hoja ya Waziri Mkuu. Mimi ni mmoja katika Wapinzani ambao waliunga mkono bajeti ya Serikali. Niliunga mkono bajeti ya Serikali! Katika bajeti ambazo tumeunga mkono sisi Wapinzani toka tumeanza miaka hii mitano nimeunga bajeti mbili na bajeti tatu tulizikataa.

Hii bajeti niliunga mkono mia kwa mia kwa sababu moja. Ya kwanza kabisa ni bajeti ambayo ilikuwa na mwelekeo wa kusaidia maskini na ndiyo jambo ambalo

nimefuata hapa. Ya pili Upinzani sio kukataa kila kitu. Upinzani unakataa kile ambacho unaona kwamba hakifai na unatoa sababu zingine mbadala.

Sasa kwa sababu mbadala tulikuwa hatuna kwani bajeti hii ilikuwa na fedha nyingi kutoka nje za wafadhili, bajeti hii ina vitu vingi sana vya kutekeleza ambavyo na mimi nilikuwa na maombi mengi Serikalini ambayo nina ahadi ya Serikali kutekeleza. Kama ningekataa hii bajeti yasingetekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina barua hapa mfukoni ya Waziri wa Ujenzi ananiahidi kujenga barabara ya *Kibosho Road* kwa kilomita 7 sasa ningekataa hii bajeti isingejengwa hiyo barabara.

Kwa hiyo, nilikuwa na haki kabisa ya kukubali hii bajeti na ni bajeti nzuri na nazidi kurudia kwamba hiyo bajeti basi itekeleze yale ambayo tuliyokuwa tumeomba Serikali ifanye kama vile kukamilisha mambo ya umeme, mashule na barabara.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika kuelezea hili jambo la upinzani maana hili jambo la Upinzan lazima nilieleze vizuri zaidi. Ni kwamba nataka nimpongeze Waziri Kigoda kwa hotuba yake jana na Mheshimiwa Beatus Magayane jana alichangia. Kwani mambo aliyosema hapa ambayo nataka watu wayaelewe ni kuhusu hii Elimu ya Siasa ya Vyama vingi.

Mheshimiwa Kigoda alikiri kwamba kwa miaka 40 tulikuwa kidogo kwenye giza sasa tumekwishafungua milango tufanye kazi. Nampongeza kwamba amejua hilo.

Mheshimiwa Magayane alizungumza kwamba wanasiasa wasomee siasa ile shule kwa mfano ya Kigamboni ya watu wa CCM sasa hivi haipo, shule za kufundisha wanasiasa hazipo kwa sasa hivi.

Kwa hiyo nafikiri Waziri Mkuu anasikia kwamba sasa wanasiasa sio utoke tu mahali labda umefukuzwa kazi ukarukia kwenye siasa ukasema wewe ni mwanasiasa. Zile shule zirudi ili watu waweze kujua siasa na tuweze kufanya kazi ya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwamba nataka wanielewe Wabunge wenzangu kwamba Siasa ya Vyama Vingi ni sawa sawa na binadamu na meno. Binadamu ana meno na mwili sasa meno ya chini ndiyo Chama Tawala, meno ya juu ni Upinzani.

Meno hayo hayatafanya kazi kama una ya chini peke yake huwezi kutafuna nyama na utatafuna nyama kama una ya chini na juu ukitafuna hiyo nyama ndiyo mwili unakula ndiyo wananchi. Kwa hiyo, wananchi wanapata faraja kwa kuwa nyama ile imetafunwa na inayotafunwa kwa sababu kuna meno ya juu na ya chini.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana, hata Mwalimu Nyerere alisema hawa, wapinzani wamekubalika asilimia 20 tu. Lakini akasema ni lazima tuwe na haya meno ya

juu tuweze kutafuna hii nyama, wananchi wale, na ndiyo maendeleo yaliyopatikana sasa hivi katika nchi yetu. Tumepata maendeleo makubwa kabisa kwa miaka kumi iliyopita, ni kwa sababu sasa tunatafuna nyama na nyama hiyo wananchi wanakula, wanafurahi, maendeleo yanakuwa makubwa, ni lazima tukubaliane hilo.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye, utawala bora, juzi juzi hapa, ulionekana unashitakiwa, ukaitwa mahakamani. Lakini ni kwa sababu tu ya mtu mmoja ambaye alikuwa na madaraka wa Mahakamani, ambaye amesoma, aliamua neno moja tu kwamba, kesi hii siiwezi lakini akaifuta. Yaani anajua kitu anacho kifanya, sasa kufanya hayo tunaona kwamba mtu mzima ambaye anajua kitu anachokifanya, halafu anafanya makusudi bila kujali athari zitakazowapata wengine. Kwa kweli hilo tuliangalie, na hilo tunalisema hapa kwa sababu huna sababu yoyote ya kusema kwamba, Je hapo hapakutembea rushwa? Kwa sababu mazingira yanaonekana pale, unajua mlango wa kuingilia ni huu unasema hapana hili ni dirisha na sio mlango, na wakati umesomea na umepewa wadhifa huo. Cheo kikubwa, mpaka unaitwa *Resident Magistrate,* aibu.

Mheshimiwa Spika, hayo yamepita, yameamuliwa vinginevyo na Jaji wa Mahakama Kuu na sina haja ya kuendelea na hayo. Lakini ninachosema hapo, katika suala la utawala bora, kweli tuna Mahakama, tuna *legislators* na tuna Serikali Kuu. Sasa tusiwe na madaraka tukayatumia vibaya kwa kuumiza wengine, ukijua kwamba unayatumia vibaya. Hilo ndilo nataka niliseme hapa.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo ninaomba sana Serikali hii iliangalie sana ni kuhusu utendaji wa Wizara. Hizi Wizara, kuna Wizara ya Kilimo, kuna Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maji. Hizi Wizara makao makuu yake yanakuwa Dar es Salaam, kule chini wale waajiriwa wanaotenda kule chini, hawawajui hawa viongozi. Yaani wale kule chini hawawajui Mawaziri wao, hawawajui Makatibu Wakuu wao na hawawajui Watendaji Wakuu wa Wizara, wanamjua Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.

Kwa mfano yule Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Moshi, yeye ni Mtaalam wa ardhi, hajui mambo ya kilimo, hajui mambo ya maji. Lakini yeye ndiye anaye waajiri watu hao, na unaambiwa kwamba eti yule ndiyo mwisho na ndiyo anaye waajiri. Taarifa tunazo zitoa hapa ambazo zinatakiwa ziwafikie wale *Extension Officers,* wa mifugo na wa maji hazifiki. Kwa sababu zitaenda kwa Mkurugenzi ambaye hana hata *interest* na maji au kilimo, labda anajua mambo ya ardhi peke yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba hilo liangaliwe upya kwa nguvu zote. Kweli ni katika utawala bora kuwa na Serikali za Mitaa, na kwamba watu wahudumiwe pale pale walipo. Lakini hapa tulipo tunaiambia Wizara, namna ya utekelezaji kule chini, jinsi kulivyo na tatizo.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kusema hapa na leo nalisema tena hapa, kwa sababu ni hotuba ya Waziri Mkuu ambaye ameitoa kwa kipindi cha miaka 10, liangaliwe na Serikali hii ilione, hatuta kwenda. Mambo mazuri ambayo tumefanya ya kiserikali hapa tulishirikiana tukayafanya tusisema ni CCM peke yao, tumeshirikiana na sisi wapinzani tukayafanya. Ni mazuri yanatikwa sasa yaonekane mpaka kule chini, lakini

kama tunamweka mtu hapa katikati ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, ambaye kama nilivyosema hana *interest* na vitu vingine, ni lazima kuwepo na *regulatory body*, kama mnataka hivyo kuwe na kitu ambacho kina *link* kutoka Wizarani kwenda kwa yule mfanyakazi wa chini. Kule watu wengine wanafanya kazi za ajabu ajabu tu, una wapa labda hata mapiki piki lakini utakuta wameshinda kwenye vilabu vya pombe, kwa sababu saa nyingine hawana *directive* yoyote iliyowafikia kutoka Serikali Kuu, na saa nyingine Serikali Kuu ikipeleka *directive* inakaa mwezi mmoja ndiyo anaipata, wakati imekwisha *expire.* Naomba Serikali iliangalie hilo jambo kwamba ni jambo ambalo si zuri sana.

Mheshimiwa Spika, niseme kuhusu mambo ya kahawa, nasema hili kwa sababu gani? Kuna pesa za *STABEX* zilikuja hapa, pesa zile zilikuja hapa toka mwaka 2002, eti ni zakuboresha kahawa, *fine* tukashukuru *EU* imetoa pesa bilioni 42. Kila leo hapa tunamuuliza Waziri maswali, vipi zile pesa, oh zimekwenda hivi, zitatengeneza *feeder roads. Feeder road*s za kwenye kahawa. Tukapata habari kuwa hizi pesa sasa zitatengeneza *regional roads*, na juzi hapa Mheshimiwa Waziri alitujibu, kwamba kule Karatu hawa ku-*qualify* kwenye *regional roads.* Sasa hizo kahawa zinakaa kwenye *regional roads?* Hizo ambazo zinahitajiwa kuboreshwa zinakaa kwenye *regional roads*? Kwa sababu kuna vitu vingine, Waheshimiwa wangu Mawaziri ambao tupo hapa leo ambapo sijui kama tutakutana mwaka kesho, lakini nafikiri kazi nilizofanya Moshi Vijijini, wananchi wangu watanichagua tu. (*Makofi/ Kicheko*)

Kweli hizo barabara kuu za *regional* ndiyo zinaboresha kahawa kule kijijini? *Is it true?* Nilitaka hayo Mawaziri tuliowachagua ambao ni wafanyakazi wazuri tu, myahoji hayo sio wa kina Ngawaiya tu, sio mtu aje hapa, kwa sababu ni mzungu katoa pesa aseme za kuboresha kahawa, tunaenda kuwaambia wanachi kule hizi hela ni za kuboresha kahawa.

Lakini nimeenda mpaka kwenye *internet*, ni kakuta kweli zimeandikwa ni za *regional roads,* wale wazungu wamesema zitengeneze barabara na zingine ziwekwe benki. Wametoa bilioni 10 kule Lyamungo wanasema wekeni kama *sinking fund* wekeni huko benki zizae mtakula ile faida tu. Kama wanatoa hela kwa moyo mmoja watoe! kama wanasema ni za kuboresha kahawa ziboreshe kahawa, kama wanasema ni za kutengeneza barabara zitengeneze barabara. Barabara na kahawa ni vitu viwili tofauti nani asiyejua, hivi kahawa ni barabara, angalau basi wangesema zile *feeder roads* zitengenezwe tungeelewa.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo naendelea kushukuru, kuna barabara ya lami ambayo iko Kibosho na Waziri amekwisha nipa barua ya kutengeneza Km. 7. Naomba basi mara ya mwisho alisema ni hela zinatafutwa, kwa sababu tuna hiyo barua basi Waziri Mkuu nimkumbushe kwamba katika utafutaji wa hizo pesa za Serikali basi na hiyo barabara ikumbukwe kwani barua walishanipa kwamba hiyo barabara itatengenezwa *Km 7* nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ambayo nimeyajenga katika Jimbo langu ndiyo yanayofanya watu kuja kwa wingi kutaka kugombea huko. Lakini kitu kimoja ninachosema katika utawala bora, na naomba hicho tukiangalie kwa makini ni kuhusu kofia mbili za Rais Serikalini. Mwaka uliopita viongozi wakuu wa Serikali walichangisha

milioni 100 kwamba Jimbo langu wanalitaka. Mwaka huu tumesoma hata sisi wenyewe kwenye magazeti, zimechangishwa milioni 160. Wananchi wakala zile milioni 100 wakasema sisi tunampenda Ngawaiya wetu, aende akatutetee kule sisi wanyonge.

Sasa na hizo milioni 160 naomba wale wananchi wazile na Ngawaiya wao wamlete huku Bungeni awatetee kama anavyowatetea, na kwa ushirikiano wa mimi na Serikali nina amini tu kwamba, mtu anayechaguliwa kule ni mimi. Kwa hiyo, tunaangalia ni nani anayetetea zaidi sio suala la chama zaidi. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, mwisho nataka nimalizie kwa kusema kwamba namshukuru Mheshimiwa Mungai, nilikuja na jani linaloitwa isale hapa, ni la Kichaga kwa ajili ya maombi maalum kuhusu shule ya Meli Sekondari. Kwamba jana kulikuwa na sherehe ya ufunguzi wa hiyo shule na wamenituma kwamba nije nimshukuru Waziri hapa. Madiwani wamenipigia simu wamesema niishukuru sana Serikali kwamaba ile shule sasa imeanza na kwamba kweli, kumbe Serikali ikiombwa kitu inasikia. Namshukuru sana Mheshimiwa Mungai kwa niaba ya wananchi wa wa Moshi Vijijini, baada ya kumwomba kwa kutumia jani la *isale* la Kichaga.

Mheshimiwa Spika, basi nikushukuru tena wewe, nishukuru na Serikali hii, kwa kazi tuliyofanya pamoja na tutaendelea kuwa pamoja tusiwekeane sasa vikwazo ili Ngawaiya arudi tena mwaka 2006 hapa, ahsante sana (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dr. Luoga na Mheshimiwa Bwana jiandae. Ngoja kidogo Waheshimiwa wane watakotufikisha saa sita, ni Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Danhi Makanga na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba nzuri zilizoko mbele yetu. Kwanza kabla sijaingia huko, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Mbinga Magharibi, natoa rambirambi nyingi kwa kifo cha Mheshimiwa Abu Kiwanga Mbunge wa Jimbo la Kilombero, naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, na mimi naungana na wenzangu Wabunge walionitangulia, kutoa pongezi nyingi sana, kwa wagombea wote wa nafasi za kitaifa, nikianzia na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuteuliwa ili waweze kugombea nafasi za Urais na kuchukua jukumu la kuongoza nchi hii kwa miaka mitano ijayo. Nawaombea Mwenyezi Mungu awape afya njema na baraka nyingi ili nia yetu hiyo iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, tumepata hotuba tatu sasa, ni hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, hotuba ya Waziri wa Fedha na jana tumepata hotuba ya kiongozi wetu wa Serikali hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hotuba zote ni hotuba zimechambua utekerezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kipindi cha miaka 10. Hotuba zote zimechambua kinaga ubaga, jinsi uchumi wetu ulivyokuwa, jinsi mapato ya Serikali yalivyoongezeka, jinsi mwenendo wa upunguzaji wa mfumuko wa bei

na mambo hayo yote yamedhihirisha wazi kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelezeka. (*Makofi*)

Mimi kwa niaba ya wananchi wa Mbinga Magharibi, itakuwa ni ajabu nisipounga mkono hotuba hizi zote. Ni hotuba zinazoelezea mafanikio na mafanikio makubwa yameonekana, uchumi umekuwa, mapato ya Serikali yamekuwa, sasa zaidi ya hapo tupate nini. Kwa niaba ya wananchi wangu naunga mkono hotubi hizi zote. Mimi nina mambo machache ya kuchangia, kwa sababu utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni Mambo yote katika nchi hii na mambo hayo yote yametekelezeka, lakini nina mambo kidogo ya kuweza kuyaelezea

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Mbinga tuna tatizo la mpaka wa Ziwa Nyasa na mpaka huu unatuathiri sana. Mipango mingi ya maendeleo inayaotakiwa ifanyike katika maeneo hayo, kwa mfano uboreshaji wa mazingira ya mabonde ya Maziwa, Ziwa Nyasa halimo.

Mabonde ya Ziwa Victoria, mabonde ya Ziwa Tanganyika yanaboreshwa, mazingira yake yanaboreshwa, lakini upande wa mabonde ya Ziwa Nyasa, mabonde hayo hayaboreshwi kutokana na matatizo ya mpaka kati ya nchi yetu na Malawi na hilo linaoneka wazi wazi hata mipango ya Serikali ya kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo, Serikali haielekezi nguvu zake sehemu hizo na tatizo kubwa ni mpaka. Ningeiomba Serikali ilifanyie kazi suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili ni suala muhimu, ni suala linarudisha maendeleo ya watu, tukililea tatizo hili bila kulifanyia kazi, miaka inapita na hii ni raslimali moja wapo ya wananchi itakuwa ni jambo ambalo sio jema. Hotuba zote zimejikita jinsi ya kuinua uchumi na kuondokana na umaskini na hasa umaskini uliokithiri.

Ni kweli umaskini upo sehemu zote, umaskini upo mijini na upo vijijini. Lakini umaskini uliokithiri hasa uko vijijini, ndiyo kwa maana unawaona vijana wengi wanakimbia maisha magumu ya vijijini, wanakimbia shuruba za vijijini, wanakimbilia mijini na tatizo kubwa hawawezi kujiajiri katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo kazi yake ni ngumu sana, mwananchi anatumia muda mwingi, anatumia nguvu nyingi, sehemu anayolima ni kidogo, anacho kipata kidogo chenye thamani ya chini, kwa hiyo hakikidhi kuinua maisha yake, ndiyo kwa maana vijana wengi wanakimbilia mijini.

Sasa mpango wa MKUKUTA, mpango wa kuboresha uchumi na kupunguza umaskini ningeishauri Serikali, ielekeze nguvu nyingi za ziada vijijini. Huko ndiko kuliko kita umaskini. (*Makofi*).

Barabara sehemu nyingi hazipitiki, maji hayapatikani, tulipitisha Sheria ya umeme vijijini, mpaka sasa hivi katika Bajeti hii hatuoni, wala hukuna mahala inayoelezea jinsi gani Sheria hii itakavyo tekelezeka. Kwa hivyo ni vema hatua ya kwanza, *program* hii ya kuboresha uchumi na kupunguza umaskini, ni lazima mikakati maalum na uwezo maalum uelekezwe na utolewe vijijini ili kuinua maisha ya watu.

Kilimo ndiyo sehemu pekee wanayotakiwa vijana wabaki kule na wajiajiri katika kilimo, wao wanakimbilia mjini kuuza soksi moja kwa siku. Sio kama hawataki kujiajiri, tatizo kubwa kazi ya kilimo ni ngumu, Serikali iboreshe sekta ya kilimo na sekta ya umwagiliaji maji, Serikali iboreshe barabara vijijini ili wanachi waweze kuitumia waweze kusafirisha bidhaa wanazozalisha, waweze kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana mpango wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini kwa asilimia 50 ya Bajeti iliyotengwa ielekezwe vijijini, ndiko hasa watu wanapata shida na umaskini.

Kuna mipango mizuri Serikali imefanya, kwa mafano wa kugharamia usafirishaji wa pembejeo. Mwaka jana 2004 Serikali iliweka bilioni 2 na mwaka huu imetenga bilioni 7.4. Lakini fedha hizo hazimsaidii sana mkulima wa kijijini Mbolea anayopata mkulima toka makao makuu ya Mkoa, anapata mbolea kwa bei ya juu sana.

Ni vyema utaratibu uwekwe, ili mbolea hiyo isafirishwe hadi Wilayani walau kwa kuanzia, badala ya kusafirisha hadi Mkoani. Lakini ukiendelea kusafirisha pembejeo hadi makao makuu ya Mkoa, mkulima ataendelea kupata shida kuipata hiyo mbolea.

Mheshimiwa Spika, jingine, ni juu ya Bajeti ilivyotenga ule mfuko wa pamoja, tunashukuru wamepunguza hisa kwa asilimia 30. Lakini kutokana na hali ngumu ya mwananchi kijijini. Mimi naishauri Serikali hisa zote zitakozouzwa kwa mwananchi kijijini ingefaa serikali igharamie nusu na mkulima alipe nusu.

Hali maisha ya mtu wa kijijini ni duni sana hatakuwa na uwezo wa kulipa shilingi 70 kwa hisa. Kama lengo tunataka hisa hizo zimilikiwe na wananchi wa chini ili ziwasaidie kuinua maisha yao, ni vema hisa hizo zikauzwa shilingi 50 kwa wanachi wote wale wa chini wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbinga ni Wilaya iko pembezoni, kama Wilaya ya Nkasi na Tunduru. Mara zote miradi inayoanzishwa na Serikali inakuwa kwenye *pilot project.* Wilaya hizo zote za pembezoni hazipati fulsa na mara zote miradi hiyo ikianza, ikimalizika kwenye *pilot project* haiendelei. Sasa naishauri Serikali huu mradi wa *TASAF* awamu ya pili ianzie Wilaya za pembezoni ikiwemo Mbinga mojawapo. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika inakuwa sio vyema mara zote mnaanzia, Wilaya zilizokaribu na makao makuu ya Mkoa, mnafanya *pilot projects* na inakwisha na baada ya hapo miradi hiyo haindelei.

Kwa hivyo mtakapoanza Wilaya zile za kwanza kabisa katika mradi huu wa *TASAF* ni vema Wilaya ya Mbinga nayo ikaingia na vile vile kwa upande wa umeme, hadi leo hii Mbinga haina umeme, mji wa Mbinga hauna umeme. Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika Mbinga na Wananchi wote walimwelezea kwa vitendo. Waliwasha vibatari kumwonyesha kwamba tumechoka na hali ya kutumia vibatari na hari ya moshi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba sana, Serikali itekeleze mradi wa kupeleka umeme Mbinga na huu mradi wa *Rural Electrification* ni vema Serikali ikaanzia vile vile Mbinga. Kwa sababu Wilaya haina umeme, vijiji havina umeme. Sasa katika hali hiyo tutaendelea vipi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hii hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Naomba niungane na wenzangu waliokwisha tangulia kutoa mkono wa pole kwa wananchi wa Wilaya ya Kilombero kufuatia msiba mkubwa walioupata wa kufiwa na Mbunge wao Marehemu Abu Kiwanga. Naomba Mwnyezi Mungu apumzishe roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitumie nafasi hii kutoa shukrani za dhati kabisa na pongezi nyingi mno kwa Mgombea wetu wa Urais ambaye tumemteua hivi karibuni, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Alipata kura nyingi, kura za heshima na kura za kishindo.

Ninapenda kuthibitisha na kuwathibitishia Watanzania wenzangu kwamba, ushindi wa Ndugu Kikwete ni dhahiri kwamba kwa kweli kijana huyu anakubalika na wengi na kwamba atapata ushindi ambao hatujawahi kutokea katika historia ya Tanzania. Hivyo, nimpongeze pia Mgombea wetu Mwenza Makamu wetu wa Rais Dr.Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa ushindi walioupata na pia wote kwa pamoja tunapenda kuwathibitishia kwamba tutajipanga inavyotakikana ili kuhakikisha kwamba wanashinda ushindi wa kishindo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nikushukuru na wewe Spika wetu kwa kipindi cha miaka 10. Umetuongoza vyema katika Bunge hili la Mfumo wa Vyama Vingi. Umekuwa ni mfano wa kuigwa ukilinganisha na Maspika wenzio wa nchi mbali mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukishuhudia kupitia Vyombo vyetu vya Habari tukiona ngumi zinaanguka kwenye jengo la heshima kama hili la Bunge. Unakuta watu wanapigana na nini…lakini katika kipindi chako hatukushuhudia vitu hivyo. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Tunapenda kukuthibitishia kwamba utuombee na sisi ili tutakaporudi tukuchague tena uendelee kutuongoza.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia niwapongeze Wabunge wenzangu wote kwa kazi zao nzuri walizozifanya kwa kipindi chote. Tunakwenda kwenye uchaguzi, lakini nikiwaangalia Wabunge hawa simwoni Mbunge hata mmoja ambaye anaonyesha dalili za kushindwa kwenye Jimbo lake la uchaguzi. Kwa hiyo Ninapenda niwatakie wote heri na baraka tele za Mwenyezi Mungu ili aweze kutusimamia na tuweze kurudi salama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri Mkuu ni nzuri sana. Ametoa Taarifa na kazi ambazo amezifanya kwa kipindi cha miaka 10. Wote tumeipitia kipengele hadi kipengele na tumeridhika nayo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda niseme kwamba kwa kweli mimi binafsi ninaiunga mkono hoja mia kwa mia.

Niwashukuru sana pia wasaidizi, Mawaziri wote walioko katika Ofisi yake, wanaomsaidia Waziri Mkuu. Nimshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Mama Rose Lugembe na wataalam wote waliosaidia kwa namna moja ama nyingine katika maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, sasa ninaomba nielekeze mchango wangu moja kwa moja kwenye hotuba hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kabla sijafanya hivyo, ninapenda nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Chanji, Sumbawanga, mimi ni Mlezi wa ile shule.

Shule hii imekuwa na maendeleo mazuri sana ukilinganisha na shule zingine. Walimu wake wamekuwa wakijitahidi, maana sisi wazazi tunachokitaka ni kuangalia ni wanafunzi wangapi wamefaulu kwenda Sekondari. Tumekuwa tukishuhudia kwenye Vyombo Vya Habari tunakuta wanafika mahali wazazi wanalalamika kwamba inakuwaje shule yetu hii hakuna mtoto hata mmoja anayefaulu kwenda Sekondari. Kuna matatizo gani? Ni matatizo ya Walimu au ni matatizo ya watoto wetu?

Lakini ninafuraha leo hii mimi kama Mlezi wa ile Shule kutamka kwamba; kwa kweli ile shule yangu ambayo mimi ninailea kama Mlezi, imefanya kazi nzuri sana na ni mfano wa kuigwa.

| **Mwaka** | **Waliofanya Mtihani** | **Waliofaulu Kwenda Sekondari** |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 2002 | 90 | 78 |
| 2003 | 107 | 83 |
| 2004 | 72 | 72 |

Kwa hiyo kwa kweli kitendo hiki kinastahili pongezi sana na mimi kama Mlezi wao kwa kweli ni kitendo cha heshima, najivuna na nawatakia heri na nawapongeza Walimu na Wanafunzi wote wa Shule hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, ninaelekeza mchango wangu kwenye hoja.

Mheshimiwa Spika, Wilaya nyingi za Mkoa wa Rukwa pamoja na Wilaya zote kwa ujumla, tumepeleka mapendekezo yetu ya kuomba kuongezwa Kata. Tuna Kata Kubwa na tuna Kata nyingi ambazo ni kubwa na zingine zinashinda hata Wilaya.

Unakuta Kata moja ina watu mpaka 20,000. Sasa hii unakuta inaleta tatizo kubwa sana la usimamiaji wa shughuli za Utawala Bora na uhimizaji wa shughuli za maendeleo.

Tumepeleka maombi ya kuomba kuongezwa Kata, si Mkoa wa Rukwa peke yake, nina amini kabisa hata Wabunge wenzangu hapa nao wamepeleka maombi hayo lakini mpaka sasa hatujapata jibu lolote. Ninaomba safari hii Serikali itoe Tamko, ni lini itatoa Tamko la Kuongezwa Kata? Tunasubiri tupate hilo Tamko kabla hatujaondoka hapa Bungeni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapokuwa anazungumzia hili, ninaomba atueleze, tunapenda kupata Tamko la Serikali. Maana maombi ya kugawanywa Kata yalishaletwa muda mrefu. Hivi inachukua miaka mingapi kufanya maamuzi kuhusiana na suala hili?

Mheshimiwa Spika, tunaomba hili basi tuweze kupatiwa majibu yake. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la Makatibu Tarafa. Wote tunaelewa kazi nzuri na kubwa wanazozifanya Makatibu Tarafa katika maeneo yetu na kote nchini. Wanasimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao na Utawala Bora na masuala mbali mbali ya Ulinzi na Usalama katika maeneo yao.

Tunaelewa kabisa kwamba kuna baadhi ya Tarafa zingine ni kubwa kushinda hata Wilaya, lakini Makatibu hawa wamekuwa wakifanya kazi yao vizuri sana, lakini tatizo linalojitokeza kwa upande wa hawa Makatibu Tarafa, tunashukuru Serikali ilishatoa nyenzo za kufanyia kazi, Pikipiki. Napenda niipongeze sana Serikali kwa hilo. Makatibu Tarafa wote chini wameishapata Pikipiki, lakini linajitokeza tatizo la mafuta. Mafuta ni tatizo ambalo linajitokeza kwa Makatibu Tarafa hawa. Sasa katika hili mimi nilikuwa

napenda nipendekeze kwamba ninashauri kwamba Serikali ione umuhimu wa kuliangalia hili upya ili ikiwezekana waongezewe kiasi fulani cha fedha kwa ajili tu ya mafuta ambayo yatasaidia katika ufuatiliaji wa masuala mbali mbali ya maendeleo katika maeneo yao.

Katika hili, ninapenda nipendekeze, badala ya fedha zile kupitia Wilayani ambako ninajua kuna urasimu mwingi na mkubwa na kuna uwezekano mkubwa pia wakajikuta hiyo fedha imekwenda kufanya kazi nyingine zaidi ya ile iliyokusudiwa. Katika hili napenda nishauri, ni kwamba ni vyema basi Serikali ikaangalia, ikiwezekana basi hizi fedha ambazo zinaelekezwa kwa ajili ya kuwasaidia Makatibu Tarafa mafuta, basi ziingizwe moja kwa moja kwenye mishahara yao. Kwa kufanya hivi nadhani kwamba tutakuwa tumesaidia vizuri katika usimamiaji katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la Wakuu wa Wilaya. Tunaelewa kabisa kuwa kuna Wilaya ambazo ni kubwa kushinda Wilaya zingine. Kwa mfano Wilaya ya Mpanda, Wilaya ile ni kubwa kushinda Mkoa wa Kilimanjaro na Tanga kwa pamoja. Kazi ya usimamiaji na uhimizaji wa shughuli za maendeleo katika Wilaya ile ni ngumu. Sasa katika hili mimi napenda nipendekeze pia kwamba ninaomba Serikali iangalie kwa zile Wilaya ambazo ni kubwa kama hii Wilaya ya Sumbawanga, Wilaya ya Mpanda, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini, Wilaya ya Nkansi, Wilaya ya Sikonge na maeneo mengine, Serikali iwaongezee pia mafuta watendaji hawa kwenye maeneo yao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana kinachokuja kujitokeza inakuwa ni kero kwa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi, maana safari zinakuwa ni nyingi, fungu la mafuta kwa Mkuu wa Wilaya limekwisha. Analazimika kwenda kufuatilia shughuli za maendeleo kule, inabidi akampigie magoti Mkurugenzi. Sasa Tuelewe kwamba hawa ndio wawakilishi wa Rais kwenye maeneo yale, naomba hili tulitazame. Lingine, katika hotuba ya Waziri Mkuu sikuona mahali ambapo amezungumzia ni Wizara ngapi katika kipindi hiki cha mwaka fedha zitahamia Dodoma, sikuona. Ila ninachojua tu ni kwamba kuna kazi kubwa inayoendelea kwa *speed* kubwa ya ujenzi wa nyumba za Mawaziri na Manaibu Waziri Dar es salaam. Sasa suala la kuhamia Dodoma tunasemaje? Ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze, ni Wizara ngapi zinahamia Dodoma mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, lingine, ni nyumba za Temeke *quarters*, zile nyumba zilishatelekezwa. Najua zinasimamiwa na Manispaa ya Temeke. Zile nyuma hazipigwi rangi, zile nyumba hazifanyiwi matengenezo yoyote, barabara sasa hivi kwenye zile nyumba hakuna, mapaa yanaangukia watu hovyo. Sasa, Serikali inatamka nini? Kwa nini nyumba zile wasiuziwe wananchi wanaokaa kwenye zile nyumba? Watu wako kwenye zile nyumba tangu mwaka 1961 mpaka leo hii, kwa nini Serikali isitamke kuziuza zile nyumba kuwauzia wale wananchi wanaokaa kwenye zile nyumba ili hiyo fedha itakayopatikana Serikali ikatumia kujenga nyumba zingine kwenye maeneo mengine, kuliko nyumba zimekuwa ni magofu, hakuna barabara ni vichaka vya majambazi, hakuna taa, zimeachwa kama zilivyo. Ninaomba nipate majibu ya Serikali kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, lingine, ni suala la Wastaafu waliolipwa kwa mkupuo. Kule Sumbawanga, wale Wastaafu kabla sijaja hapa wamenifuata. Wanaambiwa kwamba wale Wastaafu wanaoshughulikiwa sasa hivi ni wale waliostaafu kuanzia mwaka 1994 kurudi nyuma. Wao wanaambiwa wasubiri. Sasa maelekezo yale mbona yanapingana na yale tuliyoelezwa hapa Bungeni. Sasa wale Wastaafu wanatufuata wanaomba tuwasaidie.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimwa Waziri Mkuu atusaidie katika hili utekelezaji wake uko vipi, na watoe Tamko kuhusiana na wale Wastaafu walioko kule Sumbawanga, ni lini masuala yao yataanza kushughulikiwa? Kuliko wanakwenda wanapandisha ngazi wanarudishwa, wanaambiwa kwamba wale ambao wanaanza kushughulikiwa malipo yao ni waliostaafu kuanzia 1994 kurudi nyuma. Sasa hawa waliostaafu mwaka 1995 kurudi mbele wanafanywaje.

Mheshimiwa Spika, ninaomba hili Waziri Mkuu atueleze maana ni kero kwa wale Wazee kule. Wanahitaji kupata ufafanuzi wa kitu hiki.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo nilikuwa nimepanga kuyazungumza leo. Kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii na mimi kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijaendelea, natoa pole mbili. Pole ya kwanza kwa Mheshimiwa Abu Kiwanga Mbunge wa Kilombero na pole ya pili najipa mimi mwenyewe kwa sababu hata Jimbo la uchaguzi sasa sina. Kwa hivyo watu wanaposema kuwa wanaomba dua turudi sote, najua sisi wawili tumeisha toka. Mwenzangu simtaji jina. Kwa sababu Majimbo yamechanganywa kwa hivyo huna budi lazima mmoja atoke tu, hapo lazima nitoe pole. Kwa hivyo wale walioomba dua ya kuomba turudi sote, kwangu mie kama imegonga mwamba, hiyo haifiki.

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kupongeza sana wagombea wetu wa Chama Cha Mapinduzi waliopitishwa na Chama ili kugomea nafasi za Urais wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mgombea Mwenza wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea mbele naunga mkono hoja mapema hii ili nisije kusahau.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Waziri Mkuu kwa Hotuba yake ambayo imelenga muda wa mika 10 ya kipindi chake cha uongozi wa ndani ya Bunge hili. Vile vile nawapongeza Mawaziri wote na watendaji wa Wizara ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo nataka kulizungumzia asubuhi hii ni suala la Elimu ya Juu. Elimu ya Juu Tanzania ni Elimu ya Muungano, ni sekta ya Muungano. Lakini tatizo kubwa ambalo linajitokeza, ni kuwa tuna nchi mbili, lakini muhtasari unaotumika katika shule za msingi ni tofauti Zanzibar na Tanzania Bara. Lakini ufikapo juu tunachanganya tunakuwa ni kitu kimoja. Kwa hiyo maandalizi ya shule za msingi

yanakuwa ni tofauti baina ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara. Kwa maana hii sijui tunawaandaje watu wetu ili kuwaandaa na ajira au Soko la ajira la Afrika Mashariki wakati Mitaala yao inatofautiana baina ya nchi moja na nchi nyingine. Na wakati huo huo utaona kuwa Mitaala ya Sekondari inaanzia *Form One* ambao kimsingi kila mmoja katoka na msingi wake chini na kufikia juu ndiyo wanakutana na mtihani wa Elimu ya Juu wanafanya pamoja.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kuwa ipo haja nchi mbili hizi tuangalie Mitaala ya *Primary* nayo iunganishwe kama ilivyounganishwa ya *Secondary.*

Suala zima ambalo hivi sasa linatukabili Zanzibar, utaona ufanisi wa maendeleop ya Elimu kwa kweli ni mdogo. Ukiangalia watoto ambao wanafanya mtihani na ambao wanapasi katika shule zetu ni kidogo sana kulinganisha na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, naomba tulizingatie katika nchi zetu hizi au katika suala zima la Muungano, kama tunaunganisha basi tuunganishe sote katika shule za *Primary* na *Secondary,* mitaala iwe aina moja.

Hivi sasa, ukweli *World Bank* imetoa msaada wa Dola 10,000,000 kwa Zanzibar kwa ajili ya Elimu ya *Secondary* na Bara wamepewa Dola 150 kwa ajili ya elimu ya Sekondari. Maandalizi haya tayari ambayo yalikuwepo, lakini ni yale ambayo ninayasema. Kule tuna mfumo wetu wa Elimu na huku mfumo wetu wa Elimu.

Zanzibar hivi sasa wameishapisha sera, Elimu ya lazima ni mpaka *Form Four* lakini bado Tanzania Bara Elimu ya lazima mpaka Darasa la Saba. Sasa, tofauti zipo, wakati ambapo tunaingia katika soko moja lakini tofauti ya Miundo inakuwa ni hiyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninataka kulizungumzia kuhusu Mitaala na Michepuo. Ni suala ambalo hivi sasa ni gumzo au ni mazungumzo ambayo yanzungumzwa katika Taasisi nyingi nchini. Lakini ukiangalia mchepuo ni Wabunge tu wenyewe kuwa tunasahau tunakotoa na tunaelekea kule ambako tunakotaka sisi wenyewe. Ukiangalia mchepuo, sera ipo ambayo imepitishwa na Bunge ya kufuta kitu kile, lakini bado Wabunge wanalalamikia kuwa mchepuo kuwa ni kitu ambacho kinaweza kikasaidia. Lakini ni Bunge hili hili 1995, na Wabunge hawa hawa wengine wamo wamepitisha sera hiyo lakini ni wazito wa kufahamu.

Mheshimiwa Spika, naomba tufanyiwe semina tena, tuelimishwe juu ya nini mchepuo ulivyofutwa na athari zake na faida zake. Lakini hiyo ipo na kama watu wanataka kufanya *reference* waangalie *Hansard* za 1995, zipo na Wabunge wengine yamo majina yao wamechangia na wakasema kuwa wanaunga mkono hoja. Lakini leo, utekelezaji wa suala lile unapoanza basi wanakuwa wagumu wa kuunga mkono na kushawishi watu kuwa michepuo imefutwa ambayo inaweza ikaleta athari ndani yake.

Kuhusu mitaala, vile vile tulipiga kelele sana chini kuwa masomo mengi. Wanafunzi wanasababishwa kubeba mzigo mkubwa, yaani ilipochanganywa tunaona

kama ni kitu cha ajabu hivi sasa tunaanza kupiga kelele kuwa mitaala sijui unachanganya somo hili na somo lile.

Kuhusu mitaala, lakini suala hili kwa kweli wananchi na wataalam wengine wamelipigia kelele sana kuwa mzigo wa wanafunzi kwa shule zetu, ni mkubwa isipokuwa ni kuhakikisha kuwa tunapunguza masomo, tunaweka yale ya lazima ambayo yanaweza yakasogeza kwa hatima yake ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia kuhusu fedha za MMES ambazo zimetolewa kuanzia Januari mwaka huu. Lakini tatizo kubwa ambalo fedha hizo zinapitia kwenye Hazina ndogo za Mikoa, imekuwa ni kikwazo na tatizo kuwafikia walengwa.

Hivi ambavyo nazungumza humu Bungeni mpaka leo baadhi ya shule hawajapata fedha hizi kwa sababu ya urasimu, sababu ya masharti mazito na sababu nyingine ambazo ukiona ndani yake utaona kama imo utoe chochote na fedha zile ndipo upate.

Kwa hiyo, ipo haja kuangaliwa upya suala la fedha za MMES zinapoingia katika Hazina ndogo, zinawafikia vipi walengwa ambao wamekusudiwa. *(Makofi)*

Tayari shule nyingine imeisha idhinishiwa fedha, lakini wanashindwa kuzitoa kwa jinsi ya utaratibu na urasimu uliopo wa kuzipata fedha kama hizi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia kuhusu Wizara ya Elimu na Utamaduni. Kwa kweli ukiangalia sana Wizara ya Elimu na Utamaduni, imejikita sana kwenye Elimu ukilinganisha na Utamaduni. Inashughulikia sana Elimu ukilinganisha na Utamaduni. Ipo haja kama uwezekano upo, Wizara hizi kutengwa kuwa ni kitu tofauti baina ya Wizara ya Elimu na Uatamaduni. Ukiangalia mambo mengi ya Utamaduni nchini Tanzania yamekufa kabisa hayashughulikiwi.

Hivi sasa kitu ambacho ni cha msingi, matamasha ya Sanaa za Utamaduni wa Kitanzania sifikirii kama yanafanyika. Lakini utashangaa kumtafuta *Miss Tanzania,* hivi sasa wananzia kwenye vitongoji, *Miss Tanzania* wanaanzia kwenye vitongoji. Lakini usanii au zile shughuli za Utamaduni wa Mtazania, kwa kweli hivi sasa katika Vijiji au katika Miji haishughulikiwi kabisa, umekufa.

Kwa hiyo, ipo haja kuwa lazima Utamaduni wetu tuurudishe kule ambako tunakotoka. Kama upo uwezekano kama nilivyoshauri kuwa Wizara hizi mbili zitengwe baina ya Wizara ya Elimu na Wizara ya Utamaduni kama ivyowahi kuwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, mara nyingi sana hata mwaka jana 2004 niliwahi kulizungumzia ni kuhusu Lugha yetu ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ni Lugha ambayo hivi sasa inapanua mipaka yake na inaenea kwa kasi kubwa sana katika Bara la Afrika na nje ya Bara letu.

Lakini ukiangalia hapa nchini hakuna mkakati wowote au hakuna programu zozote ambazo zimewekwa za kuhakikisha kuwa hii Lugha inaweza ikakua na kuimarishwa. Kwa mfano, ukiangalia sera ya Lugha ya Kiswali nchini Tanzania haipo. Sana sana utakuta imebandikizwa tu katika sera nyingine. Kwa hiyo, ipo haja ya kuwa lazima tuwe na sera ya matumizi mazuri ya Lugha ya Kiswahili. Lakini wakati huo huo ukiangalia katika Katiba yetu haisemi kuwa Lugha yetu hasa ni Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba alipokuwa anajibu maswali ya Wabunge kipindi kilichopita kuhusu marekebisho ya Katiba, alizungumzia hivi kuwa unafanywa utafiti kuhakikisha kuwa Lugha ya Kiswahili ipo haja ya kuingizwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Hili kwa kweli ni suala zuri ambalo linaweza likasaidia huko tuendako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu malalamiko ya Walimu yaliyowekwa na Chama cha Walimu. Suala zima ambalo kwa kweli hivi sasa Elimu ya Msingi (MMEM) imeandaa mazingira mazuri, maendeleo yake kwa kweli kwa baadhi ya sehemu ni mazuri, lakini tatizo lipo kwa Walimu wapya ambao kwa kweli hawajawekwa katika mazingira mazuri ambayo yanaweza yakasaidia.

Kwanza, tatizo kubwa ambalo linawakabili Walimu hao ni ucheleweshwaji wa posho na mishahara. Hili ni tatizo ambalo kwa kweli linapigiwa kelele sana na wahusika na ipo haja Serikali ione kuwa hata kama linafanyika, lakini ni kwa kasi ndogo sana. Juzi tu nilipata malalamiko kuwa Walimu wanadai kuwa wanaopata mishahara na posho ni Walimu wanaoishi karibu na Miji hususan Dar es Salaam. Kwa hiyo, tuliondoe tatizo ili kuhakikisha kuwa mishahara inafika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu lingine ni kwamba, malimbikizo ya mishahara yanakuwa hayalipwi kwa wakati au hawalipwi kabisa. Halafu wakati huo huo mapunjo ya mishahara, *arreas* zao hawalipwi. Vile vile, uhamisho wa kiholela, yaani Afisa akimchukia tu Mwalimu kwa haja yake tu, anaweza akatoa uhamisho wa kiholela. Kwa hiyo, ipo haja suala hili lihakikishwe kuwa linaangaliwa ipasavyo, wahakikishe kuwa Walimu wetu wanafanya kazi katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni uhakiki uliofanywa katika madai ya Walimu wa Sekondari na *Primary.* Mpaka kufikia mwaka jana 2004 Tume ya Mheshimiwa Kwaangw' inasema hivi: "Walimu wa Shule ya Msingi ambao wanadai madai yao hayapungui bilioni 13 na kitu hivi, Walimu wa Sekondari bilioni nne na kitu". Madai hayo yamegawiwa katika vifungu vifuatavyo:-

Napenda kunukuu kama ifuatavyo:- "Madai hayo, aina ya wadai, kiasi cha madai na asilimia zake, uhamisho, wanadai Shilingi bilioni nane na kitu, yaani sawa sawa na asilimia 70; masomo yaani mafunzo ni Sh.798,000,000/= ni asilimia saba; safari za kikazi wanadai Sh.90,000,000/= ni sawa sawa na asilimia moja na mambo mengine yanaendelea

kama vile likizo, matibabu, posho za ajira, posho za chakula, madeni ya waliofariki na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni matatizo ya utekelezaji kwa Walimu wa Shule ya Msingi (MMEM). Leo tu asubuhi tulivyosikia taarifa ya Redioni inasema kuwa, Sengerema kuna madai ambayo ule mfumo wa elimu ya MMES, yaani watu wamevuruga pesa nyingi kweli! Sh. 42,000,000/= hazijulikani wapi zilipo na Diwani anashawishi watu wasiweze kujitolea mpaka wahakikishe kuwa madai haya yanajulikana nani ambaye amehusika. Ni kitu ambacho kwa kweli kinatisha na kushangaza kuwa Serikali ipo, Halmashauri zetu zipo, lakini usimamizi wa fedha za MMEM bado ni mbovu. Kwa hiyo, ipo haja tunatakiwa tuhakikishe kuwa fedha ambayo inalengwa kuwafikia wananchi inatumika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni Mfuko wa Elimu ya Juu. Mfuko huu tayari kwa kweli umeshawekewa sheria na sheria hiyo tayari imeshafika kwenye *Cabinet* na kufikishwa Bungeni. Lakini ipo haja ya kuwa iharakishwe kwa sababu Bunge hili ndiyo linamalizia na Mawaziri ambao walianzisha ari hii na wao wanaondoka. Kumbukumbu zinabaki, lakini ari ni ya mtu aliyeanzisha ndiyo inaleta ufanisi zaidi.

Kwa hiyo, ipo haja Mfuko huu kuangaliwa upya na kiasi ambacho kwa kweli kimekusudiwa kuwekwa ni kiasi kile ambacho wanakusudia kukiomba kwa sababu Mfuko huu unasaidia katika kuweka misingi mazuri ya Elimu ya Juu. Lakini tokea uanzishwe mwaka 2001 mpaka kufikia leo, yaani fedha anazopata kiasilimia utakuja ulipoanza fedha waliyokadiriwa kupewa wakati ule ilikuwa ni bilioni nne.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, napenda kutoa pole kwa ndugu, jamaa pamoja na familia na wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na mpendwa wao Mbunge Abu Kiwanga. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Vile vile, napenda nikupongeze kwa namna ya pekee kabisa kwa namna ulivyoongoza Bunge letu kwa kipindi cha miaka 10. Kazi uliyoifanya ni nzito na ni nzuri na ni ya pekee. Mimi nakutakia kila la kheri, ikiwezekana katika kipindi kijacho uweze kuchaguliwa kuliongoza hili Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda niliseme ni kumpongeza kwa namna ya pekee Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa namna tulivyokaa wote, alivyotuongoza na alivyotuelekeza. Hakika alifanya kazi yake na alijitoa mhanga, naye alituamini na sisi tulimwamini, hivyo tukakaa pamoja na ndiyo maana tumefikia hapa na matokeo yanaonekana. Hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu, naweza nikamwita kwamba alikuwa ni *shock absorber* alihimili kila lililokuja, hakuweza kukata tamaa.

Kwa hiyo, nakutakia kila la kheri huko uendako lakini bado jamii inakuhitaji. Waswahili wanasema: "umuhimu wa mkia wa ng'ombe unapatikana baada ya kukatika." Kwa hiyo, bado jamii inakuhitaji. Tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu, akujalie afya njema ili uweze kuitumikia jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kuhusu siasa kwa jumla,kwamba kwa kipindi hiki tunaelekea kwenye uchaguzi na mambo yanaelekea kuwa mazito, watu wanatishia, watu wanasababisha vurugu mpaka matukio ya pale Bagamoyo yanaonesha kwamba uchaguzi ujao kama tusipokuwa waangalifu unaweza ukawa ni mgumu na wa kusababisha vurugu.

Kwa vile Vyama ambavyo vimekuwa vikisababisha vurugu tunavijua, mimi napenda niwaambie wananchi wanapaswa kuwa waangalifu navyo, wavichunguze, wafanye tafakari ya hali ya juu sana, wasije wakavipa madaraka na hivyo wakivipa madaraka matokeo ndiyo hayo ya kutiana ngeu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niseme ule msemo wangu, huwa napenda mara kwa mara kusema ule msemo wa kikwetu ambao unasema hivi: "Mtu ambaye ni mlafi unamwaangalia wakati wa kunawa. Wakati anapokuwa ananawa yeye huwa anaangalia tu chakula kile, kwa hiyo, hanawi vizuri." Kwa hiyo, hawa jamaa zetu wameshaonekana wakati wananawa,. Wakati wanatafuta madaraka wameshaonekana kwamba watakuwa walafi hawa, watasababisha vurugu, watasababisha matatizo katika nchi yetu ambayo ina hali ya utulivu, amani na mshikamano. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nawaomba wananchi huko waliko wawachunguze kwa makini namna wanavyoendelea kunawa na wawakatae kabisa kwa nguvu zao zote kwa sababu watatusababishia vurugu na matatizo ambayo yatatuvunjia amani. Kwa hiyo, naomba wananchi wawe waangalifu na hawa watu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda niliseme ni kujielekeza katika hotuba yenyewe. Hotuba ni nzuri, kwani imefanya majumuisho kwa kipindi chote cha miaka kumi. Lakini kuna mambo machache ambayo napenda kwanza niyaseme hata kabla ya kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa kwake kuwa Mgombea wa Urais pamoja na Mheshimiwa Dr. Shein kuwa Mgombea Mwenza katika Kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Wote nawapongeza, nawaombea kila la kheri ili waweze kuchaguliwa tuweze kuiendeleza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo machache ambayo nimeyaona niyaseme kwanza, ni kuhusu uwekezaji. Uwekezaji wakati ulipofika, nchi ilifungua milango, madirisha na ikiwezekana hata paa kuwakaribisha wawekezaji. Lakini matokeo ya kufungua milango, madirisha na paa wawekezaji wenye sifa na wasiokuwa na sifa wanaonekana wameshaingia kwa namna ambayo wengine wanadiriki hata kuchukua kazi zile ambazo watu wetu wanaweza wakazifanya.

Juzi nilikuwa Dar es Salaam kwenye Soko la Jumapili na Jumamosi. Kitu kilichonishangaza nilikuja kuona hata wafanyabiashara wa kutoka China na wao wanauza maua pale pale kwenye lile Soko. Halafu Waasia wengi unawakuta wako kwenye *kiosk* kazi ambazo zinaweza zikafanywa na Watanzania. *(Makofi)*

Naomba kwa namna ya pekee kabisa, Kituo cha Uwekezaji kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji, wahakikishe wanafanya utaratibu wa kuwaondoa hawa wawekezaji uchwara. Hawa ambao wanafanya kazi ambazo zinaweza zikafanywa na Watanzania waondoke na wasipewe vibali. Kwa nini tufikishane hapo?! Kazi ambazo zinaweza zikafanywa na Mtanzania, zifanywe na watu kutoka nje!! Wewe tangu lini mtu unatoka China, India, unakuja kufanya kazi ndogo ndogo za kuuza maua, kutembeza soksi, kuosha magari? Hawa watu wapo! Labda kama hamjawaona, mnajilazimisha kutokuwaona, lakini wapo. Nawaomba kabisa Kituo cha Uwekezaji Idara ya Uhamiaji, ihakikishe inafanya uchambuzi kuwaondoa hawa wawekezaji uchwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda niliseme ni kuhusu mpaka wa Bukombe pamoja na Biharamulo. Mpaka sasa hivi wale wananchi wanaokaa katika mpaka huo ambao ni wa Vijiji vitano, hawajui hata wakati wa kupiga kura waende kupigia kura katika Kata ipi, wala hawajui wako kwa kiongozi yupi. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi wale wananchi hawaeleweki wanapaswa kufanya nini. Miradi yote ya MMES, MMEM, Zahanati, vyote hivyo hawajafanyiwa hata kidogo.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili suala la mpaka kabla sijaondoka hapa Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, zihakikishe zinatuma viongozi waende wakasimamie makabidhiano ya mpaka huo kwa sababu tunawanyima haki yao wananchi hao, kuendelea kuwaweka hewani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu suala la madini. Suala la madini bahati nzuri katika Wilaya ya Biharamulo, tuna mgodi mmoja unaitwa mgodi wa Turawaka na nafikiri tarehe 20 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atakwenda kuuzindua. Lakini hawa wawekezaji katika Sekta ya Madini, nimekuja kuwashtukia kitu kimoja ni kwamba hawathamini wananchi pamoja na mali zao walizozikuta pale. Wakati wanapeleka mitambo yao, wanapeleka vyombo vyao kwa ajili ya kuanzisha ule mgodi; kuna barabara moja waliyoikuta pale waliyokuwa wanaitumia, wameiharibu, imekuwa ni mahandaki matupu na hiyo barabara ndiyo ilikuwa ni tegemeo la wananchi wa pale.

Baada ya kuiharibu, tayari wameshajitengenezea barabara ya kwao, ile wameiacha katika hali mbaya. Wizara ya Nishati na Madini, nafikiri kabla hatujakwenda huko na mimi bahati Mwenyezi Mungu akijalia nitakuwa mmojawapo, nitapenda kabisa Mheshimiwa Waziri Daniel Yona, awasiliane na Kampuni hiyo ya Pangea. Hiyo barabara kwa kweli isipotengenezwa, lazima tupewe maelezo, maana wao ndiyo walioiharibu na wameiacha tu. Kwa hiyo, hiyo barabara ihakikishe inatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda niliseme ni kuhusu Hospitali yetu Teuli ya Wilaya ya Biharamulo. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hotuba yake alisema kwamba Hospitali zote za Wilaya na Rufaa zilipewa *X-Ray*.

Nakushukuru sana kwa hilo kwamba tulipewa *X-Ray*. Kwa taarifa, Mheshimiwa Waziri wa Afya, alipotembelea katika Wilaya ya Biharamulo, aliitembelea Hospitali Teule akaelezwa kwamba zile *X-Ray* zote ambazo zimepelekwa katika Wilaya mbalimbali na Hospitali za Rufaa hazina kitu kinachoitwa *printer*. Kwa hiyo, *printer* inapokosekana ina maana yule anayekwenda kuchukua picha hawezi akafanya *recording*. Matokeo yake yule aliyekwenda kuchukua picha ndiye anapaswa kwenda kutibu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa namna ya haraka sana hizo *printer* zipelekwe kwa ajili ya kukamilisha huo mradi wa kupeleka *X-Ray* ili ukamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa naomba nishauri ni kuhusu Vyombo vya Habari. Vyombo vya Habari kwa kweli vinafanya kazi nzuri, vinaelimisha, vinahabarisha na kuburudisha. Lakini nimefanya uchunguzi nikakuta kwamba wakati wanapokuwa wanasoma Taarifa ya Habari kwa mfano Redio Tanzania, *TVT, ITV, Radio One Stereo, Radio Free Africa* wanapokuwa wanasoma taarifa, wanasoma kama ni saa 2.00, wote wanasoma kwa pamoja.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba wakae pamoja na Baraza la Habari ili wapange wakati tofauti tofauti ili wananchi sasa tupate maonjo tofauti kuliko sasa ukifungua *ITV*, ukifungua *TVT*, ukifungua Radio Tanzania, zinagongana habari. Hivi kwa nini msikae pamoja mkapanga? Maana yake mnafanana na wale vimburu. Vinakaa pamoja hiki kinachimba, hiki kinaruka matokeo yake, hata jambo moja halieleweki. Kwa hiyo, nilikuwa naomba vikae pamoja Vyombo vya Habari, viweze kuhakikisha kwamba vinasoma taarifa kwa wakati tofauti ili wananchi waweze kujichagulia ni wapi wanaweza wakasikiliza. Huo ulikuwa ni ushauri. *(Makofi)*

Nilikuwa naomba tu niseme kwa kifupi kuhusu Sekta ya Madini. Sekta ya Madini Mheshimiwa Waziri Mkuu uliunda ile Tume. Ile Tume bahati nzuri ilipotuletea ile taarifa ili tuijadili, tukawa tumeahirisha na tulikuwa tunasubiri kwamba katika kipindi hiki zitatengwa siku maalum kwa ajili ya kujadili ile taarifa ya Tume. Lakini sijui kama bado mpango huo upo, maana tulikuwa tunataka tujielimishe.

Kwa mfano unaweza ukakuta pale kwenye mgodi unaoitwa Mgodi Nyamongo, niliwahi kusema siku moja kwamba pale kuna Askari kutoka nchi ya Nepal ndiyo walinzi wa pale na Nyamongo iko Ukuriani, iko Mkoa wa Mara na Wakurya ndiyo tunasema ni Jeshi la Ulinzi tangu zamani, kwa nini muwaletee Askari wa Nepal, watoke nchi ndiyo walinde ule mgodi?

Hilo ni jambo la kusikitisha sana kwa Wakurya kwa sababu wenyewe ndiyo walinzi, sasa mnawaletea watu kutoka nje, ina maana gani? Mimi nafikiria kwamba sijui Watanzania tuko wageni katika nchi hii! Mimi sijaelewa wewe utamtoaje Askari kutoka Nepal kuja kulinda huku? Ni jambo la kusikitisha sana. Naomba wale Askari waondolewe, tuwaajiri Wakurya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ambayo sikuitegemea. Kabla ya yote kwanza sitaweza kuzungumza lolote isipokuwa kutoa pole na rambirambi kwa familia ya Marehemu Abu T. Kiwanga - Mbunge wa Jimbo la Kilombero, naomba kutoa pole nyingi na vile vile namwombea Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia kabla sijaenda moja kwa moja katika Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ningependa kutoa pongezi za dhati kwa Marais wetu wateule, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kupitia Chama cha Mapinduzi, vile vile Rais wa Zanzibar na vile vile Mgombea Mwenza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Nawapongeza na ninawatakia afya njema, wafikie siku hiyo tupate ushindi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Vile vile, ningependa kusema kitu kimoja kwamba kwa Rais wetu wa Zanzibar kwa wale ambao walikuwa wanategemea kwamba safari hii watachukua Urais Zanzibar, nafikiri hii itakuwa ni ndoto ya alinacha. CCM itashinda na itashinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, ningependa kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wengine wote ambao waliiandaa hotuba hii ambayo ni hotuba nzuri yenye kuleta mwelekeo, yenye kuonyesha njia. Naomba kuwapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa muda wa miaka kumi kama walivyoeleza wao wenyewe katika hotuba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia mambo mawili/matatu ambayo nimeyaona katika hotuba hii. Naomba kuanzia na Menejimenti ya maafa ambayo iko ukurasa wa 50. Napenda kuzungumzia suala hili kwamba katika Menejementi ya maafa wamechambua, wameona, wamefanya utafiti, wameimarisha mambo chungu nzima katika Menejimenti hii na wametoa Sera ya Taifa ya Maafa. Kwa hiyo, nawapongeza. Lakini ningependa kuzungumzia kitu kimoja ambacho kama ni ushauri. Tumeona uimarishaji wa Jeshi la Zimamoto. Kwa kipindi kirefu tumeona majengo yanaungua moto, sijui kama utafiti umefanyika kuona chanzo chake.

Pia, jana tumeona Jengo la Kitega Uchumi cha Bima limeungua moto na hii ikiwa ni mara ya tatu. Lakini sasa sijui katika utafiti walioufanya walifanya pamoja na utafiti wa kujua chanzo cha majengo kuungua moto kiholela, mpaka Ikulu ikaungua moto. Kwa hiyo, nafikiri ni vyema katika utafiti wao ambao wanaufanya, wachunguze na chanzo cha majanga haya ya moto unasababishwa na kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia kwamba katika Mkoa wa Mwanza, Ziwa Victoria tumeona kuna majanga mengi tu ambayo yametokea. Tumeona kuzama kwa *MV Bukoba,* tumeona kuzama kwa ndege ambayo juzi ilikuwa inaendeshwa na Warusi. Sasa sehemu kama hii ingekuwa ni vyema tukaweka Kitengo Maalum cha

Uokoaji katika sehemu ile kwa sababu tulivyoona tukio lile la *MV Bukob*a ilikuwa muda wa siku ya kutafuta wazamiaji, wengine kutoka Zanzibar, wengine kutoka nchi za nje tukawakosa, watu wengi wakazama kutokana na kwamba hakuna Jeshi la ukoaji wa haraka haraka la wazamiaji na vifaa tulikuwa hatuna na tulivyokuwanavyo vilikuwa duni.

Kwa hiyo, walikuwa wanasaidia tu wananchi wa pale wenye mitumbwi na kadhalika. Kwa hiyo, nafikiri ni vyema kuweka kitengo maalum pale kwa sababu tunajua kwamba majanga yanatokea pale hatuombi yatokee mengine, lakini tujihadhari kwamba lazima tuweke kitengo cha uzamiaji na uokoaji na vifaa vya kisasa ili kama litatokea janga la namna hiyo, basi tutakuwa tunasaidia kuokoa wananchi na mali zetu kwa haraka haraka ili tusipoteze kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni janga la Ukimwi. Naliita janga kwa sababu linatumalizia nguvu kazi za vijana wetu. Kwa hiyo, hili naliita ni janga vile vile. Ni vyema tuendelee kutoa elimu. Tunatoa elimu Mijini sana kuliko Vijijini, tunasahau kama na kule binadamu vile vile wanaweza wakapatwa na janga hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba inaonekana wanapata elimu kidogo, lakini hata hivyo nguvu nyingi zinaelekezwa Mijini. Ingekuwa vyema basi Vijijini nao wakapata taaluma nzuri zaidi kwa kupitia viongozi wetu wa Vijiji, kupitia Viongozi wetu wa Mikoa.

Mifano hai imejitokeza katika kiambatanisho cha hotuba yako namba kumi inaonekana asilimia 10.9 ya wakazi wa Mijini ambao waliathirika na asilimia 5.3 wa wakazi wa Vijijini ambao ni waathirika.

Hii inaonekana kwamba Vijijini bado hawajajitokeza asilimia kubwa kwamba Vijijini wameathirika wengi, lakini hata hivyo ningeomba elimu ipelekwe Vijijini. Kuna Mikoa ambayo imejitokeza ambayo ina asilimia kubwa ya waathirika mfano Mkoa wa Mbeya asilimia 13.5, Mkoa wa Iringa asilimia 13.4 na Mkoa wa Dar es Salaam asilimia 10.9. Haya siyasemi mimi, nasema kutokana na maandiko yaliyoandikwa katika hotuba hii.

Hii inaonekana bado elimu haijawafikia vizuri kwa sababu tunatoa elimu Dar es Salaam tu, tunasahau kutoa elimu katika Mikoa mingine ambayo iweze kusaidia na kujua ya ugonjwa huu na kwamba hauna dawa na unatumalizia nguvu kazi yetu nyingi na inatumalizia vijana wengi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Vile vile, napenda kuzungumzia kwamba pamoja na kwamba tunatoa elimu ya kujikinga ya kujihadhari, lakini vile vile tuone kwamba jinsi gani tunawasaidia hawa vijana wetu waathirika kwanza. Vile vile, tuwasaidie hawa vijana ambao walioachwa na wazazi wao ambao hawana pa kwenda mpaka sasa hivi, kuna watoto ambao wamefiwa na baba, wamefiwa na mama hawana pa kwenda wapo tu wanazurura katika Mitaa.

Nafikiri Serikali ingejikita zaidi kuwasaidia hawa yatima. Najua kuna *NGOs* zinasaidia, lakini kama Serikali haijajikita moja kwa moja kusema kwamba sisi tunasaidia hawa kutokana na wazazi wao kwamba wamefariki tukawa sisi tunaachia *NGO* tu moja kwa moja, nafikiri ni vyema Serikali ikawa inajihusisha moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu huduma za jamii kwa ujumla. Kwanza natoa pongezi kwa Chama cha Madaktari Wanawake ambao wamejihusisha moja kwa moja na kujitolea muhanga kwa kuwasaidia wanawake wenye kansa ya matiti.

Kuna wanawake ambao wanaishi hapa duniani hawajijui maskini kama wao tayari wamekuwa na matatizo haya ya matiti, wanaona ni mambo ya kawaida. Kwa sababu wakati mwingine anaweza akapata maumivu wakati hapati maumivu. Kwa hiyo, yeye hashughuliki na kujipima kuona kwamba afya yake ikoje.

Lakini ninawapongeza sana Chama hiki cha Madaktari kwa kusaidia hawa kina mama kuweza kujitokeza kwa wingi na tunaona michango mbalimbali inatoka kwa kuwasaidia wanawake hao. Lakini ningependa vile vile isishughulikie Mkoa wa Dar es Salaam peke yake, kuna Mikoa mingine ambayo akina mama hawawezi kusafiri kutoka katika Mikoa yao kwenda katika Mkoa wa Dar es Salaam ili kujitokeza nao waweze kupimwa na kujulikana kama wameathirika au hawajaathirika. Kwa hivyo, ningependa Madaktari hawa wajishughulishe sana katika Mikoa iliyokuwa pembezoni, pengine wanawake hawawezi kujitokeza na kuja huku Mkoa wa Dar es Salaam na kujishughulikia kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, lingine ningezungumzia kuhusu Hospitali ya *Ocean Road.* Ninawapongeza Madaktari, wanahudumia sana wagonjwa, wamejitahidi sana wamekarabati jengo lao vile vile, huduma ni nzuri nawashukuru sana. Lakini kwa kuwa ugonjwa wa saratani sasa hivi unaongezeka kwa kasi mno, wagonjwa ni wengi sana, ukienda pale utaona ni jinsi gani wagonjwa walivyokuwa wengi walioathirika kwa saratani tofauti. Kwa hiy,o ningependa, pamoja na kwamba wamefanya ukarabati mzuri, lakini vile vile zingeongezwa *wards* za wagonjwa. Kwa sababu mimi mwenyewe nimekwenda pale na kuona *ward* ya watoto, wanalala kitanda kimoja watoto watatu au wanne.

Kwa hiyo, utaona kwamba *wards* ni finyu mno, ziongezwe *ward* na vile vile kuna wagonjwa ambao wanataka kujilipia wao wenyewe. Vile vile, itasaidia kwa upande mwingine watapata pato zaidi. Wangeweka basi *Grade "A"* pengine kuna wagonjwa wanataka kujihudumia pale na kulipa kidogo kwa kusadia. Kwa hiyo, ingekuwa vizuri zikaongezeka *wards* ili wagonjwa wasiwe wanasongamana kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni kukupa pongezi wewe kama Spika kutuongoza katika miaka hii yetu 10. Umetuongoza vizuri na vile vile matokeo ya uongozaji tumeyaona. Vile vile, umejitahidi kukarabati Ofisi ya Dar es Salaam, umejitahidi kujenga Jengo la Bunge hili hapa ambalo tunaliona, halikadhalika na

Jengo la Bunge la Zanzibar pia unajitahidi. Kwa hiyo, hii yote ni juhudi yako kama Spika na Uongozi wako kwa ujumla. Kwa hiyo, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo yote mazuri uliyoyafanya, lakini kuna moja dogo ambalo ningekuomba Mheshimiwa Spika kwamba Ofisi za Wabunge bado ni kilio na ni kero kubwa mno. *(Makofi)*

Ukiangalia kwamba Waheshimiwa Wabunge tumepewa bendera, lakini mpaka leo hatujui tuziweke wapi kwa sababu Ofisi hatuna. Wengine wamejenga majumba yao, wameweka bendera mbele ya majumba yao, kwa hiyo, tuseme wapigakura wao wanakwenda majumbani mwao! Wengine hata hatuna Ofisi, tuweke wapi?

Tunakwenda katika Ofisi za Wilaya, sasa kama Ofisi za Wilaya ni kubwa hujui bendera ya Mbunge utaiweka sehemu gani, unaambiwa tuingie katika Ofisi za Wilaya, tuingie katika Ofisi za Mikoa, utaiweka wapi sasa hiyo bendera? Ili ajulikane Mbunge yuko hapa, wapigakura wako wanababaika hawajui waende wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri mazuri hayo uliyoyafanya ya kujenga Ofisi za Bunge na ufanye mazuri ya kufikiria kujengea Wabunge Ofisi zao, kwa upande wa Bara, nafikiri pia hakuna na upande wa Visiwani pia hatuna Ofisi za Bunge. Kwa hiyo, naomba ulifikirie hili suala.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu Hisa za Benki ya Dar es Salaam, *City Bank*. Kwa kweli hili suala la *Community Bank* ningeomba kulisema hapa. Ni kwamba linatuumiza sisi Wabunge tulioingia Hisa katika Benki ile. Kumbe Benki ile ilikuwa bado haijaingia katika Soko la Hisa, halafu wao wakaja wakatuambia kwamba jiungeni mpate Hisa katika Benki hii. Sasa mambo haya yakoje? Tunapata utatanishi hapa, hatujui tufanye nini, hatujui tumwendee nani! Tukienda huku tunazungushwa, tumekuwa watoto wa kambo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba tupate ufafanuzi wa hili twende wapi. Kwa sababu sasa hivi wanasema bado faida hatujapata, japokuwa wametangaza jana kwamba tutapata faida. Lakini mpaka leo sisi kama ni Wanahisa hatujafanikiwa hicho kitu. Kwa hiyo, tunazungushwa tu.

Mheshimiwa Spika, lingine ningeomba kupongeza kupitishwa asilimia 30 ya wanawake. Nashukuru sana ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kuhusu Ofisi za Wabunge, napenda kumwarifu Mheshimiwa Salama Khamis Islam kwamba tarehe 25 mwezi huu wa Juni, 2005 nakwenda kufungua Ofisi ya kwanza ya Mbunge katika Jimbo la Longido, ambayo imekamilika. *(Makofi)*

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wa mawazo yangu katika hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini kabla pengine sijaendelea na mchango wa mawazo yangu, naomba niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Abu Kiwanga. Namwombea kwa Mwenyezi Mungu, roho yake iwekwe mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, kabla sijaanza kutoa mchango wa mawazo yangu, naomba nitumie nafasi hii niishukuru Serikali kwa jambo zuri ambayo imenifanyia katika Wilaya yangu ya Kishapu.

Jambo ambalo nataka nilizungumzie ni juu ya wachimbaji wadogo wadogo katika Mji wa maganzo ambao kwa muda mrefu kwa kweli walikuwa wameleta maombi yao ili waweze kupatiwa eneo la kuchimba madini. Kama tunavyofahamu, kwa utaratibu uliopo, Serikali ilitoa kipaumbele kwa wachimbaji wakubwa tu, ikawasahau hawa wachimbaji wadogo. Lakini kwa hali ya sasa na kwa taarifa ambazo ninazo, Serikali imetoa maeneo kwa wachimbaji wadogo kwa maeneo ya Maganzo. Kwa hiyo, kwa niaba ya wachimbaji, napenda nitumie nafasi hii kwa kweli niishukuru sana Serikali kwa kutambua hilo. *(Makofi)*

Baada ya hayo, sasa nataka nianze kutoa mchango wa mawazo yangu katika hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza nampongeza kwa hotuba yake nzuri, kaelezea mambo mengi mazuri tu na wengi tunayakubali, isipokuwa na sisi kama moja ya kazi ya Mbunge kwanza ni kuishauri, kuikosoa na kuisadia Serikali ili itawale vyema. Kwa hiyo, nami nataka niongezee machache katika kuboresha hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini pengine katika hayo nitakayoyazungumza, mengine yataelekea zaidi kwenye eneo ninaloliwakilisha. La msingi ambalo nataka niliongelee hapa, katika hotuba ya Waziri Mkuu nimejaribu kuangalia sehemu nyingi, sikuweza kuona eneo ambalo linazungumzia suala la njaa. Nimeangalia sana, lakini sikuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia njaa ipo katika maeneo mengi sasa katika nchi yetu. Nadhani wote tunafahamu hali ya hewa ilivyokuwa. Mimi nataka nilizungumze bila uoga, mimi katika Jimbo langu la Kishapu nina hali mbaya, nina njaa kubwa. Kwa hiyo, nilishindwa kuelewa baada ya kusoma humu sikuweza kuona jitihada za Serikali kusaidia suala hili la njaa. Nadhani siyo Kishapu, nimetembea maeneo mengi, sehemu kubwa ya Mkoa wa Shinyanga na maeneo mengine yote, lakini hapa pako kimya kabisa hapakuzungumziwa nini jitihada ya Serikali kusaidia suala la chakula katika maeneo yalioyo na njaa. Labda Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza akatusaidia.

Vile vile, tukumbuke hasa tunakwenda kwenye kipindi cha uchaguzi ambacho kwa kweli kingehitaji watu wakae kwa amani na utulivu, wafanye kazi za uchaguzi kwa utulivu bila kuwa na matatizo yoyote. Sasa kama watakuwa na njaa, nadhani hata uchaguzi huu unaweza ukawa wa matatizo sana. Nilikuwa naomba pengine Mheshimiwa Waziri Mkuu labda atusaidie suala la njaa Serikali inalichukuliaje?

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyosema, ninakotoka tayari watu wameanza kuja kwangu kulalamikia suala la njaa. Sasa tunaomba Serikali ilipe uzito wa aina yake. Ni tatizo kubwa! Labda nilielezee kwa kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani Serikali ilikuwa imetoa msaada wa chakula kwa watu wa upande wa Shinyanga. Ilitoa nadhani tani 360 Maswa na Meatu, Kishapu nilipewa tani 60 ambazo hazikuweza kusaidia. Nilijaribu kuwasiliana na Waziri

wa Nchi, Ofisi ya WAziri Mkuu, Mheshimiwa William Lukuvi, nikamwuliza; ni kwa nini nimepewa tani 60 tu wakati nina matatizo makubwa? Maana Shinyanga maeneo ambayo yenye matatizo makubwa hasa ni Kishapu na Meatu. Nikaambiwa kwamba, mgao uliopewa ndio huo. Nilipewa majibu ya mkato tu. Vinginevyo nenda *SGR*. Basi, kwa sababu ilikuwa ni simu nilikata, niliona nisiendeleze hoja, tunaweza tukaleta vurugu tupu, nikaacha.

Lakini nataka tu niseme kwamba tuna hali hiyo ya njaa. Kwa hiyo, tunaomba Serikali isadie. Ni kweli ni jukumu la mwananchi yeye mwenyewe kujilisha. Lakini inapotokea tatizo kama hili, basi ni wajibu wa Serikali kumsaidia ili apate chakula na aweze kulichangia pato la Serikali. Kwa hiyo, naiomba Serikali isaidie kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie, nadhani nizungumzie juu ya hili suala ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Waziri kihusu utekelezaji wa mkakati wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Mimi nadhani ni wazo zuri ambalo amelizungumzia katika hotuba yake na wananchi sehemu nyingi kwa kweli wameitikia wito huo na wamekuwa wakitoa mchango mkubwa tu kusaidia kujenga uchumi wetu wa Kitaifa. Lakini nataka nionyeshe ni wapi ambapo nina wasiwasi kama kweli Serikali inatambua juu ya mchango mkubwa wa wananchi. Ninataka nijielekeze kwa kweli kwenye sehemu ya wananchi wanaolima zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, juhudi za wananchi katika kuinua uchumi kama nilivyosema ni kubwa isipokuwa mimi nataka nizungumze kabisa, Serikali sijui kama inatambua juhudi zao au sijui ni namna gani! Nataka nizungumzie juu ya suala la wakulima wa pamba. Kwa mfano mwaka jana katika Bunge la Bajeti tulipokutana hapa, tulikaa pamoja na Waziri Mkuu na baadhi wa Wabunge wanaotoka Mikoa inayolima pamba, tukakubaliana kwamba zao la pamba kwa sasa hivi kila kilo itauzwa kwa Sh.250/= na radio zilitangaza na watu wote walijua hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kurudi kwenye maeneo yetu, bei ya pamba iliteremshwa sijua na wafanyabiashara kwa sababu ya kuwapa uhuru, sijui biashara huria, wakauza kila kilo shilingi 180/=. Tulihoji kwamba Serikali imetamka kupitia kwa Waziri Mkuu kwamba kilo moja ya pamba ni shilingi 250/=, kwa nini imeteremka mpaka shilingi180/=? Wakasema kama mnaona nyinyi bei hiyo ni ya chini, basi nunueni wenyewe. Ndio majibu tuliyopewa.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niseme tu kwamba mimi naona pengine hata hii biashara huria Serikali imeipa uhuru mno. Wafanyabiashara wanafanya wanavyojua, wanavyotaka siyo biashara huria sasa ni biashara holela. Nimejaribu kuangalia hata jinsi pamba ilivyokuwa inauzwa nje, kwa mfano mwaka 2004 thamani ya mauzo ya pamba iliongezeka kwa asilimia 60.4 hadi Dola milioni 74.6, kutoka Dola milioni 46.5 mwaka 2003. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mauzo ya pamba kwa asilimia 52 kutoka tani 46,900 mwaka 2003 hadi tani 71,300 Mwaka 2004. Bei ya pamba, katika soko la Dunia iliongezeka kwa asilimia 5.4 hadi kufikia Dola 1,045.7 kwa tani

mwaka 2004 ikilinganishwa na Dola za Marekani 992.0 kwa tani mwaka 2003. Sasa hii ndio bei ya Soko la Dunia.

Lakini sasa ukiingia kwa upande wa soko la kwetu, bei ilitangazwa ni Sh.250/=, lakini utekelezaji wake ni Sh.180/=. Tumejaribu kuhoji; je, ni kwa nini tumefikia hatua hiyo? Jibu hakuna. Lakini mimi ninachotaka nikiseme tu ni kwamba Serikali imetoa uhuru mkubwa kupita kipimo kwa wafanyabiashara pamoja na kwamba ni kweli tuko katika biashara huria. Nadhani moja ya kazi ya Serikali ni kusimamia na kuangalia haki inatendeka. Sasa je, kwa mfano hawa wakulima wa pamba bei ya pamba inateremka mpaka kufikia Sh.180/=, tamko la Waziri Mkuu alizungumza Sh.250/=, sasa, hivi kauli inayoheshimika ni ya Waziri Mkuu au ya wafanyabiashara? Sasa mimi nasema, niiombe Serikali iweke jitihada kubwa katika kusimamia mambo haya, pamoja na kwamba haiwezi kupanga bei. Sasa ni kweli huwezi kupanga bei, lakini hata biashara unapoona kweli hapa wananchi wanaonewa Serikali ikae kimya?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba kwa hili Serikali yetu ijaribu kusaidia wakulima ili utekelezaji wa mkakati wa kukuza uchumi, basi twende nao vizuri. Tukumbuke hawa wakulima wanafanya kazi kubwa, ni wavuja jasho, sasa wanachotegemea nao wapate haki yao.

Lingine ambalo nataka nilizungumze ni juu ya mgao wa fedha za kimaendele. Mgao wa fedha pato la Taifa nadhani mwaka jana mimi niliongea sana juu ya mgao wa fedha hizi za kimaendeleo. Ilionekana baadhi ya Mikoa mingine wanapewa pesa kidogo. Nilizungumza kirefu, kwa hiyo, najaribu kuangalia ukisoma hiki kitabu cha mpango wa maendeleo wa mwaka 2005/2006 unaonyesha kidogo inaridhisha juu ya mgao wa fedha za ndani. Lakini ukija kuchanganya na mgao wa fedha za nje, bado hali ni ile ile au ni mbaya zaidi.

Kwa mfano walio na kitabu hiki wanaweza wakafungua ukurasa wa 51, kwa mfano Mkoa wa Pwani ukijumlisha fedha zote za ndani na za nje wana Shilingi bilioni 7.9. Halafu Dodoma wana Shilingi bilioni 4.9, Iringa Shilingi bilioni 5.6 sasa ukija hawa ndugu zangu wale wale waliokunywa uji wa mgonjwa Kigoma Shilingi milioni 577 na Arusha ni wale wale Shilingi milioni 471, halafu ukija hapa Shinyanga Shilingi milioni 770. Sasa mimi bado naendelea kuzungumza, hivi ndugu zangu huyu aliyepata bilioni saba na huyu aliyepewa Shilingi milioni 400 kama Arusha, Kigoma, Tabora, Rukwa, Rukwa wamepewa Shilingi milioni 519, hivi haya maendeleo tunayoyazungumzia, maendeleo si ya haki na usawa, hivi kweli tutalingana kwa hali hii? *(Makofi)*

Tulikuwa tukizungumzia juu ya suala hata la madini, kulikuwa na wakati fulani mimi nilikuwa nazungumzia suala la madini kwamba haya madini hatuoni faida tunayopata sisi wenye maeneo ambayo yanayochimbwa madini. Ikatokea lugha ukisemwa sijui yasaidie kwako je, na mwenye makaa ya mawe sijui na mwenye nini!! *Okay,* mimi nikakubali kwamba tukubali kwamba sasa tuchangie wote kweli hili pato la Taifa tuweze kupata chochote kinachopatikana kwa usawa. Lakini mimi nauliza, basi kwa hali hii ya Shilingi bilioni saba mpaka Shilingi milioni 519, tutakwenda sawa kimaendeleo? *(Makofi)*

Sasa ndugu zangu mimi nilikuwa nafikiri katika utaratibu wa mipango wenzetu mnaokaa kupanga hii mipango, pangeni basi mipango ambayo italeta usawa. Wote tuko hapa kuwakilisha mawazo ya wananchi, wote tuko hapa kutetea maendeleo katika Mikoa yetu. Sasa huyu wa Shilingi bilioni saba na Shilingi milioni 500, nani atakayekwenda kasi zaidi? Sasa nitakufikisha mahali tuhoji ni Mkoa gani unaotoa mchango mkubwa Kitaifa na unasaidiwa nini?

Kwa mfano mimi ninavyofahamu, pamoja na uelewa wangu mdogo, Mkoa wa kwanza najua ni Dar es Salaam, wa pili Mwanza, wa tatu ni Shinyanga. Lakini je, pamoja na mchango wake mzuri, unatendewa haki kweli kupewa pesa za kimaendeleo? Hakuna! Sasa hili ndugu zangu mimi nadhani tuliangalie. Nadhani tofauti kubwa ya kimaendeleo itaendelea kuwa kubwa tu.

Sasa mimi naomba katika kupanga mipango yetu, jambo hili tuliangalie. Tuna matatizo mengi sana. Tatizo la barabara, matatizo ya maji, tunahitaji umeme, tunahitaji ujenzi wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Sasa tofauti hizi kubwa zinaonyesha kabisa wazi kwamba maendeleo yetu kwa hali yoyote yatatofautiana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWANAMKUU MAKAME KOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nikiendelea, naomba nitumie fursa hii kuungana na wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa wenzetu familia ya Marehemu na Wapigakura wote wa Kilombero kwa kufiwa na Mheshimiwa Mbunge wao Mheshimiwa Abu Kiwanga. Namwombea Dua Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema Peponi roho ya Marehemu. Amina.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea naomba pia nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Wagombea wetu tuliowachagua kule Chimwaga, wa kwanza akiwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ndio Mgombea wetu wa Urais na tuna matumaini ya mia kwa mia kwamba Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ataibuka Rais kwa mwaka 2005/2010. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuchaguliwa tena kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar kwa kipindi chake kingine. Nampongeza pia Mheshimiwa Ally Mohamed Shein kwa kuteuliwa kuwa Mgombea mwenza wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ndiye Rais wetu mtarajiwa. *(Makofi)*

Pia, napenda niwapongeze Mawaziri wetu ambao tayari wameshapitishiwa hoja zao, lakini pia niwapongeze na wao kwa sababu ilikuwa ni Bajeti nzuri ya kutia moyo kabisa. Nikianza sasa na hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kwanza nimpongeze na yeye kwa kazi nzuri iliyofanyika hata mpaka tukapata hotuba kama hii. Ni hotuba nzuri ambayo imezingatia mambo yote muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitazungumzia machache tu nikizingatia kuwa yeye Mheshimiwa Waziri Mkuu ndio kiongozi msimamizi wa Serikali na Wizara zote kwa ujumla. Katika hotuba hii nitatoa ombi au ushauri juu ya tatizo letu linalotukabili. Lakini kwanza niipongeze sana Serikali yetu hii ya Awamu ya Tatu kwa kazi nzuri iliyofanyika. Kwa hakika wenzetu hawa Viongozi wataondoka katika madaraka kwa hivi sasa tu, pengine baadaye watarudi tena. Mheshimiwa Rais ameshamaliza kazi yake, lakini wengine huenda wakarudi tena kwa mara nyingine.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa hivi sasa wanaondoka katika hali nzuri na kama tunavyoona ahadi zote zilizomo katika Ilani ya Uchaguzi tayari zimekamilika. Kwa hiyo, tuna matumaini kwamba watakaokuja kushika madaraka kwa mara nyingine, basi nao watafuata nyayo kuendeleza mambo haya ili tuweze kuendelea vizuri ili tuweze kukuza uchumi wetu sawasawa au tuweze kukuza uchumi wetu zaidi na zaidi wananchi wetu wapate kukwamuka kutoka katika hali ngumu hii ya umaskini walionao.

Kwanza nitazungumzia juu ya upandaji bei wa mafuta yakiwa ya *petrol*, *deseal* na hata mafuta ya taa. Bidhaa hii kwa kweli ni bidhaa muhimu inayomgusa kila mtu katika nchi hii na bidhaa hii inapanda bei kila baada ya mwaka na wakati mwingine haufiki hupanda hata katikati ya vipindi. Ukitizama bidhaa hii, ikipanda ya mafuta kwa kweli ni kupanda kwa mambo yote yaliyopo nchini, kuanzia nauli mpaka nyanya za kupikia.

Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa linalotukabili ambalo nataka niiombe Serikali ifanye kila njia, ikae itafakari tuweze kupunguza kidogo bei hii ya mafuta ili angalau tuwapunguzie mzigo wa hali ngumu ya uchumi wananchi wetu.

Najua kwamba mafuta yakipanda hayapandi hapa kwetu tu Tanzania, ni mambo ya Ulimwengu mzima. Lakini hata hivyo, ningeiomba Serikali kama tulivyopunguza mafuta ya ndege tufanye utaratibu wa hali ya juu. Najua ni kazi kubwa, najua ni tatizo kubwa litakalotukabili kwa sababu pale napo tulikuwa tukipata mapato kiasi fulani. Lakini hata hivyo, wananchi wetu tutawasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mzigo waliobeba kwa sababu mafuta ni jambo tunalolitumia kwa mambo mengi sana. Mafuta ya gari tunayotumia kwa mambo ya gari, ndio nauli na nauli ni kitu cha lazima. Mafuta ya taa vile vile, tunatumia kwa kuona kama tunavyoona umeme wetu sio kote katika Tanzania ulikofika.

Kwa hiyo, mafuta ya taa nayo pia ni kitu kinachotumika na ni jambo muhimu sana katika nchi yetu na kwa watu wote. Sasa naiomba Serikali iweze kufikiria zaidi juu ya suala hili la upandaji bei wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu walio wengi au zaidi ya robo tatu hawapandi ndege, wanaopanda ndege ni hao watu wengine wanaojipatapata au pengine ni kwa sababu ya hawa watu wetu wawekezaji na hawa wawekezaji wetu ni vizuri kuwawekea mazingira mazuri. Kwa hiyo, mimi hilo sina tatizo nalo, lakini vile vile ni vizuri kuwawekea mazingira mazuri yakipungua pia wananchi wetu waweze kujikimu katika maisha maana yakipungua bei mafuta itakuwa nafuu ya matumizi imepatikana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hali ya wanafunzi wetu, wanavyodhalilika hasa watoto wetu, dereva anaona akimpakia mwanafunzi kwenye gari na kutokana na bei ya mafuta ilivyo, tayari ameshapata hasara. Kwa hiyo, utaona watoto wengine wanarudi majumbani mwao usiku. Kwa hiyo, wanadhalilika kiasi fulani na watoto wengine wa kike hubidi wadhalilike zaidi, wanyanyasike zaidi. Yote ni kugombea wapate ule usafiri na hii yote huletwa na matatizo ya bei hii ya mafuta iliyopanda au inayopanda mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili la upandaji bei wa mafuta tukae kitako katika Serikali yetu tulizingatie suala hili la upandaji wa bei ya mafuta ili tuweze kufanya utaratibu tupunguze kidogo hii hali ngumu inayotukabili.

Mheshimiwa Spika, pili nizungumzie juu ya madawa ya kulevya. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kaeleza hapa kwamba kuna hatua chungu nzima Serikali inachukua na zinaonekana. Inachukua hatua kutaka kudhibiti haya dawa za kulevya katika kuingizwa humu nchini mwetu na vile vile inachukua hatua kudhibiti hawa watoto wetu waache kutumia dawa za kulevya. Pia, Serikali inachukua hatua, mimi nakubaliana nayo. Kuna tume chungu nzima tu zilizoundwa. Ndani ya Tume hizi kuna Maaskari wa kila namna, lakini bado madawa ya kulevya ndio kitu kinachoshamiri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa kwanza Mijini tu mambo haya ya madawa ya kulevya, lakini mpaka sasa hivi Vijijini ndio Vituo Vikuu vya mambo haya ya madawa ya kulevya. Sasa utaona matatizo ya dawa za kulevya ni sumu kubwa katika nchi yetu! Watoto wetu wengi sana wanakataa kusoma, hawasomi hasa kutokana na kujiunga katika vigenge hivyo vya mambo ya dawa za kulevya.

Sasa sisi wenyewe tunapiga kelele kuwa watoto wetu wapate ajira, wasome wapate elimu, lakini madhali tatizo hili hatujalipatia ufumbuzi mzuri, basi nina wasiwasi sana. Katueleza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake kwamba kuanzia mwaka 1997 mpaka huu mwaka 2000 dawa zilikamatwa kiasi cha kilo 3,300 na kitu, lakini hapa kaandika madawa ya viwandani.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui hii kakusudia kuwa ndio dawa za viwandani, ndio madawa yenyewe ya kulevya au madawa gani! Lakini tatizo hili ni tatizo kubwa na mimi nina wasiwasi kwamba hawa wanaosababisha mambo haya ya kuleta madawa ya kulevya, hawapati adhabu ya kutosha au Sheria bado ni nyepesi sana inakuwa haiwashi hata wao. Vile vile, wanapokamatwa kwa sababu hapa kaandika wamekamatwa na wamechukuliwa hatua. Lakini hakutueleza ni hatua gani zilizochukuliwa au ni adhabu gani hawa watu walizopewa.

Mheshimiwa Spika, pia, nina wasiwasi mkubwa kwamba labda hata hivyo adhabu zinazotolewa ni adhabu hafifu sana ambazo haziwatishi kabisa. Hawa ni makatili, hawa ni mahaini na wamefanya mpaka vijana wetu hawa ambao tunawategemea kuwa ndio Taifa letu, hawa ndio Taifa letu la leo na kesho na ndio nguvu kazi yetu hii, hawa vijana. Lakini naiomba Serikali sasa ichukue juhudi tena zaidi kwa sababu jamani, mtaona labda

dawa za kulevya kuna uchawi unaofanyika ndani yake. Kweli ulinzi wetu au hii *system* yetu yote ya ulinzi hawawapati hawa watu wanaosababisha mambo haya. Basi, naweza kusema labda kuna ushirikina, lakini na sisi tufanye namna ili tuweze kuwakamata hawa watu kwa sababu hao ni wahaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi kwa sababu naona nimeshakaribia mwisho niseme tu haraka haraika juu ya hii *4.5 percent*. Tulikuwa tukipiga kelele kwamba tunataka Tume hii ya pamoja ya fedha iundwe. Tume tayari imeundwa, lakini hatuoni utaratibu unaoendelea hii kuweka kiwango hicho cha aslimia hiyo kwa kweli imeshapitwa na wakati. Sasa Tume ipate nafasi ikae ilijadili hili suala ili *4.5 percent* angalau ibadilike tupate *percentage* nyingine ya mgao wa misaada husika.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwamba kwa sababu huu ni wakati wa lala salama, niwaombee dua Waheshimiwa Wabunge wanaokwenda Majimboni kugombea. Niwaombee Wabunge wenzangu wa Viti maalum na wengine watakaoingia katika Bunge kwa kipindi hiki cha mwaka 2005/2010. Nawatakia kila la kheri, Mwenyezi Mungu awajalie muweze kuwashinda hao Wapinzani watakaokuwepo huko, muingie tena Bungeni kwa kipindi cha mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, pia nami mniombee dua kwa sababu mara hii mwenzenu sigombei, sina adhima ya kugombea kabisa. Nawashukuru wenzangu, nashukuru Chama changu, nawashukuru Wanawake wenzangu *UWT* naishukuru sana. Nawashukuru wanawake wenzangu wote na Chama changu, kwa kweli ni jambo kubwa walilonitendea, nashukuru sana na naendelea kushukuru, sasa ni lazima niwaombee na wenzangu dua kwa sababu mimi hiki ndio kipindi changu cha tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaombea dua na nyie muweze kuingia katika kipindi kijacho na *inshallah,* tutaweza kukutana japokuwa sitaingia humu ndani, lakini tutakutana japo kwa nje. Kwa sababu muda bado upo, nigusie tena kuhusu mambo ya ubinafsishaji. Mambo haya ya ubinafsishaji ni mambo mazuri sana. Ni kitu kizuri sana kubinafsisha Mashirika yetu ambayo yametushinda. Lakini siku zote tunapiga kelele kuhusu ufuatiliaji. Tusitosheke na kubinafsishwa tu, ufuatiliaji uwepo kwa sababu hao wanaochukua Mashirika wengine wanajifanyia mambo watakavyo. Katika ajira, wanaajiri watu ambao pengine sio Watanzania na sisi tunapiga kelele watoto wetu wapate ajira. Adhima ya kubinafsisha ni kwamba watoto wetu wapate ajira na nchi ipate maslahi zaidi.

Lakini utaona ufuatiliaji bila kupiga kelele bado haupo, Mashirika mengine toka yabinafsishwe bado hayapitiwi wala hayajafanywa chochote. Wale waliobinafsishiwa hawayaulizi, wao wamekomea milango yao, hawafanyi kitu chochote hapati na sio lengo letu. Kwa hiyo, ningesisitiza zaidi kwamba ubinafsishaji utakua lakini na ufuatiliaji uwepo, tena wa hali ya juu kuona watoto wetu wanapata ajira zaidi na Serikali yetu ipate kipato zaidi kwa sababu hayo ndio malengo yetu tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nizungumzie juu ya soko la matunda. Sasa hivi wakulima wetu walishajinawirisha kwa kupanda matunda ya kila aina. Lakini utaona katika Mikoa mingi sana matunda yanaonza, kwa mfano machungwa, mananasi,

yanaozeana. Ningeishauri Serikali kama tulivyowahamasisha hawa wakulima wapande mazao kama haya ya matunda na mambo mengine, basi tutafute soko kwa ajili ya matunda na mambo mengine tupate soko na wananchi wapate moyo zaidi wa kuendeleza kilimo hiki waweze kujinasua kiuchumi. Pia wasaidiwe au Serikali iwe na mpango wa kuwafundisha wakulima walime kwa kutumia mbegu zitakazoweza kupata soko na pia namna ya kuhifadhi matunda yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia kwa mia ahsante.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze na mimi kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kwanza nitoe pole kwa msiba mkubwa uliotupata sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge pamoja na familia na Wapigakura wa Marehemu Mbunge Abu Kiwanga wa Jimbo la Kilombero, uliotokea mwezi uliopita. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe pongezi na kukishukuru Chama chetu cha Mapinduzi na Wapigakura wa Chama cha Mapinduzi waliofanya jambo zito na la kihistoria tarehe 4 mwezi Mei, 2005 na kuweza kumrejesha Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kuwa Mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, pamoja na Mgombea mwenza wake Dr. Ali Mohamed Shein. Hali kadhalika, pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa fursa aliyoipata tena kugombea nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, sasa nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi alivyoiwakilisha hotuba yake nzuri katika Bunge letu Tukufu. Kwa hakika kama ingekuwa sio utaratibu wa kuchangia, tungesema hii inapita bila kupingwa kutokana na jinsi alivyoipangilia na hotuba ya miaka kumi alivyoweza kuifupisha na kutuwezesha sisi kuielewa vizuri. Nampongeza kwa uwezo huo pamoja na Mawaziri na Watendaji Wakuu wa Ofisi yake. Kwa misingi hiyo, nisije nikasahau, naipongeza naiunga mkono mia kwa mia kuanzia sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye kipegele cha maendeleo ya jamii na kijinsia ambayo kwenye hotuba yake aliitolea maelezo. Kipengele ambacho nataka kukizungumzia ni kile cha ongezeko la asilimia 30 kwa Viti vya Wabunge wa Viti maalum. Natoa shukrani za dhati kabisa mimi mwenyewe kwa nafsi yangu na wenzangu ambao ni watarajiwa Wagombea wa Viti maalum Mkoa wa Shinyanga kwa jinsi walivyofurahia nafasi hii kwa sababu safari hii kila Mkoa kunatoka Wabunge wawili. Atakayebahatika namba moja na namba mbili, basi tunasubiri tu kuapishwa Mheshimiwa utakapokuwa kwenye Kiti chako. *(Makofi)*

Tunashukuru kwa sababu kidogo *pressure* ya kukanyaga kama sisimizi walivyoisema Waandishi wa Habari, imepungua. Kwa hiyo, nafasi hii tunaishukuru Serikali. Lakini pia wanawake wa Mkoa wa Shinyanga ambao ndio nawawakilisha, nao pia waliniomba niwasilishe ombi lingine mbali ya hii asilimia 30. Ombi hilo ni kuhusu

ongezeko la kima cha mikopo inayotolewa na Serikali. Maadam Serikali imeweza kufikiria kuongeza asilimia thelathini ya nafasi za Bunge, basi haitakuwa vibaya kama Mheshimiwa Waziri Mkuu ukaangalia mafungu yako ukaongeza pia asilimia ya fedha ambazo wanawake wanapewa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wale ambao watashindwa kupata Ubunge, wale ambao ni wakulima, wale ambao ni wafanyabiashara wakipata mikopo mikubwa itawawezesha na wao kuinua hali yao ya maisha na kuona kwamba Serikali inajali maeneo yote, kwa upande wa wanawake na hili pia litawarahisishia waume zetu gharama ya kutegemea kuwaomba misaada au huduma za watoto, kikiongezeka kipato kwa mwanamke basi ni nafuu kwa familia nzima.

Kwa hiyo, tunaomba hilo liweze kufikiriwa kuweka nafuu kwa wanawake na mikopo yao wanayopewa na hali kadhalika wameomba asilimia inayotozwa riba pia ifikiriwe, ipunguzwe. Kwa upande wa Serikali afadhali kidogo sio kubwa lakini yale mashirika ambayo yanatoa mikopo, bado hawajakubali kupunguza riba wanazoziweka katika mikopo wanayotoa, ingawaje inatusaidia lakini bado unaumia mno kuwezesha kurudisha ule mkopo unakuwa huna raha kabisa ya kuuchukua ule mkopo ingawaje umeuchukua.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka nichangie ni kuhusu sherehe zetu za wanawake, sherehe za wanawake kwa kweli zinapofanyika kwa kujumuisha wanawake wengi tunafaidika sana kuelewa mambo mengi ambayo wanawake wa maeneo mbalimbali wanapokutana mahali pamoja tunajifunza mambo ya kutosha kuliko inavyofanyika sasa hivi. Sasa hivi kila sherehe inapofanyika basi robo tatu ya sherehe wanasema fanyeni kwenye Wilaya zenu, fanyeni kwenye mikoa yenu, jitegemeeni. Wanawake hawa wanasema wajitegemee, pesa wapate wapi! Wakaombe tena kwa waume zao, kwa kuomba mikopo au kitu gani ambacho kitawawezesha wanawake waweze kujitegemea katika sherehe hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo wanawake wanakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, utenge fungu maalum kwa ajili ya sherehe hizi za wanawake. Kwa sababu kule kwenye Wilaya zetu na hali ya kiuchumi katika Manispaa au Halmashauri zilivyo nazo ni duni kutokana kupunguzwa zile ruzuku na kufutwa basi imekuwa ukienda kwa Mkurugenzi na yeye anatamani kulia unapomweleza kwamba anahitaji pesa kwa ajili ya sherehe za wanawake, hasa hii sherehe ya Siku ya Wanawake Ulimwenguni ya tarehe 8 Machi ya kila ya mwaka, sherehe ambayo wanawake wanaipenda na wanapenda kujumuika pamoja, lakini wanashindwa kukutana kwa sababu ya kutokuwa na fedha za kukamilisha suala hilo na pia Siku ya Watoto Duniani, hii ni sherehe kubwa sana, watoto hawa ni pamoja na waume zetu ambao kwanza walikuwa watoto, halafu sasa waume zetu. Tunatakiwa tuweke kumbukumbuku, naomba nirudie kama haikueleweka.

Mheshimiwa Spika, nimesema hivi hii sherehe ya tarehe 16/6 ambayo jana imefanyika, ni sherehe ya watoto wetu na sisi wanawake si ndio tunazaa watoto sasa watoto hao nao baadaye wanakuwa waume zetu au wakwe zetu. Sasa kwa misingi hiyo lazima ithaminike sherehe hii ili iweze kuwekewa fungu maalum kwa ajili ya sherehe

zake. Kwa mfano, sherehe za jana zimefanyika tu kimkoa hapa Dodoma walizifanya viongozi tu kwa sababu ya ukosefu wa pesa, Mheshimiwa Waziri Dr. Asha Migiro walipita katika maeneo kwenye shule zile ambazo zinahusika na watoto yatima lakini walishiriki hapa Kimkoa tu sio Kitaifa, nini tatizo, tatizo ni lile lile kwamba hakuna fedha. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba hili ulifikirie na ingawa unasema kwa Sheria ndio umemaliza unatuaga lakini ukiyaacha maandishi yako vizuri basi na mwenzako atakayefuata ataendeleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Vyuo Vikuu vya hapa nchini, wanafunzi wameelezwa katika hotuba yake Waziri Mkuu kwamba wameongezeka sana watoto wa kike katika vyuo vyetu vikuu na hali kadhalika watoto wa kiume.

Sasa mimi kwa msemo huu au kwa taarifa hii nimefurahi lakini bado nilikuwa naomba vijana wetu hawa wanapata shida sana wanapokuwa kwenye mazoezi nje ya vyuo, zamani utaratibu ulikuwa mzuri kidogo ilikuwa wanapokwenda kwenye *practical* yaani mafunzo ya nje ya vyuo walimu wakuu wa vyuo hivyo utafuta nafasi kwa ajili ya wanafunzi wao kwenda kujifunza katika maeneo mbalimbali kwenye Taasisi vyombo mbalimbali vilivyopo, lakini sasa hivi imekuwa ni tatizo vyuo hivyo kinachofanya ni kutoa barua kwa mwanafunzi aende yeye mwenyewe akatafute maeneo ambayo atakwenda kupata nafasi ya zoezi kabla ya kufunguliwa tena shule.

Sasa kwa upande wa wasichana, kwa kweli wanapata matatizo sana waende ofisi hii wanaambiwa hapa nafasi zimejaa ukienda huku nafasi zimejaa wanarudi kwa wazazi. Wakirudi kwa wazazi sasa ndio mzazi uhangaike mbio mbio kama una madaraka basi nafasi itapatikana, huna madaraka unaendelea kupata tatizo katika maeneo ambayo wanatakiwa kujifunza zile fani ambazo wamezichagua. Pia zamani ilikuwa wanapewa na posho kidogo ya chakula lakini siku hizi kwenye Taasisi ambazo wakipata nafasi wanaambiwa nafasi ipo lakini hakuna chakula hakuna nauli.

Mheshimiwa Spika, sasa mzazi tena utoe chochote ili umsaidie mtoto wako, tunaomba Serikali utaratibu mliokuwa mnaufanya mwanzo urejeshwe ili kuwapa raha watoto hawa katika mafunzo. Kwa sababu inapokaribia tu kipindi cha mafunzo nje ya vyuo wanakuwa hawana raha kwa sababu hawajui kwamba watapata nafasi na kama wakienda huko watakula nini na watakwenda na usafiri gani.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala dogo tu kuhusu huduma zetu za treni, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi nilimshauri kipindi fulani katika swali langu na akatekeleza mambo mengi tu ya kuweka gari ndogo ndogo za kuchukua mizigo pale Dar es Salaam ili tatizo la kupishana na watu wanaoswali kwenye treni sasa hakuna, lakini limezuka tena suala lingine limerudi la watu kukaa kwenye maeneo ya vyumba utakuta wamekaa mle hakuna raha unapisha tu watu unawaruka miguu mara uwakanyage, inafikia wakati na wao wanakasirika ingawa hawana vyumba.
Sasa hili nalo tunaomba wale watendaji wadogo wafuataliwe, kwa sababu Waziri akishatoa maagizo, wanatekeleza kwa muda mfupi tu, kwa mfano hapa kwetu Dodoma hakuna hata gari lakini ulinzi ni mzuri sana hakuna wizi sasa hivi. Inabidi mtu ukiteremka kwenye treni uanze kubeba mzigo wako kichwani hakuna vile vigari, naomba

na lile aliloliahidi kwamba anaweza akaweka vigari vidogo na hapa aweke kama alivyoweka Dar es Salaam. Lakini mimi nampongeza sana kwa kazi nzuri anazozifanya pamoja na Naibu Waziri wake na watendaji kwa hiyo, naomba wafuatiliwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya waziri Mkuu, mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kutoa salaam za rambirambi kwa aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa urais kupitia Chama cha Mapinduzi, nina mhakikishia kwamba na nimehakikishiwa na wapiga kura wa Mbinga kwamba atapata kura zote.

Vile vile naomba nichukue nafasi hii kumpongeza mgombea mweza wake Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa na kupitishwa na Chama cha Mapinduzi. Sambamba na hilo napenda nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza mgombea wa urais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi na napenda niwahakikishie kabisa kwamba ushindi ni wa wazi sio suala la kunukia tu. *(Makofi)*

Baada ya hapo napenda nichukue nafasi hii nimpongeze mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wa Nchi katika Ofisi yake, bila kuwasahau Watendaji Wakuu wa Ofisi ya Rais wakiongozwa na Katibu Mkuu wao Mama Rose Lugembe, hongera sana kwa kazi nzuri sana. Mheshimiwa Spika, haijawahi kutokea taarifa ya miaka kumi ikasomwa kwa saa mbili tu na ikatoa mambo yote ambayo yamefanyika na watu wote wakafurahi, hongera sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Kabla sijaanza kuchangia kwa kweli katika mazingira ya kawaida nisingepaswa kuchangia, ilitakiwa nisimame hapa na kuunga mkono. Kwa hiyo, naunga mkono asilimia mia kwa mia, lakini sambamba na hilo na kwa lengo la kuboresha tu naomba nianze kwanza kushukuru sana kwa kile ambacho Serikali imefanya kwa kipindi cha miaka mitano ambayo mimi nimekuwa Mbunge katika Jimbo lango la Mbinga Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nilipoanza kuwa Mbunge hatukuwa na simu, sasa hivi tumeshapata simu za *Mobitel, Celtel* pamoja na *Vodacom.* Hii ni hatua kubwa, mawasiliano sasa yamefungua kabisa mlango wa watu wa Mbinga ambao wanakaa pembezoni mwa nchi na maeneo mengine duniani.

Vile vile napenda niseme hapa wazi kabisa kwamba miaka mitano iliyopita safari ya kutoka Songea hadi Mbinga ilikuwa inachukua saa tano, sasa inachukua saa moja na nusu, kwa hiyo, hili sio jambo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na shule za wananchi zisizozidi kumi, sasa hivi kila Kata imeanza kujenga sekondari zake kuna baadhi ya kata zimejenga sekondari mbili na zote zimeshaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, ari imekuwa kubwa sana katika kupanua suala la elimu, sio hilo tu, Mbinga imekuwa ni moja kati ya Wilaya ambazo zimefanya vizuri sana katika ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu, kwa kupitia mpango wa MMES, nayo ni moja ya mambo Serikali ya awamu ya tatu imeyafanya na kuyatekeleza kwa umakini na uadilifu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nianze kwanza na suala la kuhamia Makao Makuu Dodoma. Kama wenzangu walivyosema kimsingi kasi ya kuhamia Makao Makuu hairidhishi. Mimi nilitegemea Mheshimiwa Waziri angeaga kutoka Dar es Salaam na timu yake yote ya Mawaziri lakini sasa itabidi akaagie Dar es Salaam, nadhani hiyo ningeomba kabisa ikiwezekana utaratibu ubadilishwe ili tujue angalau nusu ya Mawaziri wahamie hapa kabla ya Bunge hili kuvunjwa na nashauri ili kuweka changamoto basi Wizara ya Fedha ianze, ukifanya hivyo mimi naamini hakuna Wizara itakayobakia Dar es Salaam hata Mwanasheria Mkuu wa Serikali atahamia Dar es Salaam.

**WABUNGE FULANI:** Dodoma.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Atahamia Dodoma, *I am sorry,* lakini vile vile nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Spika, kwa jinsi alivyoamua hasa kuupanua mji huu wa Makao Makuu. Ninamwomba achukue fomu arudie tena ili jengo hili ndio awe wa kwanza kuwa Spika katika jengo na Waheshimiwa Wabunge wote nawaombea warudi ili waweze kufaidi matunda ya kazi ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala hili la ujenzi wa Makao Makuu kweli Serikali imechukua hatua, zinajengwa sasa hivi nyumba mia tatu katika eneo moja. Mimi binafsi nimesikitishwa sio na ule ujenzi lakini na mpangilio wake sasa yale majengo kwa jinsi yalivyojenga kwa vyovyote vile yanaharibu mandhari ya mji huu. Huu mji hatujengi kama makambi ya kuhama tu ya wakimbizi, lazima mji huu tuujenge kama mji hasa wa Makao Makuu na mimi ningeshauri tusijenge jenge nyumba za ovyo ovyo namna hii, tujenge nyumba za ghorofa. Sasa jengo la Bunge litakuwa mfano halafu majengo mengine ovyo ovyo basi kwa kweli hata ile mandhari ya Chimwaga imeshaanza kuharibika kwa sababu ya kuyaweka majengo mahali kama pale. Kwa hiyo, mimi nashauri siku zijazo, jamani pawe na mpangilio unaoeleweka.

**WABUNGE FULANI:** Siku za mbele.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Siku za mbele, baada ya kusema hayo naomba sasa nizungumzie hoja ambayo kwa kweli nimetumwa niiseme hapa, kwanza suala la fedha za *STABEX,* fedha za *STABEX* zilikuwa na lengo la kuboresha mawasiliano na miundombinu katika maeneo ambayo yanalima kahawa kwa wingi. Lakini kwa bahati mbaya fedha hizi hazijaenda huko ambako kulitakiwa. Zimechukuliwa na *TANROADS* na *TANROADS* hawana barabara zinazoelekea kwenye maeneo yanayolima kahawa, kwa hiyo, mimi ningeshauri tusiwadanganye watu.

Mimi sipingi fedha hizi zitumike katika barabara hapa nchini, basi tuseme tunaboresha barabara lakini tusiwape matumaini ya wananchi wanaolima kahawa kwamba hizi fedha zitaboresha miundombinu katika maeneo yao. Hii haijawahi kutokea na haipo Mbinga, kwa mfano eneo la Rundu au Mbaha hawalimi kahawa katika Mkoa wa Ruvuma kule wanavua samaki, sasa badala ya kuwapelekea nyavu, sisi tunasema kwamba hela hizi zikatumike huku, mimi sielewi sijui watatuelewa namna gani.

Kwa hiyo, mimi ningeomba ni vizuri suala hili likaangaliwa upya, hizi fedha ziende hasa kwenye maeneo ambayo yanalima kahawa. Naiomba sana Serikali ilitizame upya pamoja na kwamba kuna masharti ya kutoka kwa hao wanotupa fedha lakini ni vizuri na sisi tukawa na kauli inayoeleweka ili kama ni fedha kwa ajili ya kuboresha kahawa basi iende kule ambako wanalima kahawa.

Mheshimiwa Spika, pili, leo Serikali yetu imefanya mambo makubwa sana na dunia imefanya mambo makubwa sana tumefutiwa madeni ambalo ni jambo lakupongezwa sana, vile vile Serikali yetu imeweza kuondoa kero kwa kuwajeresha kwenye *payroll* wastaafu waliochukua fedha zao kwa mkupuo, hilo halina budi kupongezwa. Lakini kuna tatizo kwa wakulima, wakulima walikopa fedha kupitia kwenye vyama vyao, wakawa na madeni makubwa sana na vyama vikafutwa, vingine vikashindwa kujiendesha. Kwa kweli halikuwa kosa lao, lilikuwa ni kosa tu la sera iliyokuwepo wakati ule.

Sasa mimi naomba kwamba Serikali sasa ifute madeni yote yanayotokana na vyama vya ushirika, ifute ili tuanze upya kwa sababu hatuwezi tukafufua ushirika katika hali kama hii na ukiangalia sana madeni mengi yalikopwa kutokana na benki iliyokuwa ya *NBC* ambayo ni marehemu. Sasa marehemu atadai vipi?

Mimi nadhani tufute hivi vitabu ili Serikali ichukue jukumu la kuyafutilia mbali haya madeni na kuwawezesha hawa wakulima waanzishe vyama vyao vya ushirika vyenye ari mpya na kasi mpya. Kwa hiyo, hili ni ombi langu, lakini la pili, naomba mali ile iliyokuwa ya *MBICU,* Chama cha Ushirika cha Mbinga ambacho kilifilisiwa, wananchi, wakulima wameomba Serikali iwarejeshee mali yao.

Mheshimiwa Spika, ikizingatiwa kwamba wao wenyewe hawakutaka chama chao kifilisiwe, walitaka walipe lile deni ambalo wakati ule halikuwa kubwa sana lakini sasa wameomba sana kwamba Serikali iangalie madaam wameunda chama chao kipya cha *MBIFACU,* basi chama hiki kwa kuwa kimeshajiandaa upya, kikabidhiwe mali hiyo hasa ikizingatiwa kwamba mali ile ilikuwa na thamani kubwa na nyingi ipo katika hali ya kuharibika na nyingi inapotea bila kumbukumbu, sasa si vizuri tukawakatisha watu tamaa ambao wamefanya kazi kubwa sana ya kujenga maisha yao, kujenga uchumi wao, kwa sababu tu kiongozi mmoja au wawili alisababisha hali ya chombo chao cha ushirika kuanguka au kufilisiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho nasema hivi, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa *Sir* George Kahama, watu wenye dhamana ya ushirika wametangaza kutogombea tena, mimi

sijafurahishwa na nitafurahishwa tu kama maombi yetu haya ya kuwafutia madeni wakulima yatatizimizwa kabla hawajaacha ofisi.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo itabidi nijenge hoja wasitoke mpaka watakavyofanya kazi hiyo. Baada ya hapo naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapa tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi, Ofisi ya Waziri Mkuu imeshajenga utaratibu wa kualika viongozi Wakuu wa Mikoa kuja kuhudhuria mjadala wa ofisi yake na wa TAMISEMI na kwa mwaka huu wamefanya hivyo. Kwa hiyo, ni vizuri nitambue kuwepo kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa katika *gallary* ya Spika, kwa sababu hawa ni viongozi wenzetu, pamoja na Ma-*RAS* wao, lakini watu waliostarabika wanapotambulishwa na Spika, huwa wanasimama ahsanteni. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa Wakuu wa Mikoa pamoja na Ma-RAS waliotambulishwa walisimama)*

**SPIKA:** Waheshimiwa wabunge, baada ya hapo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.54 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii mchana huu ya kuzungumzia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nianze na mimi kwa kutoa rambirambi kwa wapiga kura na jamii yote ya aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho yake. *Amin.*

Vile vile napenda nichukue nafasi hii mimi kama mwanachama wa Chama cha Mapinduzi kutoa pongezi za kina na za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuchukua bendera ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi wa Urais mwaka huu. Salaam za kina vile vile kwa Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi kugombea Urais Zanzibar na kwa Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa nafasi ya Makamu wa Rais ya Jamhuri ya Muungano, Mgombea Mwenza wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kabisa, kwa hotuba nzuri na nimpe pole kwa sababu alionyesha jinsi alivyo na *energy,* aliongea kwa saa mbili hapa na sauti yake ilibakia ile ile, nampongeza sana. Lakini nimpongeze kwa jinsi hotuba yake ilivyokuwa *comprehensive* kiasi kwamba naweza nikasema inaweza kuwa ni *reference* ya haraka kwa kweli kwa kipindi cha miaka

10. Unaweza tu kupitia kwenye ile hotuba ukaenda uka-*expand* ukafahamu zaidi kuhusu eneo ambalo alikuwa analizungumza. Lakini niseme tu kwa kifupi kwamba imekuwa ni kielelezo cha kazi kubwa iliyofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Tatu ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

Lakini vile vile naomba nimpongeze yeye mwenyewe binafsi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa jinsi ambavyo amelitumikia Taifa hili katika nafasi mbalimbali na hii nafasi yake ya Uwaziri Mkuu kwa miaka 10 na natoa pongezi hasa kwa sababu ametangaza kwamba hatagombea tena, kwa maana hiyo uwezekano wa yeye tena kwa mujibu wa Katiba yetu kuwa Waziri Mkuu ni mdogo au haupo kabisa kwa sababu Katiba inataka Mbunge wa Jimbo ndiyo awekwe na agombee nafasi au ateuliwe na Rais kwa ajili ya kupata ridhaa ya Bunge kuwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye hatafanya hivyo, kwa hiyo, napenda nitambue mchango wake katika miaka 10 na niseme kupitia tendo lake hilo la kung'atuka kwamba hakika katika kipindi chake chote tunajua amevuna hazina kubwa ya uzoefu, lakini na ufahamu ambao bado Taifa hili na kwa kweli kwa umri wake bado atakuwa ni wa msaada mkubwa. Sasa tuna taratibu katika nchi hii ya kutumia viongozi hata wale waliostaafu. Lakini kuna haja nadhani ya kurasimisha sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka katika mabadiliko ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaliyoletwa na Serikali kulikuwa na mapendekezo ambayo baadaye yaliondolewa na mimi nilikuwa napenda niseme kwa kweli nilikuwa mmoja kati ya watu ambao nilidhani kuwa na Baraza la Ushauri la Rais ndani ya Katiba haikuwa kitu kizuri. Lakini si kwamba kuwa na Baraza la Ushauri ilikuwa ni kitu kibaya, hapana. Isipokuwa kuwemo hilo Baraza ndani ya Katiba ndiyo ambalo nadhani halikuwa jambo zuri. Kuna *implications* zake ambazo nisingependa niingie ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme leo kwenye gazeti la Mwananchi, wametoa sura sita za Mawaziri Wakuu, sasa unaweza ukaona tu kwa kuanzia hapo hazina ambayo ipo. Huu ni uzoefu ambao uko pale. Ni uongozi uliotukuka kwa sababu wote wamepata nafasi ya kutoa uongozi na mpaka wakaacha madaraka hakuna aliyepatwa na kasheshe kama lile la Makamu wa Rais, Jacob Zhuma huko *South Africa.*

Kwa hiyo, nasema hii ni akiba kubwa na kwa kweli usipoitumia utakuwa unajinyima wewe mwenyewe nafasi ya kutumia akiba hiyo na ndiyo maana nilikuwa nadhani katika nafasi yangu hii leo ya kutoa mchango kwenye Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu niseme kwa kweli ni muda tena muafaka kurejea katika wazo hilo la kuunda Baraza la Ushauri ambalo si lazima liitwe jina hili ambalo nalitumia sasa hivi. Lakini kikubwa mimi nilikuwa nadhani linatakiwa ku-*preside* au kuwa *under arm* ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa asili yake Bunge kwa mujibu wa Katiba linafanya kazi ya kuishauri Serikali na hawa watakuwa ni watu *eminent* ambao wamekusanya uzoefu na walikuwa viongozi ambao kwa kila namna wanaitakia mema nchi hii na wangependa kupata nafasi ya kuendelea kutoa mchango wao mahali rasmi

kwa wao kufanya hivyo nadhani ingekuwa ni chini ya mwamvuli mmoja ambao mimi kwa hivi sasa natoa mapendekezo ya awali tu kwamba hili wazo lirejee, Serikali itakayokuja nadhani italiwekea maanani na kuangalia uwezekano wa kuwa na Baraza la hawa Wastaafu wa aina hii kuanzia Marais, Makamu wa Rais waliopo, Mawaziri Wakuu na kuna Wakuu wa Mikoa wengine waliofanya kazi za kutukuka ambao wamekwisha acha kazi na wengine *probably* wataondoka hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wabunge ambao walikuwa na nafasi nzuri sana, Mawaziri, kunaweza baadaye kukawa na namna ya kuwapata hawa watu. Lakini walau kwa kuanzia hawa watu wa juu kabisa, Rais, Makamu, Waziri Mkuu wana nafasi katika Baraza la namna hiyo. Hilo ni pendekezo ambalo ningenda niishie hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Tabora na Tabora tumbaku ni siasa na siasa ni tumbaku. Leo hii asubuhi wakati swali namba 87 likijibiwa na ndugu yangu, alikuwa ni yule kijana wa Kigogo nadhani. Yule kijana mdogo mdogo wa Kigogo sijui yuko wapi sasa hivi hapa, ametoka, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, amepotea njia nafikiri hajafika Bungeni hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu wakati anajibu hili swali lilifuatia swali la nyongeza la Mheshimiwa Said Nkumba. Mheshimiwa Said Nkumba, alimweleza au aliuliza kwamba ni kweli kwamba leseni walizopewa wanunuzi wa tumbaku ni za kununua tumbaku tu peke yake na kwamba hawana *authority* ya kiwango hicho cha leseni katika masuala ya pembejeo na jibu lilikuja hivyo hivyo kwamba ni kweli na kwamba haya mambo ya pembejeo ni ombi lilitoka kwa Serikali kwa sababu hawa ndiyo walioonekana wako karibu na wakulima na kwa *interest* yao vile vile kupata mazao mengi wakati pembejeo zinafika.

Sasa muda haukutosha, tungependa tuulize maswali mengine ya nyongeza. Lakini napenda nitumie nafasi hii kusema tu kitu kimoja na naamini watakaofuata naamini Mheshimiwa Ally Karavina, atalipanua tena zaidi. Sasa hivi tunapata matatizo baada ya mafanikio kwa kweli katika nyanja hii ni kuanzia kwenye sheria yenyewe ya Tumbaku ya mwaka 2001 ambayo imeleta sura na mahusiano mazuri sana kwenye tumbaku na kwa kweli *improvements* zimekuwa ni nzuri sana na kipato kinaonyesha hayo.

Lakini matatizo bado yapo, vile vile kubwa ambalo limeendelea kuwa tatizo mpaka sasa ni jinsi gani hawa wakulima maskini watajitegemea au kujikwamua kutoka kwenye ile *contract farming.* Unapokuwa na lile kampuni ndiyo linalotoa pembejeo wakati huo huo ndiyo lina leseni ya kununua tumbaku yako, uko katika mkataba na kwa kweli mikataba hiyo ipo. Sasa wakulima wetu wameanza kujikomboa, wanataka kuondokana na hii mikataba. Kuna *efforts* ambazo zimefanyika za wao ku-*access* mikopo ya benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia nafasi hii ndani ya nyumba yako hii Tukufu, napenda nimwombe tena kijana wa Kigogo, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje na Wizara yake kwa kweli Mheshimiwa George Kahama na Wizara nzima walitilie mkazo hili suala la kuwawezesha hawa wakulima wetu ku-*access* mikopo. Nisingependa

nizungumze sana na kwa kina kuhusu hili. Lakini nilitaka niseme kuna vikwazo ambavyo kuna kila sababu ambayo inaweza kufanya mtu ambaye unatafakari uamini kwamba hivi vikwazo vinaletwa na mmoja kati ya wadau walioko kwenye suala hili la pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana ni kama anaona ananyang'anywa tonge lake. Sasa sisi tunadhani ni ukombozi mkubwa wakati wakulima wetu wana *access* mabenki na tunaomba kwa kweli ni bora wakasaidiwa na hapa nataka nisisitize. Nimekwishasema hapa ndani siku zote, Serikali inaweka mazingira mazuri ya biashara, inafanya hivyo. Inajiondoa kwenye biashara, lakini nataka niseme tena isijitoe moja kwa moja na hasa inapofika kwenye kuwasaidia wakulima, wakulima wanahitaji kila aina ya msaada, ikiwa ni pamoja na msaada wa ushauri na pengine inabidi kwa kweli kuwashauri kwa nguvu, naomba mniwie radhi kusema hivyo, lakini kuna mahali chaguzi zinakuwa zile ambazo zinaleta wasi wasi. Kwa hiyo, Serikali kwa sababu unataka uamini kabisa, inawatakia mema wakulima wake lazima ione hili na itoe ushauri na itoe ushauri na kwa kweli itumie nafasi yake kama Serikali kutoa ushauri na ushauri ambao utakuwa wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nitoe rai hiyo kwamba Wizara hii ya Ushirika na Masoko iangalie vikwazo ambavyo vimeanza kuwasibu hawa ndugu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliachie hapo hilo la tumbaku, niendelee kwenye suala la barabara. Kwanza niseme, hivi sasa kuna *Mtwara Corridor* na hii *Central Corridor* ambayo iko kwenye *process* ya *conception.* Nimekuwa nikiuliza na mpaka sasa kwa kweli nataka niseme mbele yako sijapata *definition* ya *Central Corridor. Central Corridor* inavyokuwa *defined* haijaridhisha maana nzima ambayo unataka kuipata unapoongelea *Central Corridor.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa sababu muda unataka kunitupa mkono, unapokuwa unatengeneza *Central Corridor of course* kuna *SDI's* nyingi ndani ya *corridor and one of them* ni barabara. Unapotengeneza barabara lazima utengeneze barabara kwa *economic sense.*

Kuna barabara hapa ya kutoka Itigi kupitia Kigwa kwenda Tabora, Urambo kuendelea mpaka Kigoma ipo pale muda mrefu na kila mtu anajua ndiyo barabara fupi kabisa ya kukufikisha wewe *DRC* ambako kuna mzigo wa kutosha kabisa kubadilisha hali ya uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Lakini nashangaa hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anajibu hapa hoja yake alikuwa anazungumza anazunguka zunguka tu anaikwepa hii barabara. Unashangaa huyu ni Waziri wa Fedha ungefikiria kwamba anafikiria sehemu ambazo atawekeza ili nchi ipate fedha. Hapo hiyo barabara alikuwa anazunguka zunguka tu mpaka tukaanza sisi tena kujiuliza maswali yale yale kwamba hivi Mkoa wa Tabora na haya maeneo mpaka Kigoma tuna matatizo au kuna makosa tulifanya katika nchi hii au basi hawa wenzetu hawalioni hili tunaloliona sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu manufaa siyo ya Tabora peke yake, manufaa yatakuwa ni ya nchi. Tutapata manufaa makubwa, sasa nashangaa kuna Wizara ya *Planning* pale Mheshimiwa Basil Mramba wakati anajibu hoja yake pale anaanza kusema kwamba kulikuwa na Waheshimiwa Wabunge wa sehemu fulani walikuja tukazungumza na wewe unaweza ukaja tukazungumza na Mheshimiwa pale unaweza ukaja tukazungumza anawaambia hapa watu. *What kind of planning is that?* Wanatoa pesa wapi, huyu Mheshimiwa Basil Mramba anapowakaribisha hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ajabu kabisa, wakati una Wizara ya *Planning* bado unaweza ukasimama kwenye *podium* hapa ndani ya Bunge mahali ambapo tunapitisha pesa zote na tunapitisha na sheria ya ku- *appropiate* hizo *funds* bado *you can spare some money, I don't know where,* una-*invite* watu waje wa-*negotiate for that money out of plan, what is this? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisema kwa uchungu kwa sababu sisi ndiyo tunajikuta tunawekwa nje, wakati tunaaamini kabisa sisi ndiyo *geographically* tuko *located* mahali ambapo kama tungepitiwa na hii barabara uchumi ungekuwa mkubwa kwa nchi hii si tu kwa eneo lenyewe peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hii ni *anomaly* kubwa sana, inatakiwa kusahihishwa kabisa. Sasa wamefanya kosa lingine wamekwenda kusaini *contract* ya kujenga reli kutoka Isaka kwenda Kigali. Unaenda kumsaidia *competitor* wako ku-*compete* na wewe umepata kuona wapi hii. Wewe mtu wa Yanga unakwenda kuwasaidia watu wa Simba kufunga goli Yanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is a paradox to me, what kind of thinking* ambayo iko pale kwenye Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Unakwenda kabisa unajua kabisa hapa ukiwa na *direct access* ya Kongo, una mzigo wa Kongo ukamwacha huyu mtu kwa sababu sasa huyu atakuwa anachukua pesa pale, sisi tutapata makapi kama mizigo ya Kongo itapitia Kigali halafu ije huku Tanzania, jamani. Sasa hivi watu hawa wa Burundi na Rwanda *they can afford actually* kuvuta matishari yakiwa na mizigo yao kushusha mpaka chini kule. *We can do that,* hapa *distance* ni fupi sana kutoka Kigoma kukatiza upande wa pili pale kilometa sijui 45 pale. Unakwenda mpaka mmoja sasa unataka ku-*subject* bidhaa ile kwenye mipaka mingapi, watu wangapi sasa watakuwa wamefungua midomo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi hili na kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu nasikitika sana kwamba bado tunaweza kuwa na *this kind of planning.* Niseme haraka haraka nataka niligusie hili suala la Bunge. Bunge ni moja kati ya mihimili mitatu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunasema *every now and then,* kwa nini Bunge walau kwa kuanzia haliwezi kusimama ndani ya Bunge lenyewe likaomba pesa zake, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tena Mheshimiwa Waziri Mkuu ameomba pesa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, analiombea pesa Bunge na mimi nilikuwa najiuliza kwa nini iwe hivyo? Mheshimiwa Frederick Sumaye, anapenda kazi yake amefanya vizuri sana.

Ninasema tu, kwa kweli ningependa nimkwamishe kwenye hili. Lakini ni kwa sababu ya kazi nzuri napenda nisimkwamishe, lakini nataka niseme, naunga mkono kama nilivyosema, sitamkwamisha. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri na Waziri Mkuu wanaitwa kwa vyeo vyao maana wengine wameitwa vijana wa Kigogo, unaita Waziri Mkuu Frederick Sumaye. Ningependa Mawaziri na Waziri Mkuu waitwe kwa vyeo vyao, Kanuni inasema hivyo. *(Makofi)*

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani na mimi kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu.

Lakini awali ya yote na mimi niseme kwamba tarehe 2 Juni, 2005 tulimpoteza mwenzetu hapa, Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Abu Kiwanga. Kwa hiyo, naomba kabisa nitoe salaam za rambirambi kwa wapiga kura wetu wale walioko kule Kilombero na kwamba hiyo ni kazi ya Mwenyezi Mungu waione hivyo. Wasiwe na wasi wasi kwa sababu ndiyo hitma ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nisipoteze wakati mwingi, niingie moja kwa moja. Nataka kuzungumzia mambo matatu leo. La kwanza ni kuondoa umaskini na ajira za vijana, la pili, nitazungumzia ubinafsishaji ulivyokuwa muda uliopita, muda tulio nao na tunaenda wapi na la tatu, na mimi lazima nigusie miundombinu hususan Kanda ya Maendeleo ya Kati mojawapo ya Kanda ambazo nimekuwa nazizungumzia kwa muda mrefu toka mwaka 2001. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondoa umaskini, mimi mpaka sasa bado siamini kwamba kwa mpangilio ulivyo katika Serikali ya Tanzania na mfumo wa Tanzania wa namna unavyopanga mambo yake kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi kuja kwenye utekelezaji ndani ya Serikali tunaweza kusubiri mpaka huo mwaka 2015, 2025 kuondoa umaskini naamini kama tutaamua kuwa *bold enough* tunaweza tukauondoa umaskini mapem zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, ulipokuwa unaanza mpango wa MMES kila mtu kwenye nchi alikuwa na wasi wasi, mpango MMEM, kila mtu alikuwa na wasiwasi. Tunawapelekea fedha wale walimu kule chini vijijini maskini ya Mungu hawajazoea kushika mamilioni, wamezoea kushika hela ndogo ndogo tu na kila mtu alikuwa ana mawazo kwamba sasa hela zile zitaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeona mafanikio ya mradi wa MMEM yamekuwaje. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kupeleka hizi fedha chini kwa wananchi na bado

zikapewa vipaumbele ambavyo wananchi wenyewe ndiyo wanafikiria ni mpango mzuri wa kuondoa umaskini wao. Sasa mimi nina wazo, kwa sababu tumepeleka fedha za MMEM, zimefanya kazi na sasa tunapeleka za MMES zinafanya kazi na tumekuwa na mradi wa *TASAF* umefanya kazi vizuri sana na ukiangalia miradi yote hii mitatu imekuwa inatumia mfumo wa kuwa-*consult* wananchi waseme wanataka mradi gani kwenye vijiji vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini? Kwa sababu tuna Serikali kamili za vijiji. Sasa tusianze kuweka bajeti za Serikali za vijiji. Kwa nini tumeanzisha Sheria na Serikali. Serikali za vijiji kisheria kabisa halafu mpaka leo hazina bajeti hata kidogo. Tuanze na ndiyo tutaweza kupima sawa sawa. Fedha nyingi zile ambazo tunazikwamisha juu basi tuzipeleke kule chini sisi tufanye kazi ya kusimamia kuondoa ule umaskini kwenye ngazi ya kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kabisa hazitaliwa, isipokuwa zitafanya kazi ya kuondoa umaskini kwa haraka zaidi kuliko tunavyofanya sasa. Kwa hiyo, hili wazo mimi nafikiri hebu tuanze kulifanyia kazi na ndiyo maana nimesema lazima tuwe *bold enough,* tusiwe na woga kama tumeweza kufanya haya tuliyoyafanya basi kwa nini tuwe na woga wa kufanya hivyo.

La pili, kule kwenye vijiji, kuna vyama vya ushirika vya msingi na kama tunavyoelewa wote vyama vya ushirika ndiyo fimbo ya mnyonge. Mimi nachelea kusema kwamba vyama vya msingi mpaka sasa hatujavisimamia sawa sawa kwenye ngazi ya kijiji kwa sababu kwa kweli kwenye ngazi ya vijiji pamoja na kwamba ndiyo uzalishaji mkubwa wa kilimo uko kule. Lakini tumewaacha wanajiendea wenyewe tu, hatujawasaidia na mikopo. Hatujawasaidia na chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa mambo ambayo tumeanza kufanya kule kwetu. Nina vyama vyangu vya msingi nane na mimi nilivishawishi sana na kuviombea na kuvishinikisha sana na kuvisaidia kwa kweli kupata mkopo wa *CRDB.* Nimepata takriban milioni 600 kwa vyama hivyo.

Mimi nitakwambia kilichotoa, kwa mara ya kwanza hawa wakulima wa tumbaku hawakuweza kuuza ile mbolea waliyokuwa wanachukua kwa bei ghali na kuiuza kwa bei ndogo kwa sababu ya ukapa ule unaokuweko kati ya kilimo na kuuza na kupata fedha zao. *(Makofi)*

La pili ni kwamba hawakuweza kuuza chakula chao walicholima. Kwa sababu walikuwa na *bridging finance* kati ya kuuza na kati ya kupata na la tatu, wameweza sasa siyo kung'ang'ania tu mkopo wa mbolea, kitu kimoja tu zao la biashara yaani tumbaku. Ile fedha sasa wanaweza kununua mbolea yoyote ile ya chakula na vitu vingine vyovyote. Lakini pia ile fedha inasaidia kama njaa ikitokea ghafla kwa ngazi ushirika wa kijiji wanachama wake inaweza kuwapatia chakula bila wasi wasi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tu hapa mwenzangu aliyepita alichokisema, baada ya wenzetu wanunuzi na hapa ndiyo nataka nilizungumzie soko huria na mimi

nilisema muda uliopita, mpaka sasa hatuna soko huria kwenye sehemu nyingi, afadhali sasa kuliko ilivyokuwa mwaka 2000 wakati tulikuwa hatuna hizi *controlling organizations.* Lakini kule kwenye tumbaku bado tunalo soko holela. Kwa sababu huwezi kuwa na soko huria mpaka umekopa kwingine angalau ukauza kwingine na umaskini wako. Ndiyo hapo mkulima atakuwa na uhuru wa kuuza na ndiyo hapo mkulima atakuwa na uhuria wa kuuza. Lakini kwa *contract farming* inayofanyika sasa hivi, ukishaingia tu ile *contract* tumbaku yote unayolima wewe ni manamba, siyo ya kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile tumbaku yote siyo ya kwako na kuna kiwango ambapo yule mnunuzi anaweza akafanya lolote. Tunashukuru Serikali na tunashukuru sana Bunge hili kwa sheria ile waliyoisimamia ikapitishwa ya Tumbaku ama sivyo hali ingekuwa mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wenzetu hawa sasa pamoja na kwamba wana leseni ya kununua tumbaku peke yake, lakini kwa sababu waliruhusiwa kuuza pembejeo, hiyo pembejeo sasa imekuwa bei ghali sana na inakuwa bei ghali sana kwa sababu wameigeuza kuwa biashara. Siyo kwamba wanafanya biashara tu ya kununua tumbaku. Lakini wanafanya pia biashara ya pembejeo. Wana asilimia 35 ya faida kwenye kilo ya pembejeo. Kwa hiyo, mfuko wa tumbaku leo hii unauzwa zaidi ya shilingi 25,000/=. Huyu mkulima atapata faida gani? Tumeleta ukombozi kidogo tunasema basi kama ni hivyo basi wakope kwingine ili wawe na uhuru wa kuuza. Tunawapa mikopo ya *CRDB* hawa wenzetu mimi sitaki hata kuzunguka sana. Hawa wenzetu hawa wameanza kuwaletea chokochoko wanasema hawa mnaowapa mikopo mara mbili watu wetu hawa. Nani ana watu wake zaidi ya nchi hii kuwa na watu wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyosema kuna mikopo mingine imesimamishwa bila sababu nzuri ya hao mabwana pamoja na kwamba mpaka sasa kwa magulio waliouza, tayari wanadai makampuni. Tayari wana uwezo na kulipa huo mkopo wa *CRDB* na bado wanabaki na pato kubwa zaidi kuliko mikopo yote miwili. Hata *logic* ya kuchukua mkopo mimi sielewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri mkopo maana yake uwezo wako wa kulipa kama una uwezo wa kulipa. Ndiyo sharti kubwa, lakini kama kuna masharti mengine ya kuwakandamiza wakulima wawe daima duni, wabaki maskini ndani ya soko holela, basi hata siku moja hawatafaidi soko huria. Mimi nitaomba Ofisi ya Waziri Mkuu na nalisema hili ni jambo ambalo nataka litatuliwe kwa nini mikopo hiyo ya *CRDB* imezuiwa kinyemela?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niende kwenye *point* yangu ya pili kwa sababu muda najua ni mchache, ubinafsishaji. Nafikiri tumemaliza kubinafsisha kila kitu sasa hivi, viwanda vyote vimekwisha. Sasa tumeanza kubinafsisha miundombinu hii ya kijamii hususan reli, sijui tutakwenda *TANESCO,* sijui tutakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekti, nataka nitoe tahadhari, ubinafsishaji wa miundombinu hii ya jamii ni kitu cha hatari sana. Hakuna *formula* mpaka sasa duniani ya ubinafsishaji

wa miundombinu. Ndiyo maana tumejaribu pale wanasema watakodisha. Sielewi ukisema unakodisha hususan kwa mfano, Shirika la Reli. Reli ilijengwa mwaka 1907 hadi 1909. Imemaliza miaka karibu 100. Huna cha kukodisha ni reli inayotaka kubadilishwa yote ili iweze kumudu mzigo wa sasa. Unakodisha nini? *(Makofi)*

Shirika lile halina mabehewa, halina nini. Kwanza mabehewa mengine ya abiria ndiyo yale yalikufa pamoja na wale watu kwenye ajali ile ya hapa Dodoma, unakodisha nini? Kwa sababu ukisema unakodisha, hutopata hicho unachokitaka kwamba huduma ita-*improve,* ita-*improve* na nini? *Rolling stock* hakuna, lakini unatakiwa iwekezwe reli. Kwa hiyo, utakodishaje, lazima aidha, ubinafsishe au Serikali yenyewe iwekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwekeza kwenye reli kwa mtu binafsi ambaye malipo yake yaani *return on investiment* inakuja baada ya miaka 100, si rahisi kwa mfanyakazi wa binafsi, si rahisi kwa mfanya biashara. Tunadanganyana, reli zote ninazozijua mimi duniani sasa zilizobinafsishwa na nyingine zimekwishaanguka hazizidi masafa ya kilometa 150. Tunazungumzia reli yenye zaidi ya kilomita 1000! *(Makofi)*

Tunazungumzia reli inayopita sehemu nyingine ambayo hakuna *alternative* ya usafirishaji ni reli tu. Sasa mimi nataka kutahadharisha na nataka kutahadharisha kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu hii kwamba tusije tukajikuta wananchi wetu wanaathirika zaidi ya hivi ilivyo sasa. Kwa sababu tunaogopa kuchukua maamuzi magumu zaidi kwamba kuna miundombinu ya wananchi ambayo lazima Serikali yenyewe iwekeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni namna gani utabinafsisha *TANESCO* wakati kwa kweli inahudumia asilimia kumi tu ya wananchi. Kwa kawaida ya uchumi, maana yake tatizo lenyewe ni suala la uchumi wa kuekeza hizi, ile *fixed investment* ya *municipal organizations* kama hizi taabu yake ni kwamba ni gharama kubwa mno na huwezi ukai-*recover* mtu binafsi kwa miaka ishirini au kidogo kidogo au huwezi ukai-*recover* kwa watu asilimia kumi kutumia, lazima iwe ina *intensive utilization* na lazima aidha, iwe ya muda mrefu. Asilimia kumi tena uivunje vipande vya *transmission, generation* na nini unategemea iweje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natahadharisha, sasa tumefikia wakati mgumu sana wa ubinafsishaji sio rahisi rahisi tu vile *PSRC* walivyokuwa wanafanya inabidi wakae chini waone namna gani hasa hiyo Serikali ya awamu inayokuja wasiingize matatani, wasiingize kwenye matatizo makubwa inabidi watu wakae chini wafikirie hili ni la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa sababu muda sina, nizungumzie miundombinu. Utakumbuka mimi nimezungumzia *corridor* hapa toka mwaka 2001 wakati ule nilikuwa naonekana kama juha hivi, lakini sasa nafikiri kila mtu kuelewa na mimi namshukuru sana Rais wa miundombinu huyu Rais wa Awamu hii kwa kuzindua rasmi mwezi uliopita Kanda ya Maendeleo ya Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wengi sana waliokuja kule kwenye ile sherehe wanatoka Afrika Kusini lakini mimi naelewa, shauri yenu Watanzania tunaweza

tukavamiwa kwa sababu kwenye kutengeneza fedha mpya ndio inatengenezwa huku kwenye *corridor* hizi. Kwenye hizi *special development initiatives* ni kutengeneza fedha mpya.

**WABUNGE FULANI:** Ni shauri yetu.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Sasa ni shauri yetu wenyewe na mimi narudia tena kwenye *Central Corridor* niliwahi kusema tunacheza na mahali ambapo tuna *comparative advantage* ya biashara na kuwaruhusu watu wenye *competitive advantage* kuja ku-*erode comparative advantage* yetu. Nataka niiseme tena hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Tafsiri.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Muda wa kuitafsiri sina ningechukua muda kidogo kuitafsiri lakini nasema hivi Tanzania kwa mzigo wa Kongo ambao kutoka huko mpaka unapanda kwenye meli ni dola 120 kwa tani na una tani milioni 10,000 za dola 120 kwa tani piga hesabu trilioni 10 wewe mwenyewe unajua ni fedha gani, ndio biashara ambayo tunaikosa ambayo tuna *comperative advantage* nayo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Kwanza kabisa, niungane na wenzangu waliotangulia kutoa salaam za rambirambi zangu kwa kuondokewa na mwenzetu, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero ambaye tulipofikiri tutaondoka wote hapa na kurudi pamoja lakini Mungu ameamua akamtwaa. Naomba Mungu ailaze pema roho ya marehemu. *Amin.*

Pili, naomba niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu imegusa sehemu zote ambazo kulingana na mafanikio yaliyojitokeza katika Awamu hii ya Tatu baada ya kuijenga Awamu ya Tatu kwenye misingi ya awamu zilizotangulia, kuna mahali imetufumbua macho na kwa hakika imedhamiria kutupa nafasi kama dira kutuonyesha huko tunakoelekea ni nini tunaweza tukafanya. Nampongeza sana pamoja na Wizara nzima na ninaiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Pamoja na yote hayo, ipo nafasi nzuri ya kutoa ushauri. Katika hotuba nzima sikuona mahali ambapo limezungumzwa vizuri na kutazamwa suala la matokeo ya tatizo la UKIMWI katika Taifa letu hasa tunapojua imetangazwa UKIMWI ni janga la Taifa. Pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imesemwa kwamba wako yatima karibu milioni mbili katika Taifa letu hili na milioni mbili hii wapo pia wajane, lakini sikuona ni wapi kabisa ambapo imewekwa mipango ya kuhakikisha kwamba yatima hawa watasaidiwa kuishi. Yatima hawa wako katika vituo vya kulelea watoto *(orphanages),*

wako shule za msingi, sekondari, wako katika machimbo ya madini, wako katika mashamba makubwa ya biashara, wako mitaani wanahangaika wanakufa kwa minyoo, malaria, mafua, haionekani kama wamewekewa utaratibu kamili kwamba hawa watu ni Taifa la kesho na ndio watakaozaa kurudishia hawa wanaokwisha ili waweze kusaidiwa. Tunasema kwamba kuna dawa za kuongeza maisha, tunasema kwamba tunaendelea kuwa na *NGOs* kuendelea kusaidia katika mapambano dhidi ya UKIMWI lakini hawa wako wapi kusaidia malezi ya wimbi hili la watoto yatima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati kama huu nilizungumza katika hotuba ya bajeti kwamba ilikuwa ni vizuri kitengo cha watoto kikaondoka chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo lakini mpaka sasa ni mwaka mmoja watoto hawa wako huko wanateseka. Hatuwezi kushughulikia mambo ya michezo, tukashughulikia jeshi kubwa la vijana nchini ambao tunajua hali yao ilivyo na mzigo ambao Serikali inapaswa kuubeba kusudi kuwaendeleza vijana halafu tukazungumza na watoto wa mwaka mmoja, miezi mitano, miezi kumi na mitano.

Mimi naomba kabisa Serikali ifikirie kitu hiki kwa sababu Taifa litatokomea. Watoto hawa wanahitaji kufanyiwa kazi na iwezekane pengine litengwe fungu maalum kwa kuwasaidia watu hawa kwa njia nyingi tu. Kwa mfano, Mfuko wa Elimu kwa sababu ya wale vijana wasiojiweza wanaokwenda sekondari unapaswa kuongezwa. Watoto hawa wanahitaji kutoka katika eneo la Wizara hiyo ya Kazi na Maendeleo ya Vijana waingie chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili waweze kuwekewa uhakika wa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo ambayo nafikiri lazima tuyatazame. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake pamoja na Baraza la Mawaziri kuweza kutufikisha mahali pa kufutiwa madeni mengi kiasi ambacho tumekiona safari hii. Mimi naomba kabisa nizungumzie hii pesa ingepaswa kwenda wapi kwa wakati huu. Tunaimba kuondoa umaskini. Mimi nafikiri umaskini katika Taifa lolote ambalo ni maskini unatokana na vitu viwili vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwa sababu ya ujinga na pili ni kwa sababu ya ukosefu wa kilimo chenye uhakika hasa katika nchi ambazo hazina viwanda, Tanzania ni mojawapo. Kwa maana hiyo basi, naomba fedha hizi zielekezwe katika nafasi ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nakumbuka vizuri watoto wa darasa la saba walioshinda kwenda sekondari mwaka 2004 walikuwa ni wengi sana lakini asilimia karibu 35 tu ndio wamekwenda sekondari. Mfano ni wa Wilaya ya Ngara ambako katika watoto 2,232 waliofaulu na Wilaya ikafanikiwa kuwa ya pili Kitaifa ni watoto 929 tu ambao wamekwenda sekondari 1,303 wako kijijini wakiwa na alama za A, B na C, hawa ni *genius.* Huwezi kuondoa umaskini kama watu ni wajinga, wanaweza wakakaa mahali wakaridhika kwamba wao wamekamilika kumbe wana mapungufu ambayo hawayajui kutokana na ujinga wao. Kwa hiyo, niseme kwamba kunahitajika majengo mazuri ili Walimu wawe na mazingira mazuri, pesa iongozwe ili kuweza kuinua utaratibu tuliouweka wa MMES na vyuo vingine zaidi vya Walimu vifunguliwe ili tupate Walimu

wa kutosha. Hii itatusaidia sana katika kupunguza umaskini Mtu asije na elimu ya darasa la saba, mara nyingi hawezi kuwa mbunifu. Hana uelewa .

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kilimo. Pato la Serikali kutokana na kilimo ni 48%, ajira ya wananchi wa Tanzania 80%. Kwa hiyo, sekta rasmi inabaki na 15% ukiondoa wafanyabiashara wakubwa na wengine ambao hatukuwaweka hapa lakini tunajua kiwango cha fedha ambacho tumekitoa katika bajeti hii. Unategemea nini kwa watu hawa mamilioni walioko vijijini ambao hawana kilimo cha hakika, cha kitaalamu, kilimo cha kisasa katika utandawazi. Hawawezi kushindana katika masoko ya dunia, hawawezi kushindana katika masoko ya ndani? Ni budi kilimo cha Tanzania kiwe cha kimapinduzi kusudi kuleta matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Jumamosi nilikuwa Mpwapwa, mvua zikinyesha milimani maji yanakuja mpaka Mpwapwa mjini. Mvua zikinyesha Monduli maji yanateremka mpaka Mto wa Mbu na haya maji yote yanapotea lakini tunaimba kilimo cha kumwaligilia. Naomba Serikali ifikirie kwamba imefika wakati tusiingie kwenye kuimba na kucheza. Kuondoa umaskini sio utani, kuondoa umaskini ni lazima tukubali kwamba kuna mipango iliyo na umuhimu wa kwanza na mimi nasema umuhimu wa kwanza unaingia kwenye elimu na kilimo. Kilimo cha umwagiliaji sasa kiimarishwe kwa kupelekwa Mikoa yote na kuongezewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie *STABEX.* Fedha hii imetutoa jasho katika nyumba yako hii. Kila Mbunge anayetoka katika Mkoa unaolima kahawa amepiga kelele. Sasa wanaotoka katika Mikoa inayolima pamba nao wanadai kupewa *STABEX,* lakini inashangaza kwamba mpaka sasa maelezo yanayotoka katika nyumba hii sio maelezo ambayo yako wazi. Ngara inalima kahawa kama ilivyo Kagera, lakini ukitazama barabara zilizopewa fedha hii ni barabara ambazo zimeacha maeneo maalum yanayotoa kahawa zimekwenda katika maeneo ambayo hata Mkoa unasema hauna habari na mpango huo. Wilaya ya Ngara kwa mfano haikuhusishwa katika suala hili na nafikiri huyo mtu aliyetoka Umoja wa Ulaya hakuweza kufika Wilayani Ngara. Ngara tumejenga kiwanda, Ngara hatumwagilii dawa, kahawa ya Ngara inakwenda moja kwa moja katika soko la dunia na inaleta fedha ya kutosha.

Lakini wananchi barabara zao zimekufa kwa muda mrefu lakini hawakupewa pesa hii. Naomba ofisi ya Waziri Mkuu ilitazame suala hili, uzungumze na Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo iwezekane kabisa Wilaya ya Ngara iwekwe katika nafasi hiyo ili kusudi tupate pesa ya kutengeneza barabara, wananchi waongezewe nguvu na motisha kwa sababu ya kuzalisha kahawa zaidi.

Naomba nizungumzie ulinzi na usalama katika mipaka yetu. Wananchi wa Ngara wanaishukuru Serikali kwa kusaidia kuondoa wakimbizi mamilioni waliokuwa katika Wilaya ile na katika Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado wananchi wana tatizo la wakimbizi wengi majirani zetu ambao wamejificha katika misitu, wanapora, wanaua, wanateka magari, bado wako msituni. Ili nchi iweze kuwa na amani, isimamie maendeleo endelevu, kuna

haja ya kufikiria ulinzi wetu unapangwaje hasa ulinzi wa ndani. Mikoa ya katikati haina kazi za kutisha sana lakini ukienda kuanzia Tunduma mpaka Sirari kutokea Mikoa ya Kigoma na Kagera hili ni eneo la nchi yetu ambalo kwa kweli liko katika matatizo makubwa sana kwa sababu ya vita katika nchi jirani.

Kwa hiyo, tungetegemea kwamba vyombo vya dola hasa vya ulinzi na usalama vingekuwepo kule na wakapewa zana za kufanyia kazi zaidi katika maeneo hayo ili kusudi waweze kufanya kazi zao vizuri. Kusema kweli katika maeneo hayo hakuna amani, watu wanakufa hovyo, mali zinaibiwa, watu wanakimbia katika nchi yao kama nao wamekuwa wakimbizi au wana vita vya ndani kwa ndani kama majirani zetu, masuala haya yanarudisha maendeleo nyuma katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unanikimbia, naomba niseme kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naiunga mkono lakini naomba maelezo na maombi niliyoyaweka kwa Serikali yetu kufanyia kazi kwa maendeleo ya wananchi wake na hasa kuondoa umaskini kwa kweli yazingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na moja kwa moja nipeleke salaam zangu za rambirambi kwa familia ya Mbunge mwenzetu wa Kilombero, Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyefariki na kwa kweli kwa wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro kwa sababu katika Bunge hili nimekaa humu tangu mwaka 1995 ni Wabunge karibu watano wamepotea wa Mkoa wa Morogoro na ndio unaoongoza kwa kupoteza Wabunge, nawapa pole sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niseme nakipongeza sana Chama cha Mapinduzi kwa sababu kuu mbili. Kwanza ni kuwa na Katiba na kuamua kuifuata Katiba yake. Katika mchakato huu wa Urais kulikuwa na kila dalili ya fujo, vurugu na nini, lakini sasa ni kimya, mambo shwari, wote tuko pamoja na atakayekuja mbele katika uchaguzi huu tunamfagilia mbali moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza wana CCM wote ambao walijitokeza kugombea na pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa ushindi usio na ubishi pale Chimwaga na kwa Katiba nzuri ya CCM. *(Makofi)*

Mimi nilipata nafasi ya kwanza kushuhudia uchaguzi mkuu na kupiga kura yangu. Nina ombi tu kwamba *next time* kwa kweli tuwape nafasi hawa viongozi, Wabunge, Wabunge wa Upinzani hawa wakaone pale Chimwaga mambo yanavyokwenda. *(Kicheko/Makofi)*

Mimi nilibahatika nikaleta Madiwani wangu niliotoka nao kule upinzani nikarudi CCM na wakashinda vizuri, niliwaleta sita pale Chimwaga. Walivyoangalia utaratibu na maandalizi, wakasema hiki ndio chama ambacho kinafaa kushika dola. Ni vizuri na wao wakaenda ili wakawaeleze kule kwenye vyama vya ubabaishaji kule. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunataka utumishi wa nchi, michakato ya vyama vingine ni ya ajabu. Wewe unaita wajumbe wanalala kwenye *godown,* hakuna chumba cha mwanamke na mwanaume, hakuna choo, hakuna nini. Halafu mnakaa kwenye ukoo tu, wewe uwe Waziri Mkuu, wewe uwe nani, utaunda Serikali ya wapi ya namna hiyo na wajumbe kwenye ukoo wakipungua wanaitwa wanakwaya wa Mbagala wanajaza mle ndani wanavalishwa *t-shirt* za chama. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawapongeza Watanzania kwa kuwa macho na vyama hivi vya ubabaishaji. Tunasumbuliwa na utapeli tu, ni njaa tu inayowasumbua watu hawa. Huwezi kuendesha chama kitapeli tapeli, endesha chama uwe *objective,* uwatumikie wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ombi hili moja kwa moja kwa kweli kwa Msajili wa Vyama. Msajili wa Vyama ndiye mlezi wa vyama lakini *with all due respects, Mr. Tendwa* ni rafiki yangu, tulisoma naye Chuo Kikuu lakini hapa hafanyi kazi. Mimi namwona Bungeni hapa tukianza Bunge yuko hapa asubuhi, mchana, jioni mpaka tunafunga Bunge. Sasa vyama viko vingapi hapa Bungeni? Vyama vifuatwe kule. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa alishasema tunataka vyama vya upinzani imara viweze kumulika na kuikosoa Serikali. Sasa Mheshimiwa Tendwa yuko hapa Bungeni hana hoja Bungeni wala sio Waziri lakini yuko hapa kila siku. Badala ya kwenda kuratibu vyama kule vina wanachama wangapi, ruzuku ngapi inakwenda kule, vina mtandao gani, vina matatizo gani ili aishauri Serikali ilete hoja hapa tumpe hata yeye meno basi ya kuingia ndani kwenye vyama, kuna udikteta mtupu kwenye vyama huko, hakuna demokrasia kila mtu na chama chake kwenye mfuko hata sera hawana. Huyu anasema utajirisho, huyu anasema kujaza watu mifuko wakati amefilisika sasa wewe utajaza nani mifuko ajaye pesa wakati wewe nyumba inapigwa mnada umeshindwa kulipa deni? Wewe umeshindwa kulipa deni ya kukomboa nyumba unayoishi na wajukuu zako wewe unataka kufanya nini, utamjaza nani mapesa? Hivi ni vichekesho tu maana yake ni usanii afadhali na msanii anaweza kupeleka nyimbo za kushauri UKIMWI lakini hawa wanashauri nini sasa? Mambo ya ajabu kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu, ofisi ya Msajili ifanye kazi ili vyama hivi visivyofaa vifutiliwe mbali. Mimi naona hapa hata Wabunge wa Upinzani wanapoteza muda tu. Sasa unakuja hapa bajeti umepewa wewe unasema *no, abstain.* Nashauri ni vizuri Mheshimiwa Spika kabla hatujapiga kura utoe semina watu hapa hawajui *abstain* wala maana ya *no. (Kicheko/Makofi)*

Sasa bajeti hii ndio inatupeleka kwenye uchaguzi na kwa mara ya kwanza nchi hii inagharamia uchaguzi tangu kujiandikisha mpaka kupiga kura, kwa bajeti hii. Sasa mnasema mnaenda Ikulu mtaendaje bila Uchaguzi Mkuu? Unapozuia bajeti hii kwa kusema *no* maana yake tusiende kwenye uchaguzi na wewe unataka uende Ikulu kwa Mapinduzi au kwa namna gani? Tunafanya vitu gani hapa? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unasema *abstain* maana yake wewe huishi Tanzania wala hujui kinachoendelea wala hukuwasikiliza Mawaziri. *Abstain* maana yake hupo popote maana yake ni kitu kimekuvamia hujui! Afadhali hata waliosema *no* maana yake sasa wao labda wameondoka kutoka nyumba wameambiwa kasema *no.* Hata kama unamponyesha kwenye majanga makubwa yeye atasema *no.* Wewe tusikufunge jela *no*, nifunge, sasa unakwenda wapi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema tu kwamba bajeti hii naiunga mkono kabisa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, rafiki yangu kabisa amefanya kazi vizuri kabisa, tunampongeza kwa sababu amekuwa mvumilivu, mshirikishi na msikivu kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunampongeza na bajeti hii kwa kweli napenda ipite kabisa. *(Makofi)*

Tangu mwaka 1995 mpaka 1997-1999 hatukuwa na bajeti za maendeleo, tulikuwa na bajeti za matumizi tu na wakati mimi naanza Ubunge mwaka 1995 tulikuwa tunaona hata wafadhili wanalipa mishahara ya Tanzania, leo nchi hii inalipa mishahara kwa hela ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa ya maendeleo ilikuwa ni ahadi za wafadhili tu. Wabunge tulioingia nao wanajua hili.

**WABUNGE FULANI:** Sana.

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Tulikuwa hatuna *Development Budget.* Leo ukijaribu kuangalia tu mwaka 1998/1999 tulikuwa na bilioni nane za maendeleo *against* bilioni 227 za nje na zilikuwa ni ahadi ambazo nyingine hazikutimizwa. Mwaka 1999 tulikuwa na bilioni 27.17 *against* bilioni 186 za nje leo hapa tulipo tuna bilioni 358 za ndani *against* bilioni 900 zaidi ya theluthi. Sasa hapa hujafanya maendeleo kweli? Ni mambo mengi tu tunafanya jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi tu nilishangaa hata Mbunge wa Bariadi anasema *no,* tumefanya mambo makubwa Bariadi. Kama hana taarifa labda hafiki kule maana mambo yako mengi na yako wazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niyataje hapa...

**WABUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mpango wa *TASAF* Bariadi imepata bilioni mbili *plus,* mpango wa MMEM tumepata bilioni mbili *plus* katika mgao huu wa mwisho, barabara katika bajeti hii inayoisha milioni 460 na tumekwaruza barabara leo hii hata wananchi wa Bariadi wanapata daladala ya gari sio baiskeli tena, yeye hajui! Tumejenga sekondari 10 ziko njiani tumefungua juzi 6/6/2005 sekondari mpya sita. Naishukuru sana Serikali imetupa kipaumbele katika hili. Lakini siyo hilo tu mpango wa MMES, Bariadi ni ya tano katika mgao huu ukiondoa Kinondoni, Mbinga na Tarime tuna milioni 427 na

tuna mpango wa kujenga sekondari kila Kata kuna sekondari 16 ziko njiani katika mpango huu wa MMES tumeshampa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Halafu anasema *no.*

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unasema *no,* tufanye nini? Wewe unayo senti hata moja ya kusaidia hata mshahara wa *VEO? (Kicheko/Makofi)*

Watoto waliofaulu kwenda sekondari Darasa la Saba na wakakosa nafasi, Mheshimiwa Waziri Mkuu namshukuru sana alikuja na akawaambia pale kwamba mna watoto 3,321 wamefaulu hakuna sekondari maana yake Bariadi tuko zaidi ya watu 600,000 katika sensa ya mwaka 2002 lakini tulikuwa na sekondari tano tu za Serikali sasa tumefungua sita ziko kumi na moja na tunafungua nyingine sasa hapa tumeokoa angalau watoto 480 wameanza sekondari, hicho ni kitu cha kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika bajeti hii, Wizara nyingine napenda kuipongeza Serikali, hazitegemei tena wafadhili. Ningetoa mfano Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ina shilingi bilioni 45 za maendeleo, za nje hamna, sasa hawa hawasomi vitabu, sijui wameenda wapi, mbona hawapo hapa? *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Yuko Frank Maghoba.

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu maendeleo ya jamii kuna bilioni 1.3 za ndani, hamna hela ya nje. Bunge hili tunatekeleza miradi ya maendeleo ya Bunge hela ya ndani 0.95 bilioni, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo bilioni 7.2 *against* bilioni 53 tu za nje,

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda nikamilishe, hawa jamaa wamekosa dira kwa kweli na hakuna jipya, unajua hakuna *think tank* kule kila mtu na lwake, huyu anasema hiki. Mimi niliwaambia kaeni pamoja mlipe hata hela. Sasa wewe unapata kitabu cha bajeti hiki nenda ukalipe hata watu wa Chuo Kikuu wakuchambulie ulete hoja za maana hapa. Sasa unakuja tu na mkakati wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata lile la Afrika Mashariki *with due respect* Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani pale, Mheshimiwa BAsil Mramba ametueleza hapa amewatafuta yeye mwenyewe na katika bajeti ndio amesema hilo. Sasa wewe eti unazo siri zote hebu zilete basi ulikuwa wapi mpaka Mheshimiwa Basil Mramba amewatafuta na kuwapa? Leo ndio imekuwa hoja yako? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina maombi tu machache kwa sababu muda hautoshi ningependa nishauri kuhusu kilimo cha pamba na kwa kweli kama tunataka kumsaidia Mheshimiwa Jakaya Kikwete ambaye ni Rais kwa asilimia karibu zote bado kutangazwa tu, kama tunataka kumsaidia lazima tufanye mapinduzi kwenye kilimo. Kama ni bajeti sasa kilimo kipewe kipaumbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo Wizara kama tatu. Wizara ya Kilimo ziunganishwe na Ushirika, hizi ni Wizara zinazosaidiana tu, ni kazi moja tu. Halafu nyingine ni Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ziende pamoja, ng'ombe wale ni mali kabisa ambayo haina ubishi na ndio tunaweza kufanikisha hii mipango ya MKUKUTA au MKURABITA. Kwa hiyo, tuwazingatie ng'ombe ili tupate manufaa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kulikuwa na swali hapa, aliuliza Mheshimiwa Leonard Derefa. Kwa kweli hili swali halikujibiwa na Serikali. Haiwezekani Serikali ijitoe katika zao la pamba, huwezi kusema mkulima aelewane na mfanyabiashara wakati Ushirika haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapohimiza kilimo tuhimize na masoko ya mazao yanayozalishwa kwenye kilimo. Sasa tutafanya nini, utakutana na MKUKUTA kama hujazingatia bei ya mazao. Mheshimiwa Richard Ndassa alizungumza jana, akasema bei ni senti 44, hapana, mimi nimeangalia leo kwenye *internet* ni senti 54 bei ya kilo moja ya *lint.* Kwa maana hiyo, kilo moja ya *lint* itauzwa shilingi 1298/=, ukii-*convert* kilo moja ya *lint* inazalishwa na kilo tatu za pamba mbegu, maana yake pamba mbegu anayouza mkulima kule lazima inunuliwe kwa shilingi 420/=. Leo mtu anapewa shilingi 170/= Vijijini na Serikali mpo, hapana. Watu wa *ginnery* ni magabachori na ni wezi.

Mimi nasema Serikali hii ilete *computation,* ifanye tathmini kuzalisha kilo moja ya pamba mbegu ni kiasi gani. Itangaze basi ili hata mkulima akienda kuuza kwa hasara anajua yeye mwenyewe. Kwa nini wataalam tunao kule wa Ushirika, Kilimo na wengine hawafanyi hiyo kazi. Mkulima sasa anakwenda anahangaika, hajui amezalisha kwa gharama gani, anauza, anapigwa bei tena wakati mwingine anakopwa. Sasa kweli ndugu zangu tutafika? Hakuna cha MKUKUTA wala MKURABITA na tutabadilisha maneno mpaka tutachoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kabisa kwa kusema kwamba, Wizara hii ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Ushirika na Masoko zianze sasa na nguvu mpya, kasi mpya na ari mpya. Kwa mfano, viazi pale Gairo. Mimi nilishasema siku moja kwamba hizi ni mali na ni utajiri. Basi wavi-*process* viwe *reserved* kwani vitasaidia hata wakati wa njaa. Sisi tuna kitu kinaitwa mchembe kule kwetu, ni viazi hivi hivi. Vinatumika zaidi na vinaokoa wakati wa njaa.

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba, Serikali lazima isimamie bei ya pamba, sio kujitoa na isimamie Ushirika. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumza kwamba ataimarisha Ushirika na kuangalia viongozi wake katika uchaguzi wao, lakini haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote na ninawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wenzangu turudi ili tuibane Serikali yetu, tuisaidie ili iweze kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri aliyoitoa na maelezo sahihi ambayo kwa kweli kila kitu kimeelezwa na napenda niseme kwamba wenzangu wa Upinzani wakichukue hiki kitabu wakisome, warudie na kurudia na kama hawavai miwani basi wavae miwani ili waangalie jinsi Chama cha Mapinduzi kilivyotekeleza Ilani yake na kuweza kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam zangu za rambirambi kwa Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na naomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi kumi na moja waliojitokeza kugombea nafasi ya kuteuliwa kugombea Urais chini ya Chama cha Mapinduzi. Naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuteuliwa kupeperusha bendera ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuteuliwa kuwa mgombea Urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na nina uhakika tutashinda kwa kishindo kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, pamoja na askari wote wa miavuli. Kwa kweli wote tumeshuhudia jinsi ambavyo wametekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kazi zote zimetekelezwa vizuri wakisaidiana na Wakuu wa Mikoa ambao wapo hapa kwenye *gallery,* Wakuu wote wa Wilaya na watendaji wote wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la utekelezaji hasa suala la watoto. Suala la watoto limezungumzwa kwa kina, amelizungumzia pia Mheshimiwa Gwassa Sebabili na mimi mwaka jana nilizungumzia suala hili na naipongeza Serikali kwamba iliunda idara katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii kushughulikia suala la watoto, lakini naona bado haitoshi. Kwani tatizo kubwa linalojitokeza na tunavyoona kwamba kuna wimbi kubwa la watoto zaidi ya milioni mbili ambao ni yatima na ambao wanaishi kwenye mazingira magumu, mahitaji yao yameendelea kuwa mengi na kwa sasa tunatakiwa tutazame upya na tuone kama je, bado tunahitaji kuwa na sehemu mbili au zaidi ya mbili ambapo watoto hawa wanahudumiwa. Wanahudumiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, wanahudumiwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, wakiwa wagonjwa tunawakuta Wizara ya Afya, wakiwa chini ya miaka mitano wakiwa shule ya msingi wapo Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri kwamba, sasa wakati umefika iundwe Kamisheni tofauti au Idara inayojitegemea chini ya Wizara moja itakayoshughulikia masuala ya watoto na ndani ya hiyo kutakuwa na vitengo mbalimbali. Hapo ndipo tutakapoweza kuhudumia hawa watoto vizuri zaidi, la sivyo, tutakuwa tunagusa juu juu. Hatuwezi kuhudumia matatizo ya watoto yanayojitokeza sasa hivi kama kuna sehemu

mbalimbali ambako hawa watoto wanahudumiwa. Ni pale tu tutakapoangalia upya, kuona kwamba je, hivi bado tunahitaji kuwa na vitengo mbalimbali au tuweke chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambako watoto ndipo walipo, iwekwe hiyo idara maalum inayojitegemea au taasisi au Kamisheni inayojitegemea chini ya Wizara hiyo itakayosimamia watoto wote. Sio watoto wengine wapo upande huu na wengine wapo upande mwingine, kuwahudumia inakuwa ni vigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa napenda niishauri Serikali kwamba tuliangalie upya hili suala la watoto ili tuweze kuwahudumia vizuri zaidi hawa watoto, kwa sababu tuna watoto wanahitaji msaada wa kisaikolojia je, wanatoa wapi? Tuna wataalam wangapi tuliowafundisha huko Vijijini wanaotoa msaada wa kisaikolojia kwa hawa watoto? Hawa watoto wanahitaji masuala ya sheria ili kulinda haki zao, wanazipata wapi? Pia tuna watoto wa umri 0 mpaka miaka nane ambapo wapo kwenye tunasema *early childhood* ambao wanahitaji masuala ya makuzi. Je, maendeleo yao yanapatikana wapi au idara gani ambayo inashughulikia? Watoto pia wakianza shule za awali wanaingia kwenye Wizara ya Elimu na wakiwa kwenye shule za chekechea, wanakuwa Wizara ya Kazi, sasa hapa tutakuwa tunayumba.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naendelea kutilia mkazo kwamba tuliangalie upya, tujipange upya, tuone hawa watoto wanawekwa katika kitengo gani ambacho kinajitegemea au idara maalum inayojitegemea chini ya Wizara moja ili waweze kuhudumiwa vizuri zaidi.

Suala lingine ninalopenda kulizungumzia ni suala la miundombinu. Naipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya hasa kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na barabara na mawasiliano. Mawasiliano ya simu na miundombinu ikiboreka ina maana kwamba hata wakulima Vijijini wanaweza kusafirisha mazao yao kwa urahisi. Sasa leo miundombinu ambayo imeboreshwa chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndio huko Wapinzani wanakopita wakikimbia kwenda Vijijini, halafu wakifika Vijijini wanasema, hakuna lolote lililofanyika. Hivi ni kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa kulikuwa na viongozi fulani wawili wa Vyama vya Upinzani, viongozi wa Kitaifa, mwingine ni mwenzetu humu humu, walikuwa huko Ludewa. Barabara nzuri, wanakimbia huko, halafu wanawaambia wananchi hakuna lolote ambalo Chama cha Mapinduzi kimefanya. Hivi yeye angeweza kufika Ludewa mpaka huko ndani kama sio Chama cha Mapinduzi kujenga barabara. Huko Vijijini ukienda barabara zimeboreka mpaka Jimbo la Ismani huko wanaweza kupita kwa urahisi. Zote hizi ni juhudi zilizofanywa na Chama cha Mapinduzi na ndio maana sasa dakika hizi za majeruhi wanakimbia kwenda Vijijini kwa kupitia barabara zilizojengwa vizuri na zinazopitika kwa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuboresha barabara kama nilivyosema tunaweza kupata masoko ya bidhaa zetu kwa sababu wakati mwingine inakuwa ni vigumu kama barabara hazipitiki kuweza kuuza mazao na ndio maana wananchi wanakosa masoko hasa ya mahindi yanayolimwa kule Vijijini kwani ni vigumu kuyatoa. Mfano mzuri

ambao ningependa niuseme na kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie kwa vizuri zaidi, ni kuhusu barabara inayotoka Njombe kwenda Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hii barabara inatakiwa iangaliwe na ikiwezekana basi tujengewe barabara ya lami ili wawekezaji waweze kuwekeza Makete na kwa sababu ni mahali penye hewa nzuri, milima yake inavutia, kwa hiyo, hata watalii wanaweza kwenda kuiangalia na sasa hivi tumepata *National Park.*

Sasa napenda iangaliwe vizuri kama hii barabara itakuwa imejengwa ikafikia kiwango cha lami, basi wawekezaji wataweza kuwekeza kule, ajira zitapatikana, wananchi hawataweza kuhama kutoka kwenye Wilaya ile na kwenda sehemu nyingine na hatimaye yale matatizo yaliyopo ya tatizo la UKIMWI kwa sababu wananchi wengi wanahama, wanaondoka kule na wanakuja kwa msimu, yanaweza kupungua na tunaweza pia kujikomboa kwa kupunguza umaskini uliopo katika Wilaya ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri wananchi wale wataweza kusafirisha mbao zao. Sasa hivi wananchi wanapasua mbao, lakini kwa vile barabara sio nzuri sana, soko la mbao linakuwa sio zuri na wanauza ubao mmoja hata kwa shilingi mia moja sawasawa na bure tu ili mradi apasue miti yake. Naona hapa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi hayupo, lakini nafikiri kwamba nimesema mahali penyewe, kwamba hebu iangaliwe vizuri zaidi jinsi gani ambapo tunaweza kuboresha mawasiliano ya Wilaya ile ili kuweza kupitika kwa mwaka mzima na ili tuweze kupata wawekezaji zaidi wa kuweza kuwekeza katika Wilaya kwa kujenga mahoteli ya kitalii, maana yake kule hali ya hewa ni nzuri, watu wa nchi nzima wanaweza kuwa wanakwenda likizo kwa sababu kule kuna baridi na magonjwa sio mengi sana ukiachia mbali tatizo la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la mazao hasa kilimo cha mazao ya asili. Ni jambo la muhimu sana sasa hivi tuzingatie kilimo cha mazao ya asili. Pia naomba taarifa mbalimbali za mazao haya, masoko yalipo zitolewe kwenye ngazi za Wilaya. Nina uhakika kama ngazi ya Wilaya ikipata taarifa itapeleka kwenye ngazi zinazohusika. Wakati mwingine unakwenda unakuta mahali labda ukienda sehemu za Wizarani unakuta labda wanasema sehemu fulani mazao fulani yana soko mpaka nchi za nje, lakini wale wahusika katika Wilaya ile wanakuwa hawafahamu kama hili zao lina soko au halina soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo nilikuwa nasikia Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo alikuwa anajibu swali kuhusu kilimo cha zao la soya na kwamba zao linaagizwa nchi za nje kwa ajili ya kulisha mifugo. Lakini mimi ninavyoelewa ni kwamba soya inaweza kulimwa hapa hapa nchini hata Wilaya ya Mufindi inaweza kulimwa vizuri sana, wananchi wakapata pesa wakaondokana na umaskini na wakati huo huo wakauza kwa ajili ya kulisha mifugo, lakini pia wakaweza kuandaa chakula kwa sababu soya ina maziwa mazuri sana ambayo yanaweza kutumika kuboresha lishe na hawa wakati huu ambao tunazungumzia suala la lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, ni jambo la muhimu sana kuwa na taarifa za mazao yale ambayo yana masoko na taarifa hizi

zipatikane kwenye ngazi za chini na pia taarifa za uwekezaji.  Kituo cha Uwekezaji kinafanya jitihada kubwa sana na Mikoa inajitahidi.

Mimi Mkoa wangu wa Iringa unajitahidi sana kuhakikisha kwamba wawekezaji wanakuja pale na jitihada kubwa inafanyika ya kuandaa mkutano wa wawekezaji.  Lakini tulikuwa tunafikiri kwamba taarifa hizi za maeneo ya uwekezaji yaliyoko katika Wilaya fulani basi nazo zipatikane kwenye Wilaya husika, Maafisa Biashara waweze kushirikishwa vizuri ili wawe wanatoa hizi taarifa badala ya kuzipata nje ya Mikoa, basi zote ziwe zinapatikana kwenye ngazi husika, kama ni kwenye Wilaya iwe Wilaya ile, kama hilo eneo lipo kwenye Tarafa fulani basi hiyo Tarafa ipewe taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninaloweza kuchangia ni suala la Vyama vya Kuweka na Kukopa.  Ili tuepukane na umaskini sasa hivi suala la Vyama vya Kuweka na Kukopa ni muhimu sana na sasa hivi wanawake wamejitahidi, wapo kwenye Vyama vya Kuweka na Kukopa lakini tatizo kubwa ni kwamba hawana mafunzo ya ujasiriamali, wanaweka lakini miradi yao wanayofanya wanaifanya bila mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri kwamba suala la mafunzo ya ujasiriamali litiliwe mkazo na ile mikopo ambayo inatolewa na Halmashauri basi kwenye Wilaya ambako wanawake watakuwa wameunda vikundi vya kiuchumi au *SACCOS* zao, basi ile mikopo ipitie kule ndani ili wao wenyewe waweze kukopeshana na wapewe mafunzo ya kuweza kuendesha miradi yao na kuchambua miradi ambayo inakubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia, ni vituo vya Kijamii *(Community Centres).*  Leo ni mara ya pili nazungumzia hili suala, nafikiri kwamba ni muhimu sana kuwa na Vituo vya Kijamii katika Vijiji au katika Wilaya angalau kila Wilaya iwe na kituo *(Community Centre)* ambako wananchi wanaweza kukaa wakabadilishana mawazo. Hilo ni jambo muhimu sana hasa tunapozungumzia maendeleo.  Inawezekana hata taarifa hizo nyingine zinazopatikana zingekuwa zinawekwa ndani ya *Community Centre* pale na wananchi wanaweza kujisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia suala la wodi ya wanawake Wilaya ya Ludewa, *Maternity Ward* na *Labour Ward* za Wilaya ya Ludewa. Mwaka huu naambiwa zimetengwa shilingi milioni 4 kwa ajili ya *Labour Ward* au *Maternity Ward* katika Wilaya ya Ludewa. Nafikiri kwamba hizo fedha haziwezi kutosha kujenga *Maternity Ward.*  Wanawake wanachanganyika, wale wanaojifungua na wale wanaoumwa magonjwa ya kawaida. Nafikiri kwamba ni jambo la msingi Serikali, itusaidie kuweza kupata fedha za ziada kuisaidia Wilaya ili kuweza kuwa na *Labour Ward* ya uhakika na *Maternity Ward* kwa ajili ya hospitali ya Wilaya ya Ludewa kwa sababu wanawake wameongezeka na Wilaya ile haina hospitali nyingi ambazo inazitegemea, ni hospitali ile ndio inayotegemewa ni ile ndio kubwa ukiacha zile nyingine za mashirika ya dini.  Kwa hiyo, naomba jitihada zifanyike kuhakikisha kwamba kunakuwa na maternity na labour wards katika hospitali ya Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.  *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kwa kutuma salaam za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Abu Kiwanga, ambaye tulikuwa naye katika kipindi kilichopita na hivi sasa ameshatangulia mbele ya haki na tumwombee kwa Mwenyezi Mungu roho yake aiweke mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe salaam za pongezi kwa wagombea wa CCM ambao wameteuliwa na Chama cha Mapinduzi kugombea nafasi za Urais. Salaam hizo ziende kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume. Tuna imani na uhakika kwamba hao ndio watakaoliongoza jahazi hili la Tanzania na kuendelea kukitetea Chama cha Mapinduzi kuendelea kushika hatamu za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza nimpongeze kwa hotuba hii ambayo ni nzuri na ambayo imechukua eneo kubwa au eneo lote la awamu hii ya tatu kwa kipindi hiki cha miaka kumi. Tuseme kwamba hii hotuba ni nzuri isipokuwa kazi iliyopo mbele yetu sasa ni kuendelea tu kuiboresha. Kwa kweli ime-*cover* karibu maeneo yote muhimu kwa maslahi ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie baadhi tu ya maeneo ambayo nilikuwa nahisi tunaweza labda kuyafanyia ukarabati mdogo mdogo ambao pengine unaweza kutusaidia kwa kiwango kikubwa. Mimi nianzie na Ofisi ya Bunge. Katika kipindi hiki cha miaka mitano baada ya hatua ya mwanzo ya Kamati za Bunge mabadiliko ambayo yalikuwa yamefanyika tumekwenda nayo kama sikosei kwa miaka mitatu ambapo Kamati tunakwenda nazo mpaka kumalizia kunako mwezi huu unaofuatia hapo mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichojifunza kwamba Kamati zimefanya kazi nzuri na zinastahili pongezi, lakini bado kuna haja ya kufanya mabadiliko madogo madogo. Tumekuwa na kawaida Kamati za Bunge zinakutana wiki mbili kabla ya kikao cha Bunge. Matokeo yake kuna maeneo mengi ambayo bado tunayaacha yakiwa hayajafanyiwa kazi. Mimi ni mjumbe katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Niseme kwamba mfano katika eneo la TAMISEMI, Kamati ile inakuwa na jukumu la kupitisha bajeti ya Mikoa ishirini na moja, lakini ndani ya kipindi cha miaka mitatu hii katika Kamati hiyo tumefanya ziara Mkoa wa Pwani tu labda na sehemu nyingine hizi za Wizarani. Kwa maana hiyo, tumekuwa tukipitisha bajeti kwa kutumia vitabu bila kuona zile fedha zimetengwa kwa kiwango gani, zimefika na zimetumika ipasavyo. Kwa hiyo, tunapokea ripoti tunasema *okay* endelea, *okay* sawa, twende mbele. Sasa lile jukumu la kusimamia matumizi bora ya fedha za Serikali maana yake hapo kuna upungufu mkubwa sana. Sasa hali hiyo ipo kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na hata Kamati nyingine nazo zipo hivyo hivyo kwa sababu kwa wiki mbili si kweli kwamba unaweza kusimamia katika maeneo yote ya Wizara kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vyema huu utaratibu tungeubadilisha ili Kamati zifanye kazi zake ipasavyo. Mfano mzuri, wenzetu wa Kenya na Uganda, wanatumia muda mwingi ndani ya Kamati kuliko muda wa vikao katika Bunge. Madhumuni makuu ya kufanya hivyo ni kuhakikisha ule usimamizi unafikia kile kiwango kinachohitajika. Kwa hiyo, hilo la wenzetu nadhani ni zuri na linafaa kuliiga ili ule ufanisi wa kusimamia fedha za Serikali uwe umekamilika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Ofisi hii ya Bunge imeendelea na kazi za ujenzi ambazo kwa hilo napongeza, pengine kwa kuliweka Bunge katika nafasi yake inayostahili. Lakini kuna ofisi ndogo za Bunge mbili, moja ipo Dar es Salaam na nyingine ipo Zanzibar. Sasa nataka kuzungumzia ile ya Zanzibar.

Kwanza nipongeze lile jengo lililojengwa, ni zuri na lina hadhi ya kuitwa Ofisi ndogo ya Bunge, lakini kabla ya hapo ile ofisi ambayo ilikuwepo ni jengo tu la kawaida sana, ambalo pengine hata Mheshimiwa Waziri Mkuu hakuwahi kulitembelea, lakini pia nimpongeze kwa kutolitembelea kwa sababu kuna hatari pengine angekwenda pale kwa hali ya lile jengo angeweza hata kuugua *Sars* pale ikawa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jengo jipya ni zuri na lina hadhi, lakini sasa katika muundo wa Ofisi ya Bunge, ofisi ile haionekani. Sasa ni vema kama inaitwa Ofisi Ndogo basi angalau ule muundo wa Bunge iwe inaonekana na ijulikane hadhi yake. Mfano ukiangalia zipo taasisi zingine zina ofisi zake pale Zanzibar. Mfano, Jeshi la Polisi linaeleweka, Uhamiaji, Msajili wa Vyama vya Siasa na nyinginezo, lakini sasa ile hatuijui nafasi yake na hadhi yake ni ipi. Kwa hiyo, nadhani hilo lingefanyiwa kazi ikawa na hadhi yake na inaeleweka. Kwa sababu maelezo ni kwamba kuna kumbi katika hilo jengo jipya ambapo Kamati zitakutana. Kwa hiyo, ni vyema na hilo nalo lingeonekana na likafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niondoke hapo niende kunako mtiririko wa masuala ya uchaguzi na siasa. Kwanza ningeomba labda kurudia katika hiki kitabu ambapo kidogo kuna tatizo la takwimu. Katika ukurasa wa 93, nadhani hapa kuna makosa kidogo ambayo yangefanyiwa marekebisho katika kiambatisho namba 7, uandikishaji wa wapiga kura katika daftari la kudumu la wapiga kura, chini kabisa imetajwa Zanzibar ambapo wametajwa watu 15,000 waliojiandikisha. Hii nadhani si sahihi. Kwa hiyo, najua hawa wapinzani wana tabia ya kurukia rukia, hasa hawa wa *CUF,* sasa wasije kudhani wameshapata *agenda.* Kwa hiyo, nadhani hii nayo kidogo ingefanyiwa masahihisho ikawekwa namba sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika harakati hizi za uchaguzi huwa ulinzi unahitajika kwa kiwango kikubwa sana na hasa nikizungumzia mazingira yale ya Zanzibar tuliyopo sisi, kazi inakuwa nzito sana. Niwapongeze Askari Polisi ambao huwa wanajitahidi kwa kiwango kikubwa sana kudhibiti hali na kudumisha usalama. Lakini lipo tatizo ndani ya hili Jeshi la Polisi, ningetumia nafasi hii pengine kulizungumza kabisa ili itakapowasilishwa hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani hili suala tupate kujua Wizara inalitazamaje na inachukua hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, kuna habari moja ya kusikitisha sana kuhusu Askari Polisi wa Zanzibar, kuna askari ambao hawajalipwa mishahara hivi sasa mwaka mzima. Tatizo hilo limekuja kutokana na kwamba, hawa askari walipelekwa kozi. Sasa wakati wanapelekwa kozi kulingana na vyeo vyao, kabla ya kwenda kozi walikuwa wamekaribia kufikia ule umri wa kustaafu. Baada ya kwenda kozi wamepanda vyeo, maana yake sasa muda wa kustaafu unabadilika. Lakini ilipofika mwezi wa Juni tayari wameondolewa katika list ya mshahara. Kwa maana hiyo wapo ambao hawajapata mshahara mpaka hivi tunavyozungumza, wana mwaka mzima tokea Julai mwaka jana mpaka leo tupo Juni na keshokutwa tunaingia Julai hawajalipwa. Wapo wengine baada ya usumbufu wa muda mrefu wakaingizwa katika *list* ya mshahara kuanzia Machi, sasa malimbikizo yao nayo hayajalipwa. Sasa tatizo hili tumejaribu kulitafuta, hatua zilichukuliwa kuandikiwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi lakini haieleweki tatizo ni nini mpaka hivi sasa. Wapo watu wamevaa vyeo vya Sajenti na kuendelea, wengine Makoplo lakini mishahara wanayolipwa ni *privates,* tatizo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani hili likachukuliwa ili kutafutiwa ufumbuzi wa haraka kwani hawa watu wanateseka. Huwezi kuwa na familia ukawaambia mimi mwaka mzima sijalipwa mshahara wakatuelewa. Huduma za lazima zinawakabili pale pale na kazini wanaendelea kwenda, maana yake hawana muda wa kushughulika na njia nyingine za kuendesha maisha yao.

Kwa hiyo, hilo nalo ni vema likafanyiwa kazi ipasavyo ili kuwapunguzia mzigo wa maisha ambao sio wa lazima kwao kuukabili kwa sababu katika bajeti mishahara yao imo lakini hawalipwi, kwa nini? Kwa hiyo, naomba Serikali iifanyie kazi ili kuwapunguzia huu mzigo ambao nina hakika umo ndani ya uwezo wa Wizara ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kuzungumzia kuhusu suala la uhusiano wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kikao kilichopita hapa tulizungumzia kuhusu kuharakisha suala la huu Umoja wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Wabunge wengi ni kwamba tulikuwa twende pole pole na mimi hilo ningeomba kulisisitiza, bado azma ya kwenda pole pole iendelee kuwepo pale pale kwa sababu ule utaratibu wa kuingia katika umoja wa Forodha, Sarafu, *Free Movements* na ile *Common Market* maana yake tukamilishe hayo, ndio tuingie katika ile *Political Union* au Umoja wa Kisiasa au ndio hiyo *federation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haraka haraka hizo tukienda kwa haraka maana yake haya yote tumeharakisha kwa pamoja, lakini ukweli ulivyo tathmini ninayoiona mimi tunapofanya tathmini zetu ndani ya maeneo ya Watanzania bado hatujawa tayari hata katika haya mambo mengine. Mfano, Umoja wa Sarafu hiyo *Free Movement* bado hatujawa tayari. Kwa hiyo, twende hatua kwa hatua, twende pole pole mpaka tufikie hapo tunapotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndani ya umoja huu nimejaribu kuangalia angalia sijaona miradi ambayo inatazamwa na hii Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo inaihusisha Zanzibar, sasa pengine hili litakuwa ni tatizo la Tanzania. Kwa hiyo, ni vyema tunapozungumzia kuunganisha barabara kutoka Kusini mpaka Kaskazini, huwezi ukasema barabara ya Zanzibar. Kuna suala la umeme, lakini bado limekuwepo tatizo la umeme Pemba kwa muda mrefu sana kwa nini lisiingizwe katika programu hiyo ya Afrika Mashariki, tukaona Jumuiya ya Afrika inasaidia saidiaje katika kubuni hiyo miradi ya kufanikisha hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya uvuvi naona bado yako kimya ambayo nayo yange-*benefit* Zanzibar, lakini bado hayajapewa hicho kipaumbele. Kwa hiyo, ningeomba na hilo Serikali ikalitazama ili tusifike mahali tukajikuta kwamba Zanzibar kazi yake ni kuzungumzia au kupiga makofi kuhusiana na masuala ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, ni vyema na hilo tukalitazama. Kwa sababu pia ukiangalia mazingira haya ya *Free Movement* bila ya kuona umuhimu wa kuelekeza miradi mahali kama Zanzibar unaweza kukuta umeiweka mahali pagumu sana kwa sababu bado haijawa na ile *manpower* au tuseme *compitent* ya *manpower* kulinganisha na hizi nchi nyingine za Mashariki.

Kwa hiyo, bado ina hatari ya kutokuwa na *manpower* ambayo itaweza kwanza kujiajiri yenyewe pana uwezekano mkubwa hata ajira za ndani zikachukuliwa na wageni. Kwa hiyo, tuitazame katika mtazamo maalum kuinusuru hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameizungumza katika Hotuba yake kama ule wa *TASAF.* Mimi niseme kwamba miradi imefanikiwa pamoja na kwamba Wapinzani hawaoni hilo, lakini siyo kama hawaoni bado wanajifanya hawaoni. Mimi katika Jimbo langu huu miradi wa *TASAF* lazima nitoe shukrani kwamba tumefanikiwa kupata miradi miwili kuna Mradi wa Maji na mradi wa Kituo cha Afya hayo ni mafanikio makubwa na imetusaidia kwa kiwango kikubwa sana kwa hiyo, hilo nitoe pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu hakuuzungumzia kabisa katika hotuba yake, kuna mradi mmoja ambao tuliwahi kufanyiwa semina unaitwa *PADEP* kifupisho chake, kirefu chake sikikumbuki vizuri ambao nao ulikuwa na fedha nyingi sana *items of billions* huo haukutajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sifahamu kwa nini haukuzungumziwa pengine kwa bahati mbaya, vinginevyo labda nao pengine ungezungumziwa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anafanya majumuisho tukaona nao kwa kiwango gani umewasaidia Watanzania pengine pia itakuwa ni kuendelea vile vile kuwafilisi Wapinzani kuonyesha mafanikio ya miradi ambayo imebuniwa na Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nizungumzie kuhusiana na matatizo mengine ambayo pia kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nishukuru kwa kupata nafasi hii kuweza pia kuchangia katika hotuba hii ya ndugu yetu Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie nafasi hii kutoa pole sana kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, natoa pole kwa ndugu waliobaki tunasema Baba Mungu kapenda, kachukua aliye wake. Kwa hiyo, tunawajaza imani waendelee kuvumilia ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ustaarabu, siku zote walikuwa wanasema sisi *especially African's Country* huwa si rahisi kutoka kwenye madaraka na mpaka labda ulazimishwe au *system.* Ni watu wachache sana katika dunia hii akiwemo Marehemu Mwalimu Julius Nyerere ambaye alistaafu tu akasema muda umefika *let me resign or* nikae pembeni angalau niendelea ku-*watch* nchi ya Tanzania nikiwa na nguvu. Kwa hiyo, hata Mheshimiwa Waziri Mkuu ameona hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ni kawaida kwa viongozi, akina sisi unapokuwa kwenye madaraka kama una dhambi nyingi basi utang'ang'ania kuwepo ili uendelee kuhakikisha kwamba dhambi zako zinalindwa. Kwa hiyo, ukiona mtu kama huyu anatoka, basi unahisi kwamba labda hata waliyosema huenda walipandikiza tu. Kwa hiyo, mimi naomba nimshukuru kwa hilo na nimpongeze, ni ujasiri. Pia naomba nitumie nafasi hii niseme *let you watch the country and then try again after five years* nitakuwa *assistant campaign manager* wake kama ataamua kugombea. Hilo namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba pia nijaribu kugusia hotuba iliyopita ambayo sikuweza kuichangia ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mimi naomba nimhakikishie kwamba siku zote Wapinzani siyo wa kufuata mdundiko. Nitawambia kwa nini? Binadamu tumeumbwa na hulka tofauti, si rahisi kukuta kati ya watu 200 wote wakakubaliana na jambo moja, si rahisi. Lakini sisi kwa Wapinzani juzi tumeonyesha jambo la ajabu, kuna waliosema ndiyo, hapana na *abstain.* Kwa hiyo, hiyo inaonyesha kwamba hawa binadamu wamekomaa, kuna walioona inafaa na kupinga si kwamba unapinga hotuba bali hujakubaliana na mambo mawili, matatu. Sasa unataka kumtahadharisha yule kwamba mawili, matatu. sijayakubali.

Mheshimiwa Mweyekiti, sasa wewe ukisimama kusema naunga mkono halafu katika kuchangia unasema napinga hili, unakuwa kigeugeu na tunashauriwa kwamba sisi viongozi tuwe *straight forward.* Wanasema *I should go, I will never,* kwa hiyo, nilitaka kuwaambia kwamba *I should go forward* kama ni *forward* basi nitakwenda, lakini usirudi nyuma. Kwa hiyo, ndiyo binadamu unatakiwa kuwa hivyo unapoongelea la maendeleo.

Kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba sisi nafikiri ndiyo tuko sahihi. Kwa hiyo, waliounga mkono binadamu wote 200 halafu wote mnakubaliana 200 kuna nini? Nimejiuliza sana, usiku sijalala kabisa, sikulala najiuliza watu 200 wote vichwa vyao kweli vinafanana! Maana yake ukiangalia mwingine kichwa kiko hivi na mwingine kiko vile sasa wote eti 200 wafanane kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nikwambie hili la haraka haraka kwamba kuna tatizo katika Bunge lako Tukufu. Tatizo lililopo ni kwamba Vyama vyetu vinatubana mno huwezi kutoa hisia zako, huwezi kuwa huru kwenye moyo wako unalazimika kukubaliana hata na kile unachohisi kwamba si kizuri. Kwa sababu sisi ni binadamu tunahitaji kazi, tunahitaji mazingira mazuri ya kuishi, sasa ndiyo umepata Ubunge, halafu kesho wakwambie hata kadi wanakunyanganya kisa wewe siyo mwenzao unafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba jambo moja na utanifikisha hii hoja kwa Mheshimiwa Spika japo nilisikia anastaafu, kama ataendelea mwambie hivi Bunge lijalo wajitahidi Mbunge aweze kuhama Chama akiwa anaendelea kuwa Mbunge maadam ameshachaguliwa aweze kuhama Chama kama unapingana na hoja kuwa na msimamo hama Chama ingia Chama kingine endeleza hoja yako usibanwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila hivyo ndugu zangu kwa sababu nimeshuhudia, ninaweza kuhisi kwamba nimeshindwa kuendelea, ninasikitika tunalipoteza Bunge tunakuwa *rubber stamp* kama wananchi wanavyotusema kutokana na *system* za Vyama vyetu, tunakubali hata kisicho haki. Leo hii tutasema madini ni bilioni 50, madini peke yake tuliyouza ambayo wao wame-*declare* ni trilioni yameingiza katika benki nje zaidi ya trilioni 15. Bajeti yetu sisi wenyewe ni trilioni 4 ina maana tusingeweza kuwatoza hata wapiga kura tungeweza kutumia hata madini tu. Tukasema leo *enjoy* wanaita nini, *grace period,* kwenye mabenki, kwa hiyo, *enjoy* usilipe kodi, sisi tunatumia fedha ya madini ambayo Mwenyezi Mungu ametupa. Maana yake Mungu alisema nitakuweka kwenye nchi ya maziwa na asali, amekupenda amekuweka hapa anakupenda. Halafu wewe unabaki umelala tu wanabeba halafu *you are enjoying,* halafu ukija hapa unasema lakini unajua ninaunga hoja mkono, unaunga nini? *What are you supporting?* Wewe unaibiwa kabisa kisa eti Chama kitakwambia kinakunyanganya kadi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniwasilishie hiyo hoja. Ninaliomba Bunge lako Tukufu lisijigeuze kuwa mbadala wa Serikali wala Chama, lazima lisimame kama Bunge, lilinde hadhi ya Bunge na Bunge ndiyo mwongozo na hii ni timu ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza hilo naomba kusema kwamba Wapinzani tunajua kabisa na tuna akili timamu. *We are here and we know.* Kwa hiyo, wasije wakatuona kama ni watu pungufu, tuna akili nzuri tu. *We can do better than.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niondoe dhana ambayo imejengeka kwa sababu nimekuwa nikisikia hotuba nyingi zinalalama, akisimama anasema Awamu ya Tatu imefanya maajabu, Awamu ya Tatu, lakini Awamu ya Kwanza hawaisemi.

Mimi ni mjamaa na nasikitika na ujamaa wangu umetokana na kwamba mimi nimeandika vitabu vingi nafikiri vinatumika Tanzania nzima, vinatumika sasa hivi Kenya na katika nchi mbalimbali vya *Civics, General Study* na vingine sasa hivi wanavitumia mpaka *University* na vimetokana na *research* nyingi ambazo nimezifanyia kupitia Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, *it was the best and we will never get him.* Kwa sababu wengi ni ujanja tu ili mradi awepo *and will saying* unajua mwalimu, lakini *they are wrong.* Kwa sababu mimi nimefanya *research* nzuri ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwataarifu kwamba nimetembelea zaidi ya nchi 50 katika *research* yangu. Katika *research* nchi zaidi ya 50 na nimetembea kwenda nje zaidi ya mara 120 *you can't believe* na yote ni kutokana na *research.* Kwa hiyo, najua ninachokiongea ndiyo wakati mwingine naweza kukuona nikajua hujui, lakini kwa sababu wewe unataka kunilazimisha unajua *I will follow you* kwa sababu uko kwenye *system* nifanye nini ulimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi juzi naweza kuwapa mfano mmoja wa ajabu sana nchi yetu inaenda mahali pabaya. Mimi juzi Waheshimiwa Wabunge nimesikitika sana nilikuwa kwenye mchango wa Mfuko wa Elimu tukatangaziwa kwamba kuna Mfuko wa Elimu, nikaenda mimi na watu mbalimbali na tulikuwa na Waheshimiwa Mawaziri pale, kufika madini wanatoa 300,000/= madini sijui Geita wengine 200,000/= kwa kweli mimi ilinigonga rohoni, *I know them* nafahamu wanavuna nini kutoka katika nchi yetu. Kwa hiyo, nilitegemea kwamba maadam wangesema kwamba tumewalia sana *lets invest to their children* lakini walitoa 300,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli nilisikitika nilikuwa na akiba nyingine nikapiga simu nyumbani kwamba nina akiba yangu naomba kote leta nikatoa 2,000,000/= nikasema ngoja mimi ni-*invest* kwa watoto wetu, kwa mapenzi. Lakini maajabu Waheshimiwa Wabunge juzi napewa taarifa kwamba *account* zangu zote sasa hivi ziko chini ya *under* sijui wanaita nini, *my God* ni nchi gani hii! Mimi ninajitoa *openly, hardly,* naisaidia jamii yangu leo eti mnaenda kuchunguza *account* zangu zote kujua huyu mtu anapata fedha wapi, kwa nini msiende mkachunguza hao wenye madini kwa nini watoe 300,000/= ni kweli hawana fedha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapanda ndege kila siku asubuhi kutoka Dar es Salaam kwenda Kahama, leo mnakwenda kuchunguza *account* yangu. Mpaka wa Meneja wa benki anashangaa anasema kwamba *in my life I didn't see.* Haijawahi kutokea watu wanakuja wanaomba kuchunguza *account,* mimi nina fedha gani kuwashinda watu na mimi *I am openly hard* ninachomshukuru Mwenyezi Mungu kwa kweli naipenda nchi yetu kuliko kitu kingine. *I do all the best to my country* na ninafanya kila kitu pamoja na kwamba nimehujumiwa mambo mengi sihitaji kwa sababu ya muda nimehujumiwa kweli na Serikali hii. Lakini naomba tu nitoe dukuduku kwamba naomba mrudi kwenye imani ya Utanzania. Mnaweza mkahisi kwamba kuna Wapinzani ndiyo wabaya lakini nafikiri humo humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni amrudie Mungu. Kama anaitafutia mema nchi hii

amrudie Mungu na *from today* naomba Mheshimiwa Rais ajaye awe makini sana anapoteua Mawaziri kuna Wizara nyeti, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Nishati na Madini ni asili ya Watanzania na Wizara ya Elimu na Utamaduni, elimu ndiyo asili ya nchi yoyote duniani.

Kuhusu elimu naomba niseme wazi, mimi siogopi kitu kama anayeweza kuniua ni Mwenyezi Mungu sijali, nitakalofanyiwa mfanye, lakini naomba niseme mmrudie Mungu. Mimi ninajitoa siku zote katika maisha yangu napenda sana nchi yangu *I do all the best to my country* na sijawahi kuiibia nchi yangu hata kitu kimoja kama nimekwepa kodi au chochote, basi namwomba Mwenyezi Mungu aniweke pembeni na hata ukija nitakwambia hizi fedha zimekwepa kwa bahati mbaya hizi na ndiyo asili yangu nimezaliwa nifanye kazi. Lakini naomba amrudie Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema kwa hasira kwa sababu mimi nawajibika kama Mtanzania naiokoa jamii yangu na naipenda jamii yangu iwe ya maana ijisikie nimefanya ma-*research* mengi ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu nilimuahidi kwamba nitakuwa tayari hata kuzindua na nimefanya na nitaweza, *why not?* Kama Wazungu wameweza kwa nini nisiweze, nitaweza na nitafanya. Lakini ninachowaomba tunahitaji kuwa na Serikali inayojali binadamu na *especially* mtu anapoifanyia jamii yake mema aonekana anafanya mema. *Don't regard him as a opposition,* unaweza kuwa *opposition* ukawa mzuri tu na ukawa na ndugu ndiyo mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwenye hotuba yetu kwa sababu kuna vitu vingine vinanigonga mpaka rohoni. Nasikitika ndiyo maana naamua kusema wazi, Bunge lako likiamua liamue *I am truth the parliamentarian,* sihitaji hata senti moja kutoka kwenye Bunge, Mungu ameniumba nikiwa sina kitu *and I will live,* nitaishi bila kitu, sihitaji kwamba labda mtu anisaidie nafanya kazi kwa juhudi zangu ambazo Mungu amenijali namshukuru Mungu, naheshimu Waheshimiwa Wabunge wenzangu.

Lakini naomba tuitendee Tanzania mema kama tunaipenda, tusiwe wanafiki wa kujifanya maadamu wewe uko katika Chama fulani unaweza ukawa Chama chochote na ukakimaliza na watu wakakusahau wakadhani kwamba labda ni mwenzao. Maana yake naona hata vibaka siku hizi wanaweka bendera za CCM, lakini unadhani ni mtu mwema, kumbe kaweka bendera.

Mimi ningekuwa mbaya sana nafikiri nisingekaa Upinzani, ningeogopa sana kwamba *anything can happen,* lakini maadam najiamini kama litakuja baya basi ni la ubinadamu. Lakini naomba mnisamehe, nazidi kusema Waziri huyo tumwombee Mungu amrudishe kwenye imani, aipende Tanzania kama kweli ni asili Mtanzania *unless otherwise* kama siyo Mtanzania, maana yake unaweza kujifanya ni Mtanzania kumbe una asili ya nchi nyingine. Halafu unawadanganya watu kwamba wewe ni Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya pamba hairidhishi naomba waliangalie hili, uwiano wa bei ya pamba hauwiani na bei ya halisi. Ukiangalia nguo zetu, leo hii shati langu niliwahi kutoa mfano kwamba hili shati ni kotoni, lakini mimi hata Tanzania hapa

kwa shati kilo moja yaani uzito wa kilo ya mawe na kilo ya manyoya ni ile ile hata ufanyaje. Hii nguo ya kotoni, nikinunua nguo kwenye kilo zinaingia nguo 15 ambazo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kabla sijaanza kutoa mchango wangu nimpongeze Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, naona amehamia eneo au mahali wanapokaa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, ni dalili njema anaweza akarudi katika Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kutoa pole na rambirambi kwa jamaa na marafiki wa marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga na kumwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pili, niwapongeze viongozi wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikweti, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani abeid Karume, wote kuchaguliwa kugombea nafasi za uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hotuba yake ni nzuri ameeleza kwa kinaganaga mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu kwa muda wa miaka 10 amefanya kazi nzuri sana nampongeza kwa dhati. *(Makofi)*

Pili, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, mafanikio hayo ambayo tumeorodheshewa yametokana na umahiri katika uongozi wake na ni matokeo ya uongozi wake uliotukuka, kwa hiyo, nampongeza kabisa kwa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nakiri kabisa kwamba Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya mambo mengi na imepata mafanikio makubwa, kwa hiyo, sina budi kuwapongeza viongozi pamoja na Serikali nzima na safu nzima ya Waheshimiwa Mawaziri kuwa kazi nzuri imetendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya pongezi, ningependa kuainisha maeneo manne ambayo kwa mawazo yangu bado yanahitaji yapewe msukumo wa pekee. Maneno hayo manne ni kama haya yafuatayo:-

Eneo la kwanza nitakalozungumzia ni vita dhidi ya rushwa. Eneo la pili, ni tatizo la njaa Wilayani Ngorongoro, eneo la tatu, ni ulinzi na usalama na eneo la nne ni mishahara ya *VEOs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na eneo la kwanza vita dhidi ya rushwa kama alivyoelezea Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ni kweli mengi yamefanyika, jitihada zimefanyika, ufanisi upo, lakini pamoja na yote hayo bado rushwa ipo. Nafikiri tusingeifumbia macho, tukubali kwamba rushwa ipo na hivyo ni lazima tuendelee kukabiliana nayo.

Kwa maoni yangu inashangaza kidogo kwa sababu kwa kadri tunavyojitahidi kupiga vita rushwa ni kwa kadri hiyo hiyo inaelekea kwamba rushwa inaendelea kushamiri. Kwa wale wenzangu wana-*theology* kuna usemi unaosema kwa kiingereza: *"Religion is like a nail, the harder you hit it, the deeper it goes in the wood."* Tatizo la rushwa katika nchi yetu limekuwa la namna hiyo kwa kadri tunavyopigana nayo ni kwa kadri mizizi inavyoota. Unajiuliza ni kwa nini inakuwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningejaribu kusema kwamba sababu ya rushwa kuendelea kushamiri katika jamii yetu kuna sababu tatu pamoja na sababu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza, mimi naona ni mishahara midogo. Mshahara wa Mtanzania aliyeajiriwa ni kati ya shilingi 60,000/= mpaka 80,000/= kwa mwezi. *(Makofi)*

Sasa wote tunafahamu kwamba shilingi 60,000/= mpaka 80,000/= kwa mwezi unahitaji kula, unahitaji kuvaa, unahitaji matibabu na unahitaji kuwapeleka watoto shule, ni dhahiri kabisa kwamba shilingi 60,000/=, 80,000/= haziwezi kutosha. Sasa kama unakabiliwa na mahitaji ya lazima ya nyumbani ya matibabu, ya kuwasomesha watoto, ya kuwanunulia nguo kwa shilingi 60,000/= au 80,000/= na huwezi ukafanya hivyo. Kwa hiyo, dhahiri kabisa kwamba utashawishika kutafuta kipato mahali pengine na kipato hicho mara nyingi ni rahisi kushawishika kwa kutumia njia ambazo hazikubaliki kisheria, njia za rushwa ili kuongeza kipato chako.

Kwa hiyo, kwenye hali kama hiyo ambapo tunalipa mishahara isiyokidhi mahitaji ya maisha wa kulaumiwa ni nani? Unahitaji kula, unahitaji kusomesha watoto na unahitaji kuwatibu watoto lakini mshahara hautoshi wa kulaumiwa ni nani? Mimi nadhani hapa ni lazima tujaribu kutazama upya viwango vya mishahara tunayolipa watumishi kwa sababu inashawishi watu kupokea rushwa au kupata malipo ya kificho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ya pili ni eneo la kodi au ushuru ulio mkubwa. Pamoja na Serikali yetu kujitahidi kupunguza viwango vya kodi, bado viwango hivyo naona kwamba ni vikubwa na vinashawishi watu kujaribu kukwepa kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi na ushuru bado mimi naona ni kubwa, ni lazima tutafute utaratibu wa kujaribu kupunguza. Kwa sababu tukiendelea na kodi za namna hii na tukiendelea na ushuru mkubwa wa namna hii ni dhahiri kwamba tutawashawishi watu kupokea malipo ya kifichoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ni suala la ukiritimba mkubwa kwenye maeneo na taasisi za kutolea huduma. Kwa mfano, kwenye Vituo vya Polisi, kwenye Vituo vya Afya, kwenye Zahanati na kwenye hospitali. Kwenye vituo hivi ili uweze kupata huduma unashawishika kutoa chochote. Kwa hiyo, kwenye maeneo ya kutoa huduma ni lazima tujaribu kurekebisha ili tuweze kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ambalo napenda kulizungumzia ni tatizo la njaa. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake ameelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu na ameelezea tatizo la njaa ambalo linatokana na uhaba wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye tatizo hili la upungufu wa chakula au la njaa naomba ieleweke kwamba Wilaya ya Ngorongoro ni moja kati ya Wilaya ambayo imekumbwa na tatizo la njaa. Kwa hiyo, naomba katika suala hili la njaa tujaribu kuangalia kwa makini ili watu wasiweze kuathirika na tatizo la njaa au ukosefu wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni eneo la ulinzi na usalama. Naomba kunukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 44 aya 61: "Vyombo vya Ulinzi na Usalama vimeimarishwa kwa kupatiwa zana za kisasa za kufanyia kazi na kujenga mazingira mazuri ya kutekeleza wajibu wao ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo ndani na nje ya nchi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngorongoro kieneo ni moja kati ya Wilaya kubwa nchini. Aidha, Wilaya ya Ngorongoro ni moja kati ya Wilaya iliyokumbwa na tatizo la majangiri ya asili ya Kisomali. Tatu, Wilaya ya Ngorongoro ni Wilaya ambayo kwa sasa inakabiliwa na tatizo la vita vya kikabila. Wilaya ya Ngorongoro inakabiliwa na wizi sugu wa mifugo kutoka majirani zake kutoka Meatu na Bariadi. Kwa njia hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie chombo cha kusafiri kwa *OCD* wa Wilaya ya Ngorongoro ili tuweze kukabiliana na matatizo hayo sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni mishahara kwa ajili ya *VEO* wa Wilaya ya Ngorongoro. Kwa muda wa miezi minane *VEO's* wa Wilaya Ngorongoro hawajalipwa mishahara na naomba kunukuu moja ya barua waliyoniandikia: "Sisi Watendaji wa Vijiji wa Wilaya ya Ngorongoro hatujalipwa mishahara kwa miezi nane hivyo tunakuomba kwa kuwa wewe ni kiongozi wetu ujitahidi kulishughulikia kwa kikamilifu ili tuweze kupata malipo yetu tunayoidai Serikali. Tumekuwa tukifanya kazi bila malipo kinyume na taratibu za haki za kibinadamu." Kwa hiyo, tafadhali naomba hao *VEO's* wa Wilaya ya Ngorongoro washughulikiwe, waweze kupata malipo yao ili wafanye kazi walioajiriwa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri ambao wako kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu ambao wamemsaidia Waziri Mkuu kufanikisha kuleta hoja yao hapa Bungeni. Lakini bila ya kumsahau Katibu Mkuu na bila kuwasahau Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Ma-*DAS* na Ma-*RAS* kwani hao ni sehemu ya Ofisi ya Waziri Mkuu wanaomsaidia kufanya kazi zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri Mkuu kwa mambo mengi tu. Waziri Mkuu amevunja rekodi ya kuwa Waziri Mkuu kwa miaka 10. Mimi toka nimezaliwa sijawahi kusikia Waziri Mkuu amekaa miaka 10 madarakani, hii ni mara ya kwanza kusikia katika Tanzania. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa hilo kwani ameonyesha kwamba Watanzania walikuwa na imani naye na pia Rais Benjamin Mkapa alikuwa na imani na Waziri Mkuu wake katika utendaji kazi wake. *(Makofi)*

Nampongeza si kwa sababu ni rafiki yangu na si kwa sababu nimefanya kazi naye tu, hapana. Ila nampongeza kwa sababu pia najua tabia yake ya ufanyaji kazi wake alivyokuwa Wizara ya Kilimo alikuwa anafanya kazi hata Jumapili anarudi hata usiku kufanya kazi katika Ofisi yake. Kumbe Serikali ilikuwa inamwangalia na ndiyo maana ikadiriki kumpa madaraka ya Uwaziri Mkuu kwa muda mrefu. Waziri Mkuu nimefanya naye kazi kwa kipindi kirefu tu si kwamba nimemfahamu Bungeni hapa, hapana. Kwa hiyo, nasema hayo kwa sababu namfahamu vizuri. Nampongeza sana kwa kuvunja rekodi ya kuwa Waziri Mkuu kwa miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nije kwa Vyama vya Siasa nchini. Hivi karibuni tunategemea kufanya uchaguzi na kadri siku zinavyokwenda kunakuwa na maneno mengi ya hapa na pale. Vyama vyote vimekuwa vikitoa lugha za kuhamasisha wanachama wao kwa ajili ya kushinda katika uchaguzi unaokuja, lakini wengine walikuwa wakitoa lugha za ushari kidogo ambazo mimi nina wasi wasi nazo kidogo kwa wananchi wetu wanaotegemewa kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijafurahishwa hata kidogo na lugha zinazotolewa kwenye majukwaa ya siasa. Kuashiria uhasama ndani ya nchi yetu hata tunapokuwa kwenye uchaguzi kumenitia wasi wasi sana. Mimi nina wasi wasi kwamba hawa wanaotoa lugha za vitisho na vitu kama hivyo hawajaona vita ndani ya nchi zao. Mimi nimepigana vita katika nchi tofauti, watu hawajui lakini mimi nimeshiriki vita vya Uganda, Shelisheli na Msumbiji nimeshiriki kulikomboa Bara la Afrika. Watu wasituone tumekaa hapa kimya kimya wasifikiri wajinga, hapana sio wajinga tunajua tunafanya nini. Sasa kama kuna watu ambao hawajajua maana na athari ya vita wasiseme lugha za ajabu ajabu majukwaani. Tusionyeshane vidole, mtu akikosea aitwe aonywe. Tunakwenda katika uchaguzi ambao ni hatari. Vijana wengi wanashabikia lugha zile za ushari, hawajui athari yake watakaoumia ni vijana hao hao, sisi wakubwa tutajificha nchi mbalimbali tutawaacha wanaumia wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kwa sababu hili naona linakwenda, halipoi linachemka zaidi. Lakini nawaambia vijana kwamba viongozi ambao wanatamka lugha za ushari, wanaozungumza lugha za kumwaga damu vijana wasiwaunge mkono

kwa sababu najua athari yake ni kubwa. Athari yake ni kubwa tena kubwa mno. Tutaua wazee wetu, dada zetu, mama zetu ambao hawajui pa kukimbilia ni wapi. Nchi yetu ni ya amani, tuendelee kuwa na amani. Sijapendezewa katika hili nasema nchi yetu ni amani tuendelee kuwa na amani. Uchaguzi unaokuja kama una kasoro tuzirekebishe kasoro hizo mapema lakini tusiashirie kumwaga damu katika nchi yetu hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kupigana hakuna atakayetusimamisha. Mimi nasema hakuna atakayesimamisha vita hii itadumu mpaka miaka 100 inayokuja kwa sababu Watanzania watakuwa hawajui maana ya kupigana sasa watakuwa wanajifunza na wataingia na watu ambao sio nchi yao kwa kushabikia ili tuendelee kupigana ili amani yetu itoweke. Mimi nasema viashirio hivyo viondoke. Tuviondoe mapema kama kuna kasoro za uchaguzi tuziondoe mapema tuachane na shari za majukwaani za kutishia kumwaga damu na nchi hii sio ya kumwaga damu hata kidogo. Tumetumikia nchi hii kwa muda mrefu, tumepigana vita kuikomboa nchi hii iwe na amani, leo hii tunaashiria kupigana vita vya kutoka wapi na nani anasema vitu kama hivyo. Nasisitiza kwamba tuendelee kurekebisha kasoro zetu lakini tusiashirie kupigana vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Siasa hasa vya upande wangu wa Upinzani tumekuwa tukilalamika kwamba Serikali haifanyi vizuri. Ni kweli kuna maeneo ambayo Serikali haifanyi vizuri. Lakini Serikali hii haiwezi kufanya kila jambo mimi nasema toka nimekuwa katika Kamati ya Ulinzi na Usalama nimetembea karibu nchi yote na nimejionea nchi yetu ilivyo kubwa. Kwa hiyo, kwa kipindi cha miaka 40 kufanya maajabu sidhani kama tunaweza kufikia. Mimi nadhani tungefikia miaka labda 70 au 80 tungeweza kulalamika zaidi. Nchi yetu ni kubwa na ina maeneo makubwa mno kiasi ambacho hatuwezi kufanya maendeleo makubwa zaidi kwa kiwango ambacho nakiona mimi nadhani Serikali imejitahidi kwa kiasi chake. Serikali ilipokuwa inalalamikiwa na Upinzani ilikuwa inafanya, mimi nina kumbukumbu nyingi tu. Yale ambayo ilikuwa haifanyi ni pale ambapo Serikali haikuwa na uwezo. Lakini kwa kuwa Serikali sasa inaanza kukusanya makusanyo mengi, tumeona kabisa matarajio ya maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nilikuwa nawashauri wenzangu Vyama vya Upinzani kwamba tunapotaka kufanya shughuli za maendeleo katika nchi yetu tusibague na kuisusia CCM kwa sababu CCM wanapofanya wao wanaonekana wanafanya wao. Lakini tunapotakiwa kufanya shughuli za maendeleo Wapinzani tumekuwa wakaidi kwenda kwenye shughuli zile. Nimekuwa nikizungumza mara nyingi mpaka wakaniambia mimi ni CCM B, sio CCM B nazungumza *openly* na vitu ambavyo vipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mtu uliyekwenda shule unajua unachokifanya kitu gani. Huwezi ukabishana bishana tu kwa sababu unabishana. Mimi nadhani ninachozungumza ni kitu ambacho kipo. Watanzania unapokuwa umeshashika Katiba ya nchi yetu lazima ushiriki kwenye shughuli za maendeleo. Sasa unashika Katiba ya nini kama unashindwa kushirikiana na chama. Tumesema Chama cha Mapinduzi kimeshinda, tumekubaliana nao na kama tungepinga tungekaa basi nje tukapinga Serikali. Lakini

tumekubali Serikali kwamba Chama cha Mapinduzi kimeshinda kwa maana hiyo tulitakiwa tushirikiane na Chama cha Mapinduzi kubadilisha maendeleo ambayo tunayadai. Lakini tunacholalamika huku hatushiriki kwenye shughuli za maendeleo. Mimi naona tunakwenda tofauti.

Mimi nasema tusipoteze uelekeo, Vyama vya Upinzani vina kazi nzuri na vina kazi nyepesi ya kuishauri Serikali iliyoko madarakani pale inapokosea, sio kulaumu tu. Tusilaumu, twende kwenye utaratibu ambao nadhani kama tunafanya kazi tufanye kazi kwa kuishauri Serikali ili ifanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye daftari la wapiga kura. Mimi naishukuru sana Serikali kwa kusikia kilio cha Wapinzani kwamba daftari la wapiga kura linaweza likasaidia katika kuondoa malalamiko ya wapiga kura. Naipongeza kwa sababu malalamiko tuliyoyasema ndiyo yametekelezwa sasa. Serikali inapotekeleza tuungane nao basi mkono. Tujenge hoja za msingi pale inapokosea na kuisaidia Serikali. Maana yake kuwepo Vyama vya Upinzani kwa sababu ya kurekebisha yale ambayo Serikali tunadhani haioni. Sasa daftari ya wapiga kura lililalamikiwa kwa muda mrefu, leo hii limekuwepo na Watanzania wengi wamejitokeza kujiandikisha kuwania kupiga kura hivi karibuni. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa hilo kwa sababu hiyo itapunguza malalamiko ya wizi wa kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia baada ya hapo mimi niiombe Serikali kwamba Tume ya Uchaguzi, ni ushauri wangu tu ili kuondokana na mambo ambayo naona kama yataashiria umwagaji damu katika nchi yetu au fujo. Ushauri wangu kwenye Tume ya Uchaguzi, ningeshauri kwamba ikiwezekana kama nafasi tunayo wawepo na Wapinzani katika Tume ya Uchaguzi ili tuone jinsi ambavyo tunaweza kushirikiana. Maana yake naamini kwamba ushindani ni mkubwa lakini anayejiona atashinda, atashinda tu kutokana na daftari litakapokuwepo. Kwa hiyo, nashauri kwamba ikiwezekana Tume ya Uchaguzi Wapinzani pia wawepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala hasa katika jimbo langu la Kigamboni. Waziri Mkuu amesema mambo mengi aliyotekeleza katika kipindi cha miaka 10, nakubaliana nayo na mengi tumeyaona yametekelezwa likiwemo shule na maeneo kadhaa. Lakini katika jimbo langu...

**MBUNGE FULANI:** Lipi?

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Jimbo langu la Kigamboni. Mimi mpaka mwezi wa kumi ndio nakoma Ubunge wangu. Kama ulikuwa hujajua, nakueleza mpaka mwezi wa kumi bado ni Mbunge wa jimbo lile mpaka aje Mbunge mwingine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigamboni kuna matatizo katika maeneo tofauti kidogo. Kuna matatizo ya umeme. Maeneo ambayo nayazungumza ni maeneo ya Tuangoma, Kibada, Kimbiji, *Kisarawe Two* na maeneo kadhaa. Maeneo hayo ndiyo maeneo ambayo watalii wengi wanakwenda siku za *weekend,* lakini hakuna umeme na

wenye mahoteli wanatumia majenereta, wanatumia gharama kubwa sana kuwatoza watu ambao wanakuja kupumzika kule. Kigamboni yaani ukienda *weekend* hupati nafasi mpaka ufanye *booking* ya wiki moja kwenye hoteli za Kigamboni. Kwa sababu *beach* ya Kigamboni ni nzuri na imekuwa safi na watu wanapata huduma zote. Tatizo kubwa ni umeme maeneo yale. Kwa hiyo, namwomba Waziri Mkuu suala hili nimeshazungumza hata juzi kwamba sio suala la umeme tu lakini pia waangalie suala la Kivuko. Hatuna sababu ya kuendelea na Kivuko cha miaka 100 iliyopita kinahatarisha usalama wa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishashauri siku nyingi kwamba ni vizuri Waziri Mkuu mwenyewe anafahamu nimeshawahi kuongea naye kwamba ni vizuri tukajenga daraja kwa sababu vivuko vinatumia fedha nyingi kwenye *service* yake. Tungejenga daraja nadhani ingetupunguzia sana matatizo ambayo wanayapata watu sasa hivi. Kivuko kimekuwa cha wasiwasi. Leo kimekuwa kizima, kesho kimekuwa kibovu na saa nyingine kinapoteza mwelekeo. Si salama hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara ya kutoka Mji Mwema mpaka Kimbiji sio nzuri. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili alichukulie kwa uzito wake kwamba maeneo ambayo tunadhani yanaleta uchumi zaidi basi tuyawekee maanani, tuwekee uzito kuhakikisha tunarekebisha matatizo yao ili wananchi wale wafaidike na maeneo yao kwa sababu uchumi ule unatoka kwenye maeneo yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwapongeza *NCCR-Mageuzi.* Leo *NCCR-Mageuzi* wamefanya Mkutano wao Mkuu na nilikuwa naangalia nafuatilia kwenye *TV* wamemchagua Mheshimiwa Bwana Mvungi, kama mgombea Urais kwa kushika maendeleo ya *NCCR-Mageuzi* kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, Bwana Mvungi amekuwa mgombea wa *NCCR-Mageuzi* kwa tiketi ya *NCCR-Mageuzi.* Kwa hiyo, nawapongeza pia kwa utaratibu waliotumia leo utaratibu ni mzuri mno wa uwazi, mtu unafurahi kwamba sisi tunafanya nini. Kwa hiyo, naomba sana kuwapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la kuondoa umaskini. Ili kuondoa umaskini Mabenki yetu yana matatizo. Unapokwenda kuomba mkopo unaweza kuomba mkopo leo unachukua miezi saba ndipo unapata mkopo ule hata kama ulikuwa na *plan* ya kufanya biashara ile biashara inakuwa huwezi kuifanya kwa sababu tayari biashara ile unaomba, leo, kesho unaomba ile biashara uliyopanga kuifanya ufanikishe shughuli zile. Hiyo inaleta matatizo kwa umaskini ambao tunataka kuuondoa, hatuwezi kuuondoa katika misingi hiyo. Kwa hiyo, ni vizuri umaskini kama tunataka kuuondoa Mabenki yetu yaondoe urasimu huo, watoe mkopo kwa urahisi na pia wapunguze riba ya mikopo kwa wakulima na wananchi wetu. Vinginevyo tutakuwa tunazungumza umaskini nchi za wenzetu wanatumia mikopo katika maendeleo yao na kujiendeleza na wananchi wao hawatumia fedha zao za mfukoni hata siku moja. Sasa hatuwezi kusema tutafute fedha halafu twende kwenye mikopo hatuwezi. Kwa hiyo, naomba Mabenki waangalie utaratibu na waangalie jinsi ya kupunguza riba ili wananchi wa Tanzania wafaidike na Mabenki ya nchi yetu ambayo sasa yamekuwa mengi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza kwa ujumla kwa mambo mengi lakini nampongeza Waziri Mkuu na kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia moja kwamba bajeti ya Waziri Mkuu ni mwelekeo mzuri wa uchumi na maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima tukubaliane kwamba tumefanya ukweli tuunge mkono. Lakini kama kuna jambo la msingi tunakataa kwa sababu ni wajibu wetu. Bungeni hapa hatukuja kupoteza muda, tumekuja kufanya kazi ambayo wananchi wametutuma, lakini yale ambayo tunadhani ni mazuri tuyaseme na yale ambayo ni mabaya tuyaseme. Tusiseme tu mradi tunasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Kilombero kwa kupotelewa na Mbunge wao. Lakini vile vile nichukue nafasi kuwapongeza wale wote waliopata mafanikio katika chaguzi mbalimbali na walioteuliwa na vyama vyao kuwania nafasi ya juu katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa kusema jambo moja lililoulizwa hapa na Mheshimiwa mmoja kwamba kwa nini tunakubali halafu baadaye tunaanza kukataa. Niseme wazi kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kile kilichoulizwa hapa kwamba naunga mkono nini baadaye naanza kubishana.

Kimsingi sio kubishana tuko hapa kujenga mawazo, tuko hapa kuleta hoja Serikalini zifanyiwe kazi na sio kubishana. Kwa hiyo, ninachounga mkono ni yale mazuri yaliyozungumzwa na nabaki na uhuru wangu kwa kutoa mawazo yangu katika kujaribu kuweka mambo vizuri zaidi katika uendeshaji wa Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa mambo mengi mazuri yaliyofanyika katika kipindi hiki cha miaka 10. Yamefanyika mengi sana na hata nashangaa inapotokea watu wanaanza kubisha na kukebehi na kutokuona kinachofanyika.

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji alitoa sentensi nzuri sana kuelezea na nilitegemea kwamba hili lingeeleweka na watu wengi iliyokuwa ikitafsiri maendeleo. Maendeleo alisema sio tukio la kutokea siku moja kama moto unavyoweza kuwaka ikaonekana moto umewaka na basi umewaka imekwisha. Lakini bahati mbaya wenzetu bado hawaelewi kwamba maendeleo ni mchakato mrefu na inashangaza sana kwa wenzetu wachache kutaka kulinganisha miaka 45 ya nchi yetu na Mataifa ambayo yana Uhuru kwa miaka mingi sana. Sijui wanasoma historia au hawasomi, huwezi ukalinganisha nchi yetu changa na nchi zilizoendelea Ma-*giant* ukataka kuona kwamba ndani ya miaka hii tuwe tumeshayafanya hayo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyofanyika ni mengi sana kwa hali tuliyonayo. Kwa kweli katika maeneo mengine mengi naipongeza Serikali kwamba tumefanya zaidi hata mahitaji ya wananchi. Tumefanya zaidi katika baadhi ya maeneo. Nichukue nafasi hii kwa mfano kuipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano. Katika eneo hili kwenye jimbo langu mathalini kila eneo la kijiji simu zinazungumza. Sasa walitaka tufanye nini zaidi ya hicho. Tumefanya zaidi tunachohangaikia sasa ni sisi wananchi tuwe na simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaongea sana na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, nilipoanza Ubunge mwaka 2000 kuhusu mji unaoitwa Isaka ambapo kuna hii tuliyoita bandari kavu. Pale kulikuwa na njia kama 30 za simu mwaka 2000 nilipochaguliwa kuja Bungeni. Lakini Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Serikali kwa ujumla wamefanya kazi, wameongeza njia pale za simu kiasi kwamba wananchi waliopo pale hata hawazitumii pale tena ziko pale *idle* tumefanya zaidi sasa kwa nini tusikubali na kupongeza. Tunakubali na kupongeza ndugu zangu kwa sababu hizo. Katika eneo la Shule za Msingi zilivyokuwa mwaka 2000 zilikuwa na hali ngumu, lakini leo nenda vijijini utastukia kwenye pori unakuta shule nzuri sawa na ile ya Dar es Salaam na ile ya Dodoma lakini iko kijijini kwangu kule Msalala. Sasa kwa nini tusikubali na kuunga mkono hoja hizi. Maendeleo makubwa yamefanyika. Tunachokitoa hapa na kuzungumza ni kuishauri Serikali ili tuendelee kuboresha na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo na mimi nataka nichangie mawazo yangu katika eneo moja tu kwa leo. Eneo hili ni katika eneo la mapato. Zinajitokeza tofauti kubwa katika mapato. Alipokuwa akizungumza Mheshimiwa Paul Makolo hapa asubuhi leo alionyesha kwa takwimu katika kile kitabu cha Mpango wa Maendeleo ukurasa wa 54 sipendi kuyarejea yale yote aliyoyazungumza. Tulikuwa tunazungumzia sana kwamba tujaribu kutengeneza utaratibu mzuri ambapo *share* ya mapato ya nchi hii itasambazwa sawa sawa kadri ya mahitaji na hata tukafikia na tulishakubaliana kuanzisha kile kitu tunachokiita *Tanzania Assistance Strategy.* Tulikubaliana katika hii kwamba misaada yote inayopatikana inawekwa mahali pamoja na inasambazwa sawa sawa. Kama si sawa sawa angalau katika ile inayoitwa sawa sawa na mahitaji ya watu walioko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kuna mikoa ambayo bado tunalalamikia hata umeme haujawahi kufika Mkoa wa Kigoma kwa mfano.

Tumejitahidi katika fedha za ndani nazungumzia katika ule ukurasa wa 54 utakuta inasomeka 400, 500, 600 milioni sawa sawa ila Mkoa wa Manyara umepata fedha nyingi zaidi na hiyo ina *justification* zake hapa kwamba ni mkoa mpya unahitaji kujenga majengo na vitu vingine, miundombinu inayohitajika kuendesha mkoa. Katika safu hiyo katika ile *column* ya fedha za ndani inaonekana kwamba mgao unakwenda vizuri . Ukija kwenye hizi fedha za nje ambazo ndizo tumeziundia hata hiyo *TAS* mambo yako ambavyo kwa kweli siwezi kuelewa na sijui labda itahitajika tupatiwe semina tuelewe inakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishakubaliana kwamba hii *Tanzania Assistance Strategy* itajaribu kuratibu usambazaji wa hizi fedha zinazotoka nje. Lakini unakuta Kigoma 0, Rukwa 0, Tabora 0, Shinyanga sijui milioni ngapi chache, kwa nini? Hapa ukisema kwamba labda imezingatiwa kitu ambacho kwa kizungu wanaita *equity* kwa maana kwamba unagawa sawa sawa na mahitaji, Kigoma wana mahitaji zaidi nafikiri na hata Shinyanga wana mahitaji zaidi nafikiri. Ukilinganisha na mikoa mingine ambayo imepatiwa zaidi sitaki kuitaja hapa. Ningependa sana tujaribu kuliangalia hili kwa makini. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taja!

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nije pia katika eneo hilo hilo kwa upande wa Watumishi wa Serikali. Tofauti ya mapato inakuwa kubwa. Naipongeza Serikali kwa takwimu tulizozipata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba mwaka 1995 tulikuwa na kima cha chini cha mshahara shilingi 17,500/=, tumepanda mpaka kufika kiasi cha shilingi 60,000/= kwa mwezi. Takwimu zinaonekana kwamba kwa kweli kuna ongezeko. Namba zinaonyesha kwamba tumekwenda kiasi kikubwa, lakini hali halisi kasi ya kupanda kwa mapato ya wafanyakazi hawa hasa wa ngazi za chini inaonekana kasi ni ndogo kuliko kasi ya matumizi. Kasi ya kupanda kwa mapato ya halali ni ndogo kuliko kasi ya kupanda kwa matumizi ya lazima. Mheshimiwa Mathew Ole Timan amezungumza hapa kwamba pengine ni kichocheo cha rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalo ni tatizo sasa hivi, *gap* kati ya mshahara wanaopata kipato cha chini na wale wanaopata kipato cha juu ni kubwa mno. Hili limekuwa likibarikiwa kwa kujaribu hata kutengeneza hizi *agencies,* sasa watu walioko katika Serikali wanajaribu kukimbilia katika *agencies,* wanatafuta kazi, wanaomba kazi kwenye *agency* ili wahame kwenye hizi zinazoitwa Idara za kawaida. Kwa sababu kule kuna mishahara mikubwa zaidi. Lakini masoko tunayonunua bidhaa yule anayepata shilingi 60,000/= kwa mwezi na anayepata shilingi milioni tatu ni masoko yale yale na bei ni zile zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya utafiti wa migogoro mbalimbali inayotokea duniani pamoja na sababu zingine nyingi za migogoro lakini suala la tofauti ya kipato chenyewe ni miongoni mwa misingi ya migogoro inayotokea. Tumefika mahali tusianze kuaminiana tunaanza kuangaliana kwa vijicho. Tunasali hapa asubuhi Mheshimiwa Spika, akituongoza kwamba tusitazamane kwa majicho ya husuda tukianza kutazamana kwa macho ya husuda fulani anapata zaidi kuliko mimi na kinachotokea hapo ni nini? Nitoe mfano mdogo kuna jamii zingine katika nchi hii mfano mdogo tu. Ukienda kwenye jamii hizo kuna watu waliosoma na wana uwezo wa kujenga nyumba nzuri kwenye vijiji vyao lakini hawajengi kwa sababu gani. Utakuta akijenga nyumba wenzake wanamwangalia kwa kijicho na kijicho kibaya zaidi hatuamini wanamloga. Sasa hii tutaanza kuangaliana kwa mtindo huo haifai. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nishauri tu kwa Serikali kwamba ilichokifanya sio kidogo, ni kikubwa. Pengine inajaribu kujitahidi hakuna anayechukia kwamba mtu

apate fedha zaidi au apate mapato zaidi. Mheshimiwa Waziri Mkuu angefurahi kila mtumishi apate mshahara mzuri zaidi. Mheshimiwa Rais angefurahi wafanyakazi wetu wapate mshahara mzuri zaidi, lakini hizo fedha kwa kweli hazipo, pengine tunakubaliana katika hilo. Lakini pengine tungeweza kujaribu kufanya ubunifu.

Mimi naomba nitoe mawazo yangu yaingie Serikalini kwa rekodi. Kwa mfano, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha jedwali namba moja lilijaribu kuchanganua viwango vinavyopendekezwa kwa ajili ya kodi hizi za mapato. Tukasema kwamba kuanzia shilingi 0 mpaka shilingi 80,000 hawa hawatatozwa kodi ya mapato. Halafu unakwenda kuanzia shilingi 80,000 mpaka 180,000/= watatozwa asilimia 18.5 zinazozidi kwenye shilingi 80,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa napendekeza kwamba labda Serikali iangalie uwezekano kwamba ifike angalau kutoka shilingi 0 mpaka shilingi 180,000 zisitozwe kodi. Hii najaribu kuijengea hoja kwa mazingira kwamba hivi Vyama vya Wafanyakazi walijaribu kukokotoa na kuona kwamba mfanyakazi angalau kwa kima cha chini apate shilingi ngapi walipendekeza nadhani mwaka jana au mwaka juzi iwe kama shilingi 175,000 ndipo ambapo angeweza kukidhi mahitaji ya lazima tu sio ya *luxury.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi napendekeza kwamba pengine kutoka shilingi 0 mpaka shilingi 180,000 ndiyo isamehewe kodi. Sasa hiyo *gap* inayopatikana hapo ifanyejwe na itazibwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwa nia njema. Kuanzia hiyo shilingi 180,000 na shilingi moja ipandishiwe kodi kidogo. Kwa sababu hawa ni watu ambao si wengi sana. Mimi kwa mfano kwenye jimbo langu sidhani kama kuna mtu analipwa zaidi ya shilingi 180,000. Watumishi wa Serikali walioko huko vijijini kwangu ni walimu, wauguzi, waganga na Ma-*VEO* wetu, wa-*WEO* wetu ambao sidhani kama wanafika huko kote. Tutakuwa tumesaidia watu wengi katika kujaribu kujikwamua kimaisha.

Hii tutaifidia kwetu sisi ambao tuko kwenye *agencies* hizi, kwa mfano, utapandisha kodi kutoka hiyo asilimia 20 iliyopendekezwa kwenye mshahara wa zaidi ya 180,000 uende asilimia 25, halafu wale kuanzia 360,000 kwenda mpaka 540,000 iende asilimia 30, halafu wanaonzia 540,000 kwenda juu zaidi kodi iwe asilimia 35 badala ya 30. Hii itaziba *gap* litakalopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunazingatia na sidharau kwamba kweli watu walisoma miaka mingi shuleni, walipwe sawa sawa na walivyoumia na mimi nimesoma lakini basi na ile huruma iwepo kwa wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote nataka na mimi niungane na wenzangu ambao wamenitangulia kumpongeza kwa jinsi alivyoiwasilisha taarifa yake

ya miaka kumi kwa ufasaha, kwa uzuri na nawapongeza watalaam wake ambao wamemsaidia, wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ana moyo wa usikivu, kwa sababu tukiwa hapa Bungeni, nimewahi kumwambia kwamba wananchi wa Mkoa wa Mtwara wanahitaji aende akaone maendeleo yao na alijitahidi kufanya hivyo. Kwa hiyo, hicho ni kigezo kwamba kwa kweli alikuwa anajali na kusikiliza mawaidha ya Wabunge na kujali matatizo ya wananchi pia. Kwa hiyo, namtakia kila la kheri katika siku zake za baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Abu Kiwanga, ambaye ni Mbunge mwenzetu amefariki hivi karibuni na Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Hiki ni kipindi changu cha kwanza kuwa Mbunge, lakini nataka niishukuru Serikali kwa dhati kabisa wamekuwa wakinivumilia, ninapokuwa na shida ya kumwona Spika, anakuwa tayari kunisikiliza pamoja na watendaji wake, hata huyu Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka ambaye amekuja juzi, unamwambia shida na anakusikiliza. Kwa hiyo, mimi nawapongeza na nawatakia kila la kheri na waendelee kwa moyo huo, hata kipindi kinachokuja wawasaidie na Wabunge wengine sawa sawa na walivyoweza kutuhudumia sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwapongeze wanawake wa Mkoa wa Mtwara kwa jinsi walivyoitikia wito wa kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura. Ninalosisitiza kwao pamoja na wanawake wa nchi nzima, wajitokeze sasa kwenda kupiga kura siku ya uchaguzi na wakipigie kura Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Benjamin Mkapa kwa jinsi alivyofanya kazi kwa kipindi hiki, sisi sote ni mashahidi kwamba alikuwa anaumwa, lakini alipotoka hospitali alitembea na mkongojo kutekeleza ratiba yake aliyoipanga, ile ni kuonyesha uhodari au upendo kwa kuwajali wananchi wake. Hakukubali kulala, kwa hiyo, naendelea kumpongeza, ametenda mengi makuu, Mungu ambariki na atamlipa kwa yale aliyotenda maana alikuwa anajitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana katika Kambi ya Upinzani, Kiongozi wa Upinzani Bungeni ametoa taarifa. Kwenye ukurasa ule wa mwisho amesema, usipande gari la wazee, gari la kizee kwa maana ya CCM, wananchi wasiipande eti ni la kizee. Kwa hiyo, sijisikii na mimi kutokumjibu, ninachosema ni kwamba, wewe kama ni abiria unasafiri unatoka Dodoma unakwenda Dar es Salaam, unapotoka ndani ya nyumba unakuta magari mawili yamejipanga. Gari moja wamebandika karatasi wameandika *learner* na gari nyingine wameandika dereva mzoefu. Abiria mwenye mawazo, mwenye akili timamu hata panda gari ya *learner,* atakwenda kupanda gari ya dereva mzoefu. Ili aweze kusafiri na afike kwa usalama Dar es Salaam. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo wananchi wala msidanyike, mimi nasema wote pandeni gari ya dereva mzoefu ambalo ni CCM itakayo wapeleka vizuri hadi mnafika mnako kusudia kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mlolongo wa malalamiko yangu, mojawapo ambalo nataka nikiri hapa kwa kipindi chote cha miaka mitano, nimewahi kusema mara tatu. Nilikuwa naiambia Serikali kwamba geuza meza sasa angalia Kusini, hii nimesema zaidi ya mara tatu mwenyewe nakiri na kidogo nipongeza kidogo Serikali kwa hilo ila sikuelewa. Kwa sababu baada ya kutangaza Bajeti ya mwaka jana nilisema, geuza meza sasa, angalia maendeleo Mikoa ya Kusini ambayo tuko nyuma. Kumekuja na zoezi hilo la kwanza ambalo nimesema la uandikishaji ambalo mimi sikuelewa, kwa nini walianzia Mkoa wa Mtwara. Halafu la pili katika kugeuza meza, wamekuja kufanya zoezi la kuwazika wanajeshi wale ambao walikuwa mstari wa mbele kivita kule Msumbiji, hilo nalo sikuelewa. Halafu la tatu wamekuja kufanya sherehe ya sikukuu ya Maji na wakati Mtwara kuna tatizo la maji hata hivi ninavyoongea kuna tatizo la maji, mimi sikuelewa kwa nini sherehe ile ilikuja kufanyika Mtwara. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha Bajeti humu humu ndani, Waziri Mkuu nashukuru upo, mwenyewe ulipokuja kwenye ziara uliona misururu ya wananchi na nilisema hilo. Ukaahidi kwamba utamtuma Waziri wa Maji atakuja. Waziri wa Maji alipokuja, nini kimefanyika mpaka sasa hivi? Nataka nikuthibitishie kwamba katika Wilaya zote Mtwara Vijijini, Tandahimba, Newala, Masasi kwenyewe zile Kata bado zina matatizo ya maji. Sasa kuja kutuwekea sikukuu ya kusheherekea maji mna maana gani, wakati maji inajulikana ni Mikoa gani wanapata maji saa 24. Sasa hilo ndilo nimesema nitashukuru kidogo. Niliwaona akinamama walipita pita kuuza biashara ndogo ndogo, kwa sababu ilikuwa ni sikukuu ya Kitaifa hilo nashukuru. Lakini katika haya niliyosema, mimi mmenichanganya wala sikuelewa kitu. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naongea hivyo kuhusu suala la maji. Maji ni uhai, maji ni uzima. Serikali hii iliyoko madarakani ina mipango na imeandika kwenye Bajeti yake kwamba watachukua maji Mwanza watapeleka Shinyanga, ni maili ngapi kutoka Mwanza mpaka Shinyanga? Tunavyozungumza na sisi tuna vyanzo vyetu ndani ya Mkoa, kuna chanzo cha Mitema kiko Kitangari, ambacho kinaweza kikalisha Wilaya mbili na kuna chanzo cha Mkunya ambacho kinaweza kikakarabatiwa wakaleta maji yakasaidia wananchi wengine. Lakini unasema Halmashauri yenyewe iende ikafanye kazi. Halmashauri haiwezi, haina uwezo, haina kipato na kwa sababu Serikali hii ni ya wote na suala la maji ni muhimu sana kuona kwamba wananchi wanapata maji. Kama iliwezekana Mwanza itashindwaje kufanya Mtwara? Kwa hiyo, Serikali ilete maji kwa kadiri itakavyoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo katika Bajeti yetu imelenga sana watu wakubwa, wenye kipato kikubwa. Mimi naishauri Serikali iangalie na wale wakulima wadogo wadogo ambao hasa hasa ni wanawake, wale walioko vijijini. Tuwasaidie mikopo, kuwapatia fedha na ndiyo wazalishaji waliopo ambao ni wengi ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana niliuliza swali kuhusu ni kwa jinsi gani Serikali inakubali uingizwaji wa bidhaa nyingi kutoka nchi za nje yakiwemo matunda na *juice,* wakati ndani ya nchi yetu tuna mazao ambayo tunazalisha wenyewe na yangeweza kuwasaidia wananchi kujikwamua kimaisha na wakati huo huo kuwasaidia wapate fedha

za ndani na wapate fedha za nje. Lakini wanasema tuko mbioni, tunafanya mikakati. Hii mbioni na mikakati mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishauri Serikali kwamba kipindi hiki nilichozungumza, kipengele hiki nilichokizungumzia, ni muhimu kwa sababu walio wengi ni hawa ambao tunawaacha bila kuwasaidia na nadhani mmesikia. Naongea kwa kifupi kwa sababu na muda naona unakimbia.

Sasa niingie kwenye kilio cha watu wa Mkoa wa Mtwara, kwanza ni ile barabara ya Kibiti - Lindi. Wananchi wanalala njiani, gari zinakwama, muda wa wiki mbili, wiki moja na niliuliza swali humu Bungeni wiki iliyopita nikasema hivi, je, Serikali kwa nini haioni kuweka mafungu ya kuwasaidia hawa watu ambao wanakwama, kuwalipa fidia, kwa sababu hawalali kwa hiari yao. Ni Serikali yenyewe ambayo haitengenezi ile barabara na nataka nikwambie wale wanaolala pale, sio kwamba wanakuja huku kutembea Dar es Salaam, wanakuja na shida tofauti. Wengine wanakuja na wagonjwa, maana Mtwara hakuna Hospitali ya Rufaa, Rufaa iko Muhimbili na inawezekana wengine tunawapoteza njiani. Mwingine anakuja kufuata bidhaa lakini bado analala pale. Kwa bahati mbaya sana kuna jamaa mmoja aliniambia kuna kichaa mmoja aliandika kwenye gazeti eti watu wa Kusini wasisafiri wakati wa masika. Hivi ni akili hiyo kweli? *(Makofi/ Kicheko).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wasisafiri? Na wakati wanakuja kufuata mahitaji na mfano hai ni ile siku ya tarehe 16/12/2004, abiria wengi walizidi katika ile meli. Ni kweli tunaangalia upande mmoja kwamba yule mwenye meli labda alizidisha watu. Lakini si kweli, ni wale wananchi na wenyewe walichangia, lakini hawakufanya makusudi ni kutokana na wasafiri na nini kufika Mtwara? Hilo Serikali tumekuwa tunaiambia kwamba, hakikisheni mnatafuta usafiri wa uhakika unaotoka Dar es Salaam kwenda Mtwara, wananchi msiwanyime raha na wenyewe wajisikie raha na wanyewe wako huru wako katika nchi yao. *(Makofi)*

Barabara kutoka Mtwara inapita Mtwara Vijijini, Tandahimba, Newala mpaka Masasi, mimi nakataa hapa. Suala la kutuambia kwamba wanatengeneza sehemu korofi, wanatengeneza sehemu korofi mpaka lini na ile ni barabara ya Mkoa. Kwa sababu inapita katikati ya Wilaya na Waziri Mkuu mwenyewe umekuja Mtwara, wamekutembeza katika barabara ile haipiti pembezoni, inapita katikati ya kila makao makuu ya Wilaya. Halafu tunatembea sisi ina makorongo, ina mashimo kila siku na si barabara ya kileo ni barabara ya zamani, kwa nini wananchi hawa wasiwekewe lami?

Kwa hiyo, mimi nasema tunataka lami na Serikali ilisema kwamba wale wa Mikoa ambayo iko karibu itakuwa inaunganishwa. Sasa kuunganishwa kuko wapi? Mnaniambia humu kama tutaweka kokoto, tutaweka na nini, tutaziba sehemu tofauti tofauti? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba kuna lugha naisikia, utasikia nyie si kuna barabara *Mtwara Corridor,* sawa iko *Mtwara Corridor,* sasa isiwe adhabu hiyo, kwa sababu *Mtwara Corridor* zinapita pembezoni. Ninachotaka niwaambie wale

ambao hawaujui Mkoa wa Mtwara umekaa kaaje. Inakubidi utoke Mpakani mwa Msumbiji halafu uchukue bidhaa, sasa wanapotuambia kwamba tufuate barabara ya *Mtwara Corridor* ina maana tupite huko pembezoni, tuiache hii barabara ya katikati ambayo ni rahisi kusafirisha mazao na kufika Makao Makuu ya Mkoa. Kwa hiyo, hii barabara bado, mimi nasikitika sana Bunge linakwisha, lakini halijaisha, watu mpo, viongozi mpo, ile barabara tunataka lami, tunataka lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzalishaji korosha, korosho ndiyo uti wa mgongo, korosho ndiyo maendeleo yetu na hatuna zao lingine tunalotegemea katika Mkoa wa Mtwara na wanaolima ni wanawake walioiweka Serikali hii madarakani. Sasa wanapata shida masoko na wanapata shida pembejeo. Hivi vitu mimi nashauri hapa kwamba hakikisheni mnaviondosha hivi vikwazo haina maana kila mwaka tunasema hilo hilo la korosho, korosho, ondosheni vikwazo. Huyu mwananchi anayezalisha ni yule yule ambaye mmemwandika kwenye takwimu kwamba anazalisha korosho ambazo ni zao la pili kuchangia Pato la Taifa na kuiingizia Serikali mapato. Sasa kama yeye ni mzalishaji wa zao la pili, bado anahangaika peke yake kule lakini tunaona raha kuandika kwenye taarifa kwamba ni zao la pili. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi/ Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, saa ya kuahirisha Bunge imefika. Kesho kama alivyoarifu Spika kutakuwa na semina asubuhi, kwa hiyo, wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha Kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 20 Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*